# Nipashe

Jumanne Septemba 17, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580025

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Askofu Mkuu Ruwa'ichi atoka ICU, alazwa wodi ya kawaida

UKURASA 3




UKURASA 13

# JPM aibua kashfa ya ununuzi wa rada

**AWASHANGAA** wahusika kutowajibika, awalipua waliofurahia ndege kushikiliwa...*Endelea Ukurasa wa 2*




Rais John Magufuli akivuta utepe kuashiria uzinduzi wa rada mbili (picha kushoto) za kuongozea ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa (KIA) katika Sherehe zilizofanyika jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Spika wa Bunge, Job Ndugai, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Hamza Johari na Balozi wa Ufaransa nchini Fredrick Clavier. **PICHA: IKULU**

## Tancoal kulipa bil. 23/- tozo

UKURASA 3

# Maofisa tisa Uhamiaji kortini tuhuma nzito

**WADAIWA** kujiingiza kwenye mitandao ya kihalifu... *Endelea Ukurasa wa 3*

**MICHEZO** YANGA WAIFUATA ZESCO MAPEMA UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# JPM aibua sakata ununuaji rada

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli ameibua upya sakata la rada baada ya jana kushangaa waliohusika katika kashfa ya ununuzi kutochukuliwa hatua yoyote, wakati waliisababishia nchi hasara kubwa.

Amesema kiongozi wa Uingereza aliyehusika katika kashfa hiyo alijiuzulu, lakini aliyehusika kwa upande wa Tanzania aliendelea kula raha.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizindua mfumo wa rada wa kuongozea ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) iliyogharimu Sh. bilioni 67.3.

Akiwa katika uzinduzi wa mfumo huo, Rais Magufuli alisema: "..Machungu ambayo tumeyapata nchi yetu, fedha zilizopangwa kununua rada mabilioni ya fedha, na hazikuwa rada nne ilikuwa rada moja nayo haikununuliwa, nayo tukapigwa".

"..Hawa (TCCA) Mamlaka ya Usafiri Anga Tanzania chini ya uongozi wa wizara na Hamza Johari zimetumika Sh. bilioni 67 kununua rada nne zinazoona nchi nzima. Zile fedha alizotaja Spika tulizopigwa sitaki kurudia kuzitaja kwa sababu zinaumiza, ilikuwa inunuliwe rada moja nayo haikufika, aliyehusika Uingereza alijiuzulu, wa kwetu Tanzania aliyehusika nina hakika hakujiuzulu, sifahamu labda atajiuzulu siku zinazokuja".

"Na inawezekana waliohusika kutupiga (walioiba fedha) kwenye ununuzi wa rada hiyo ndiyo hao hao wakosoaji wakubwa sasa hivi, wamesahau uchafu walioufanyia nchi hii," alisema Rais Magufuli.

Aliwataka Watanzania kusimamia na kulinda rasilimali za nchi na kuweka mbele uzalendo.

"Tunakusanya pesa kutoka kwa mama ntilie tukazipeleka Uingereza, tukapigwa, wa Uingereza akajiuzulu, wa kwetu akaendelea kula raha... iiiii (mshangao)... angekuwapo kwenye utawala wangu..."

"Nawashukuru sana wabunge waliokwenda kufuatilia zile pesa zetu kwa maslahi ya Watanzania akiwamo mbunge Zungu."

Rada hiyo, ilinunuliwa kutoka Kampuni ya BAE System ya Uingereza kwa Sh. bilioni 40 na hivyo kuibua mjadala mkubwa, baada ya kubainika bei hiyo ni kubwa kuliko bei halisi.

Ilinunuliwa kwa ushauri wa aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati huo, Andrew Chenge, ambaye sasa ni Mbunge wa Bariadi Magharibi (CCM) pamoja na aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu (BoT), Dk. Idrisa Rashid.

Timu ya wabunge iliyoundwa kwenda kufuatilia malipo ya rada hiyo Uingereza ni pamoja na aliyekuwa Naibu Spika, Job Ndugai, Angellah Kairuki (Viti Maalum CCM), Musa Zungu (Ilala CCM), na John Cheyo (Bariadi Mashariki), na moja ya mapendekezo yao katika ripoti waliyoiwasilisha kwa Spika wa wakati huo, Anne Makinda ni waliohusika katika kashfa hiyo wachukuliwe hatua.

**AMSIFIA MKURUGENZI**

Rais Magufuli alimwagia sifa Mkurugenzi Mkuu wa TCCA, Hamza Johari, kutokana na kufanikisha mradi wa ufungaji wa rada katika viwanja viwili vya ndege nchini.

"Safi sana, hii ndio mifano ya vijana wanaojituma. Sina zawadi ya kukupa, lakini mwaka huu, ukiamua kwenda Hijja nitakulipia ili ukamshukuru Mungu kwa utendaji wako. Johari oyee (akionyesha

INAENDELEA UK 8




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiweka jiwe la msingi la jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi mkoani Morogoro, jana. **PICHA: OWM**

# Mashinji ajitofautisha na Dk. Slaa

**Na Enock Charles**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Vincent Mashinji, ameeleza utofauti wa mazingira na nyakati kuwa ndio tofauti kubwa kati ya uongozi wake ndani ya chama hicho nchini na mtangulizi wake, Dk.Wilbrod Slaa.

Akizungumza katika mahojiano maalum na gazeti hili wiki iliyopita, Dk. Mashinji alisema wakati wa uongozi wa Dk.Slaa akiwa Katibu Mkuu wa chama hicho kikuu cha upinzani nchini, mazingira ya kisiasa yalikuwa tofauti na hata mikutano ya kisiasa iliruhusiwa tofauti na sasa.

"Kila zama na kitabu chake yule alipita kwenye mazingira ya Kikwete ambapo tulikuwa huru kufanya siasa kukimbizana nchi nzima tofauti na zama hizi," Dk. Mashinji alisema.

Akieleza zaidi Dk. Mashinji alisema kwa mazingira ya sasa, matumizi ya nguvu sio muhimu sana bali akili nyingi, busara na hekima ili kuepusha chama na hatari mbalimbali ikiwamo kufutwa au kupoteza wanachama.

Kwa sasa Dk.Slaa ni balozi wa Tanzania nchini Sweden, baada ya kuachana rasmi na chama hicho wakati wa mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Dk. Slaa alitangaza kujiweka kando siku chache kabla ya mchakato wa uteuzi wa mgombea urais wa Chadema baada ya kutofautiana na viongozi wenzake kukubali kumpokea Edward Lowassa, aliyejitoa CCM baada ya jina lake kukatwa na chama tawala kugombea kiti hicho mwaka 2015.

Akibainisha mafanikio yake katika chama hicho, Dk. Mashinji alisema anajivunia utulivu wa kisiasa na msimano wa viongozi wa ndani katika idara mbalimbali za chama hicho, akisema ni mtaji mkubwa unaowapa matumaini makubwa ya ushindi katika chaguzi.

Akizungumzia kuhusu changamoto zilizojitokeza katika ushirikiano wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), katika Uchaguzi Mkuu uliopita ambapo baadhi ya majimbo na kata walisimamisha wagombea wawili katika umoja huo, Katibu Mkuu huyo alisema wamejipanga kukabiliana na tatizo hilo katika uchaguzi wa mwakani ili kutowakanganya wananchi.

"Changamoto hiyo ilitegemewa kutokana na maandalizi ya ghafla, na kwenye watu wengi asilimia 25 ya watu wanaweza wasikubaliane na kila kitu wakati wote kwa kuwa nchi ni kubwa na watu ni wengi," Dk Mashinji alisema.

Akijibu swali iwapo baadhi ya watu watahamia katika chama hicho kwa malengo ya kugombea nafasi mbalimbali watakabiliwa na hatari ya kukatwa, Katibu Mkuu huyo alisema hapatakuwa na matabaka ya wahamiaji au wanachama asilia, ila wote watashindanishwa katika mazingira sawa na yule atakayeshinda ndie atakayepewa nafasi ya kugombea.

## ...Awalipua waliofurahia ndege kushikiliwa

**Beatrice Moses**

RAIS John Magufuli , amewashukia aliowaita wasaliti walioshangilia ndege iliposhikiliwa Afrika Kusini, hivyo amewasihi viongozi wa dini kuwaombee ili mashetani yawatoke.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa Kiwanda cha kutengeneza mabomba Vingunguti jijini Dar es Salaam, alieleza jinsi alivyoshangazwa na Watanzania walioshangilia mkasa ulioikumba ndege hiyo ambayo imenunuliwa kwa kodi za wananchi.

"Wasaliti walikuwapo tangu enzi Mungu alipoumba dunia akatengeneza malaika, wengine wakagoma ndiyo mashetani wanaotusumbua huku, kwa hiyo wapinzani hawawezi wakakosa," alisema Rais Magufuli.

"Inashikwa ndege ambayo imenunuliwa na baba yake na mama yake, yeye anashangilia anashindwa kuelewa kuwa ile ni fedha ya baba yake na mama yake, kuelewa ni kodi ya Watanzania maskini, kwa kutokujua kwa kutumiwa anashangilia afadhali imeshikwa ndege," alisema.

Aliwataka waelewe kuwa ndege siyo ya Magufuli bali ni ya Watanzania.

"Mimi nikifa leo ndege itabaki pale, inawahudumia wengine wanawahisha wagonjwa, Kigwangalla (Hamis) anaitwa waziri kwa sababu ya watalii," alisema.

"Unaweza kujua huyu amepungukiwa kichwani, siyo mtu wa kawaida amepungukiwa kichwani, wewe uwe na duka kijijini liibiwe mtoto akashangilie, utamuona huyu mtoto ana kasoro kwa hiyo wenye kasoro wapo tuwasamehe, tuendelee kuwaombea."

"Baba Askofu muendelee kuwakemea mashetani yawatoke kichwani mwao, Masheikh muwasomee dua wakatambue Tanzania ni makabila yote, vyama vyote na kwamba maendeleo hayana vyama tunataka tuitoe nchi ilipokuwa iende mahali fulani nilishawaambia hii ni donor country."

Alisema kupitia kodi za wananchi zimejengwa hospitali 352, pia Sh. bilioni 23.863 kila mwezi zinatumika kwa ajili ya kugharamia elimu ya watoto.

Alisema katika mapambano wasitegee kupendwa. Lazima kujitegemea kwa nguvu za nchi.

Awali aliwapongeza viongozi wa kampuni huyo kwa kufanikiwa kuwekeza kwa kiwango hicho ambacho kimefungua pia fursa ya ajira.

Alisema Serikali imeweka mwongozo mzuri wa upatikanaji wa malighafi zikiwamo nyingine zinazopatikana Kisarawe, huku akiwataka wawekezaji hao kuhakikisha inazingatia kiwango cha ubora wa mabomba wanayotengeneza.

Alionya pia viongozi ambao hawasimamii na kuchukua maamuzi kwa mambo muhimu hali ambayo inewuwa ikisababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi ya maendeleo nchini.

Alitaja baadhi ya miradi iliyocheleweshwa ni pamoja na kiwanda cha machinjio Vingunguti.

" Nataka mradi ukamilike haiwezekani watu wanachinjia mbuzi chini,

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Tancoal kulipa bil. 23/- malimbikizo tozo mrabaha

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

TUME ya Madini imeitaka kampuni ya kuzalisha makaa ya mawe nchini (Tancoal) kulipa mara moja malimbikizo ya tozo za mrabaha zaidi ya Sh. bilioni 23 inazodaiwa.

Katibu Mtendaji wa Tume hiyo, Prof. Shukrani Manya, alitoa agizo hilo jana wakati alipokuwa akiongea na waandishi wa habari kuwa malimbikizo hayo ni kuanzia Septemba 2011 hadi Juni 2019.

Alisema kampuni hiyo imekuwa ikikaidi kulipa mrabaha kutokana na matakwa ya kisheria huku ikitoa taarifa za upotoshaji kudai kuwa Tume imeanza kuitoza tozo ya mrabaha kwenye gharama za usafirishaji wa makaa ya mawe kutoka mgodini hadi kwa mtumiaji wa mwisho wa ndani na nje ya nchi.

Alisema katika upembuzi na uchambuzi wa takwimu wa mauzo na usafirishaji wa makaa ya mawe, imebainika kuwa Tancoal inatakiwa kulipa jumla ya Dola za Kimarekani 10,408,798 kwa kipindi hicho ambazo ni sawa na Sh. bilioni 23.

Alifafanua kuwa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kifungu cha 87(6) kinaelekeza namna ya kukokotoa mrabaha kwa kuzingatia thamani ya madini sokoni (kwa mtumiaji wa mwisho) ambayo inajumuisha gharama za usafirishaji kwa mteja na kwamba utaratibu huo umekuwa ukifuatwa na kampuni nyingine zote zinazochimba ama kuuza makaa ya mawe isipokuwa Tancoal.

"Hii kampuni inachimba makaa ya mawe kutoka mgodi wa Ngaka Ruvuma baada ya kuchimba yamekuwa yakisafirishwa hadi yadi ya Kitai na kutokea hapo wamekuwa wasafirishaji wengine ambao sasa sio Tancoal wanachukua kupeleka kwa watumiaji wa mwisho," alisema. Pia, Tancoal imekuwa ikilipa tozo ya mrabaha kwa kuzingatia thamani ya madini yakiwa yadi ya Kitai bila kujumuisha gharama za usafirishaji kwenda kwa wateja na kusababisha mvutano bila kuzingatia matakwa ya sheria.

"Kumekuwapo na mvutano kuwa mrabaha ulipwe kiasi gani na mwisho wapi, maana hawa wasafirishaji wengine wamekuwa wakitumia nyaraka za Tancoal hivyo hawawezi kujinasua, tuliunda timu na kubaini hawafuati taratibu kama zinavyosema," alisema.

Alisema pamoja na kuelimishwa mara kwa mara kuhusu namna ya kukokotoa malipo ya mrabaha kwa mujibu wa sheria imekuwa ikikaidi kulipa mrabaha kwa kuzingatia msingi huo. "Utaratibu ambao kampuni hii inautumia kwa kuwauzia wateja wa makaa ya mawe katika yadi ya Kitai badala ya kusafirisha wenyewe au kutumia wafanyabiashara wa madini walioidhinishwa unakwenda kinyume cha sheria kifungu cha 18(1)," alisema.

INAENDELEA UK 8



Dereva teksi Mousa Twaleb (wa tatu kulia), akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kesi ya kumteka mfanyabiashara Mohamed Dewji 'Mo' kuahirishwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maofisa kortini tuhuma nzito hasara Uhamiaji bil. 1/-

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MAOFISA tisa wa Idara ya Uhamiaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), wamefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi kwa tuhuma za kushiriki katika mtandao wa kihalifu na kutengeneza stika bandia za Visa 10,800 za kusafiria.

Hati ya mashtaka iliyosomwa jana mahakamani hapo na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abdalah Chavula, aliyekuwa akisaidiwa na Wakili wa Serikali Ignas Mwinuka, inadai kuwa maofisa hao wameisababishia Idara ya Uhamiaji, hasara ya Sh. 1,225,800,000.

Kesi hiyo ya Uhujumu Uchumi, namba 7 ya mwaka 2019, inasikilizwa na Hakimu Mkazi, Pamela Mazengo.

Waliofikishwa kortini ni Ofisa Mfawidhi wa Idara ya Uhamiaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Philbert Ndege (49), Beatrice Bwire (49), Deodat Furaha (43), Athanas Oyugi (40), Godfrey Kanyamwenge (40) na Juliana Mwakanemela (40).

Wengine ni wahasibu wa idara hiyo, Philbert Clemence (34), Shaame Hamad (57) na Gemina Laizer (35).

Akiwasomea makosa yanayowakabili, Wakili Chavula alidai kuwa washtakiwa hao walitenda kosa hilo ambalo ni kinyume na aya ya 4 (1) (d) cha jedwali na kifungu cha 57 (1) na kifungu cha 60 (2) pamoja na Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 ya Sheria iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Katika kosa la kwanza, mshtakiwa Ndege na wenzake wanane, inadaiwa katika tarehe isiyojulikana, kati ya Januari mosi na Agosti 2, mwaka huu, wakiwa Uwanja wa Ndege wa KIA, Wilaya ya Hai na mkoani Kilimanjaro, wakiwa ni maofisa wa Idara ya Uhamiaji, walishirikiana na watu wengine ambao hawapo mahakamani kwa makusudi kula njama za kihalifu kwa kutengeneza stika bandia 10,800 za Visa ambazo zingetumika kusafiria. Visa hizo ni za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

INAENDELEA UK 8

# Askofu Ruwa'ichi atoka ICU

**Na Mary Geofrey**

WIKI moja tangu Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Yuda Thadeus Ruwa'ichi, kufanyiwa upasuaji wa kuondoa damu iliyokuwa imevimbia kwenye ubongo, ametolewa katika chumba cha uangalizi maalum (ICU) baada ya afya yake kuimarika na kuhamishiwa katika wodi ya kawaida.

Ofisa Uhusiano wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Patrick Mvungi, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, alisema jopo la wataalam saba wanaomtibu Askofu Ruwa'chi ndilo liliamua kumhamisha kutoka chuma cha ICU baada ya kujiridhirisha na maendeleo yake.

Jopo la wataalamu hao saba wanaomfanyia uchunguzi kiongozi huyo wa kanisa ni pamoja na madaktari bingwa watatu wa magonjwa ubongo, dawa za usingizi na magonjwa ya ndani, walaamu wa lishe, wauguzi wabobezi na wataalam wa mazoezi tiba.

"Jopo hilo limefanya maamuzi hayo leo (jana) saa 2:00 asubuhi baada ya kufanya tathmini ya vipimo pamoja na taarifa mbalimbali za maendeleo ya Askofu Ruwa'ichi tangu alivyopokelewa na kufanyiwa upasuaji hapa MOI Septemba 9, mwaka huu," Mvungi alisema.

Alisema MOI itahakikisha kuwa Kiongozi huyo wa Kanisa Katoliki, anapatiwa matibabu na kurudi katika hali yake ya kawaida kwa ajili ya kuendelea na majukumu yake ya kila siku.

"Taasisi ya MOI inawahakikishia Watanzania wote hususani waumini wa Kanisa Katoliki kwamba Askofu Ruwa'ichi yupo salama na afya yake imeimarika sana, hivyo waendelee kumuombea ili arejee kwenye majukumu yake," Mvungi alisema.

Septemba 9, mwaka huu, Askofu Ruwa'ichi alifanyiwa upasuaji wa kuondoa damu iliyokuwa imevimbia kwenye ubongo, ugonjwa unaotambulika kwa jina la 'Chronic Subdural Haematoma'.

Alianza kusumbuliwa na ugonjwa huo kisha kufanyiwa upasuaji ukiwa mwezi mmoja baada ya kushuka wadhifa huo, kufuatia mtangulizi wake, Muadhama Polycarp Kardinali Pengo kung'atuka Agosti 15, mwaka huu baada ya Kiongozi wa Kanisa hilo duniani, Papa Francisko kuridhia ombi lake.


Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

NAFASI ZA KAZI

MWANDISHI WA HABARI WA KUJITEGEMEA

Gazeti la Nipashe linatangaza nafasi kwa Mwandishi wa habari wa kujitegemea kutoka mikoa yote nchini.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

1. Awe amefanyakazi angalau miaka mitatu (3) kwenye chombo cha habari
2. Ajue misingi, miiko na maadili ya uandishi wa habari
3. Awe mwenye kujituma na mbunifu katika kutafuta habari

Mwombaji awasilishe maombi yake kupitia barua pepe **nipashe.gazeti@gmail.com**

*Mwisho wa kutuma maombi ni Septemba 30*

615421902

# Wanafunzi 2 waongezwa kesi mauaji ya mwenzao

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

WANAFUNZI wawili wa Sekondari ya Katoro Islamic iliyoko Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, wameongezwa katika mashtaka ya mauaji ya mwanafunzi mwenzao Mud Muswadiku aliyekuwa kidato cha nne shuleni hapo.

Kuongezwa kwao kunafanya idadi ya wanafunzi wanaokabiliwa na mashtaka ya mauaji, yaliyofikishwa mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Bukoba, Flora Kaijage, kufikia sita.

Wengine wanaokabiliwa na mashtaka hayo ambayo yamesomwa jana katika mahakama hiyo ni mwalimu wa Katoro Islamic Majaliwa Abdul (35) na mlinzi wa shule hiyo Badru Issa Tibagililwage (27), ambapo kuongezwa kwa wanafunzi hao wawili kumefanya idadi ya washtakiwa wote katika kesi hiyo namba 18 ya mwaka 2019 kufikia wanane.

Walioongezwa ni Sharif Amri (19) na Fahad Abdulraziz (20), huku wenzao waliofikishwa mahakamani awali wakiwa ni Husama Ramadhan (17), Sharif Huled (19), Hussein Mussa (20) na Abdalah Juma (19).

Akizungumza baadha ya kuahirishwa kwa kesi hiyo, wakili wa serikali Haruna Shomary, alisema kuwa upelelezi unaendelea na kuwa wanafunzi walioongezwa upelelezi unaonyesha kuhusika kwao katika tukio hilo, lililotokea Aprili 14 mwaka huu.

"Leo kuna wanafunzi wengine wawili tumewaongeza, awali walikuwa washtakiwa sita sasa jumla wamekuwa wanane, upelelezi wa kesi hii unaendelea maana kuna masuala bado hayajakamilika," alisema Shomary.

Hata hivyo, mmoja wa washtakiwa hao ambaye ni mwalimu wa shule hiyo Majaliwa Abdul alinyanyua mkono mahakamani na kuomba mambo matatu likiwamo la mahakama kuwapatia hati ya mashtaka, upelelezi kufanyika haraka ili ikibainika kuwa wanafunzi hao hawana hatia waachiwe na kwenda kuendelea na maandalizi ya kufanya mtihani wa taifa wa kidato cha nne.

Aidha, alitoa ombi la tatu la kuwaruhusu wanafunzi hao kupatiwa vitabu na madaftari yao ili waendelee kujisomea wakiwa gerezani.

Akijibu maombi hayo wakili wa serikali Shomary alisema kuwa kuhusu hati ya mashtaka watapewa maana ni haki yao na kuruhusiwa au kupata vitabu na madaftari ili kujisomea wakiwa mahabusu suala hilo liko katika mamlaka ya gereza na kuwataka kuwasiliana na uongozi wa gereza la Bukoba.

Upelelezi wa kesi hiyo unaendelea na imehirishwa jana hadi Septemba 30 mwaka huu, itakapotajwa tena.

Septemba 2 mwaka huu, wanafunzi wane , mwalimu pamoja na mlinzi wa shule hiyo walifikishwa mahakamani na kusomewa mashtaka ya mauaji ya mwanafunzi mwenzao Mud Muswadiku, waliyemshambulia baada ya kumtuhumu kuwa anajihusisha na ngono za jinsia moja.

## MNH yawezesha wagonjwa 10 kusikia

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imewasha vifaa vya kusaidia kusikia 'Cochlear implant' kwa wagonjwa 10 wakiwamo watoto tisa na mtu mzima mmoja.

Mkurugenzi Huduma za Upasuaji, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Sufiani Baruani, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa MNH, Prof. Lawrence Museru jana, alisema watoto waliozaliwa wakiwa hawana uwezo wa kusikia sasa wanaweza kusikia kufikia asilimia 100 baada ya kuwashiwa vifaa hivyo.

Alisema pia kiwango cha madaktari wa ndani kufanya upasuaji kimefikia asilimia 90 tofauti na awali walikuwa wakishirikiana na wataam wa nje ya nchi.

"Baada ya upasuaji watoto hawa husubiri kipindi cha mwezi mzima ili waweze kuwashiwa vifaa husika. Katika kuwasha vifaa hivi, tulikua tukitegemea pia watalaam kutoka nje, lakini kwa sasa tunafurahi kuwa eneo hilo nalo tayari tumeliweza kwa asilimia 100 na leo tutafanya wenyewe bila kusaidiwa," Dk. Buruani alisema.

Alisema katika watoto hao tisa waliowashiwa vifaa hivyo jana wametoka mikoa ya Tanga, Ruvuma na Kilimanjaro. Dk. Baruani alisema, tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo nchini Juni, 2017, wagonjwa 30 walipandakizwa vifaa hivyo kati yao, watoto ni 29 na mtu mzima mmoja.

Alisema serikali imetumia Sh. bilioni 1.1 kuhudumia wagonjwa 30 kwa gharama ya Sh. milioni 37 kwa mgonjwa mmoja.

Alisema kama wagonjwa wangeenda nje ya nchi ingegharimu Sh. bilioni tatu sawa na Sh. milioni 100 kwa kila mgonjwa hivyo kuokoa Sh. milioni 1.89.

"Huduma hii imekuwa ikitolewa kwa kushirikiana na madaktari bingwa wa upasuaji kutoka nchini Misri na mwanzoni watalaam wazalendo walikua wakisaidia, lakini hivi sasa watalaam wanafanya wenyewe kwa asilimia 90," Dk. Baruani alisema.

Alisema upandikizaji wa wagonjwa 30 uliofanyika ndani ya miezi 26 ni sawa na asilimia 60 ya wagonjwa 50.

"Hospitali ya Taifa Muhimbili, inapenda kuufahamisha umma kuwa hakuna mgonjwa atakayekosa huduma hii kutokana na kutokuwa na fedha kwa kuwa kuna utaratibu wa kutoa huduma kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kifedha," alisema Dk. Baruani. Naye Daktari Bingwa wa Masikio, Pua na Macho, Shaban Mawala, alisema tatizo la usikivu linaongezeka katika jamii kama ilivyo kote duniani.

Alisema utafiti na makadirio ya MNH, unaonyesha kuwa kwa mwaka takribani watoto kati ya 200 watahitaji huduma hiyo nchini.

"Utaalamu ambao umeendelezwa takribani miaka 20 ya karibuni unaonyesha kuwa watoto hawa wakigundulika mapema na kuwekewa vifaa vya usikivu wataishi kama kawaida, wakati wasipopata huduma hii watakuwa viziwi," Dk. Malawa alisema.



Waisai Wambura (wa pili kushoto aliyekaa), akifurahi baada ya kuwashiwa kifaa alichopandikizwa (cochlear implant) na kusikia tena upya sauti, wakati wa mkutano na waandishi wa habari, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), jijini Dar es Salaam jana. Wambura alipoteza uwezo wa kusikia ukubwani sasa anaweza kusikia tena. Wa pili kulia waliokaa ni Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji Hospitali hiyo, Dk. Sufiani Baruani. **PICHA: MARY GEOFREY**

# TZ kati ya 10 barani Afrika kunufaika EU

**Na Romana Mallya**

TANZANIA ni miongoni mwa nchi 10 barani Afrika zinazonufaika na mpango mkakati mpya wa tatu Afrika wa Umoja wa Ulaya na Ushirikiano wa Ufalme Hispania uliolenga kusaidia sekta ya maji, afya na uwekezaji wa viwanda mbalimbali.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam wakati wa mazungumzo baina ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Prof. Palamagamba Kabudi na Mkurugenzi Mkuu wa Afrika wa Wizara ya Mambo ya Nje Umoja wa Ulaya na Ushirikiano wa Ufalme Hispania, Raimundo Rubio, aliyeambatana na Balozi wa Hispania nchini Tanzania, Fransisca Petros.

Prof. Kabudi alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi 10 ambazo zimeingia kwenye mpango huo ambao utekelezaji wake ni wa miaka mitatu.

"Hispania imepiga hatua katika nyanja tofauti, tumewaomba waje kuwekeza kwenye sekta ya viwanda vya dawa, utalii na kuimarisha uhusiano katika nyanja ya elimu kwa sababu wao ni daraja kati ya Ulaya na Afrika," alisema.

Alisema mkurugenzi huyo amekuja Tanzania kuitembelea kwa sababu ni moja ya nchi zilizo kwenye mpango huo wa kusaidia katika sekta ya maji, afya na uwekezaji wa viwanda mbalimbali ili kuimarisha uhusiano zaidi.

"Hispania ilianzisha uhusiano wa kibalozi na Tanzania mwaka 1967 ilikuwa ni miongoni mwa nchi za Ulaya ikiwa na ushirikiano mkubwa na Tanzania.

"Katika mpango huu, Hispania imeweka mkazo mkubwa katika eneo la maji na utasaidia miradi ya maji katika Wilaya ya Mbozi na miradi ya maji katika vijiji 12 katika kata za Malangali na Logoyonzi mkoani Iringa.

Prof. Kabudi alisema Hispania katika sekta ya afya itaisaidia Tanzania ujenzi wa vituo vya afya na hospitali.

"Hispania imekuwa ikiwekeza na itaendelea kuwekeza Tanzania katika eneo la utalii. Hii ni moja ya nchi iliyopiga hatua katika eneo la utalii inapokea watalii wengi kutoka Ulaya. Tutashirikiana nao katika eneo hili na maeneo mengine kama viwanda vya madawa ambako wenzetu wako mbali," alisema.

Pia alisema Hispania ni wapenzi wakubwa wa mpira hivyo kwa ushirikiano uliopo wanaamini wataimarisha sekta ya michezo nchini.

"Tumeomba siyo tu tushirikiane katika matangazo ya michezo, tupate watawala wa michezo, kocha ili kabumbu letu liwe la viwango vya La Liga," alisema.

Prof. Kabudi alisema mazungumzo waliyofanya jana ni ya mwanzo na kwamba mkurugenzi huyo amekuja akipita kwenye nchi za kipaumbele ili kuona jinsi gani wataimarisha ushirikiano huo.

Naye, Rubio alisema mpango huo utakuwa ukipitiwa upya baada ya miaka mitatu na kuzitaja nchi nyingine wanufaika kuwa ni Afrika Kusini, Angola, Ethiopia, Ghana, Ivory Coast, Kenya, Nigeria, Msumbiji na Senagal.

Kuhusu bajeti ya kutekeleza mpango huo, alisema Umoja wa Ulaya umetenga Euro bilioni 44 kwa nchi hizo za kimkakati.



# Mimba, utoro, vyakosesha 35 mtihani darasa la saba

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

WANAFUNZI 35 hawakufanya mtihani wa darasa la saba katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji kutokana na mimba, utoro na vifo.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Elimu wa Shule za Msingi Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Mtauka Richard, alisema wanafunzi watoro ni 28, mimba sita na kifo mmoja.

Richard alisema wanafunzi watoro 28 ambao wametokea katika Shule za msingi Mgumile mwanafunzi mmoja, Benjamini Mkapa wanne, Kieba mmoja, Bushabani wawili, Buronge watatu, Kagera mmoja, Gungu watatu, Mwanga watatu, Kabingo mmoja, Majengo mmoja Airpoti sita, Businde mmoja na kilimahewa mmoja, hivyo jumla ni wanafunzi watoto 28.

Alisema wanafunzi waliopata mimba ni sita ambao wametokea katika Shule za msingi Benjamini Mkapa watatu, Kibirizi mmoja, Bushabani mmoja na Businde mmoja hivyo jumla sita. Mmoja aliyefariki ni katika Shule ya Msingi Airport.

Aidha, alisema utoro ndiyo umechukuwa nafasi kubwa sana katika Manispaa hiyo na juhudi ambazo wanazifanya kwa sasa ni kuwaelimisha wazazi na walezi juu ya elimu kwa watoto wao, Kamati ya shule pamoja na vikao vya shule.

Alisema hatua ambazo watazichukua kwa ajili ya wanafunzi ambao watapata mimba wazazi pamoja na walezi wao watapelekwa polisi ili hatua kali za kisheria zichukue mkondo wake.

Alisema tatizo kubwa ni wazazi kumalizana nyumbani pindi watoto wao wanapopata mimba, hivyo tatizo haiwezi kuisha kama wazazi hawatakuwa na ushirikiano na polisi ili kuwabaini watu ambao wanawapa wanafunzi mimba.

Aidha alisema wazazi na walezi ambao watoto wao watashindwa kuhudhuria masomo wazazi hao watapelekwa kwenye mabaraza ya kata au Polisi kwa ajili ya hatua zaidi.

Aliwataka wazazi na walezi kuacha tabia ya kuwaruhusu watoto wao kwenda kufanya biashara ya ndogo kwenye masoko ya usiku ya kuuza ndizi, nanasi, mifuko, sabuni za gwanji na mchicha ili kudhibiti utoro shuleni.

# Ndugai azindua harambee utanuzi wodi St. Lukes

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amezindua harambee ya kuchangia ujenzi wa wodi ya mama na mtoto katika kituo cha afya cha St. Lukes kilichopo wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma na kutoa wito kwa taasisi na wadau mbalimbali kujitokeza kusaidia ujenzi huo.

Akizungumza mara baada ya kuongoza maandamano yaliyofanyika jijini Dodoma ya kuchangia ujenzi wa wodi hiyo ya kisasa, Ndugai alisema Kanisa la Anglikana ni miongoni mwa taasisi ambazo zimekuwa zikichangia kutoa huduma ya afya kwa wananchi hivyo ni vyema taasisi, wadau kujitoa kwa hali na mali katika kufanikisha ujenzi huo.

" Nitoe rai kwa wadau, taasisi pamoja na mtu mmoja mmoja kuunga mkono maono haya ya kanisa Anglikana ya kuboresha huduma za afya, sio tu katika kituo cha St Lukes, lakini pia hapo baadaye ya kuweza kujenga hospitali kubwa ya rufaa itakayotoa huduma za kibingwa na kipekee kwa wangonjwa wa kansa

"Jambo hili likikamilika huko mbele, litakuwa lenye baraka na huduma kubwa kwa watu wetu ambao wanahangaika sana kwa ajili ya matibabu ya kansa ambayo ni ghali na nadra kupatikana katika maeneo yetu."

Naye Mganga Mkuu Kituo cha Afya cha St. Lukes, Dk. Edwin Kiula, alisema kituo hicho kina idara tano ikiwamo idara ya uzazi salama na mtoto ambazo utolewa bila malipo kama inavyoelekezwa kwenye mwongozo uliotolewa na serikali.

Alisema takwimu za miaka mitatu za kituo hicho, zinaonesha wangonjwa wa nje waliotibiwa katika kituo hicho ni takribani 8,000 kwa mwaka huku waliofika kwenye kliniki ya mama na mtoto ni 18,000 kwa mwaka.

Dk. Kiula alisema wakina mama waliojifungulia katika kituo hicho ni 400, waliofanyiwa upasuaji mkubwa ambao ni wadharura ni 250 na waliolazwa kwa mwaka ni watu 500.

"Kituo kina uhitaji mkubwa wa ongezeko ili kufikia mahitaji yaliyopo sasa, azima yetu ni kufanya upanuzi wa kituo cha afya kwa kujenga wodi yenye vitanda 40 lengo ni kufikia vitanda 60, kutoka vitanda 20 vilivyopo sasa ili kufikia mahitaji ya sasa."

Naye Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mpwapwa, Jacob Chimeledya, alisema kanisa limekuwa likitoa huduma ya afya kwa wananchi ikiwa ni kufuata nyayo za Yesu ambaye alifanya kazi tatu za kuhubiri, kufundisha na kuponya watu.

Uzinduzi huu wa Dodoma sasa utafuatiwa na harambee kubwa ambayo itafanyika jijini Dar es Salaam tarehe itakayotangazwa baadaye na kuongozwa na Rais mstaafu, Jakaya Kikwete.

# Watuhumiwa zaidi utekaji wa 'Mo' Dewji wasakwa

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi inayomkabili dereva taksi mkazi wa Tegeta, Mousa Twaleb (46) ya uhujumu uchumi ikiwamo kusaidia kutendeka uhalifu, kutakatisha Sh. milioni nane na kumteka Mohamed Dewji maarufu kama 'Mo' umedai kuwa bado unaendelea kuwatafuta watuhumiwa wengine wanne kwa ajili ya kuwaunganisha katika kesi hiyo.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa, na kwamba bado upande wa Jamhuri unaendelea na juhudi za kuwatafuta watuhumiwa wengine.

Alidai kuwa upande wa Jamhuri unaomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa tena Septemba 30, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Awali, Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi, alidai kati ya Mei Mosi na Oktoba 10, 2018 mahali tofauti jijini Dar es Salaam na jijini Johannesburg, Afrika ya Kusini, kwa makusudi alisaidia utendaji makosa ya jinai kwa nia ya kujipatia fedha.

Shtaka la pili, ilidaiwa Oktoba 11, 2018 katika hoteli ya Colloseum iliyopo Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa akiwa pamoja na wenzake ambao hawapo mahakamani walimteka Mo kwa nia ya kumuhifadhi kwa siri.



Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 249 cha kanuni ya adhabu cha 16 kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2002 kilichotumika kufungua shtaka ya kumteka Mo endapo mshtakiwa atakutwa na hatia atahukumiwa kwenda jela kutumika kifungo cha miaka saba.

Ilidaiwa katika shtaka la tatu Julai 10,2018 eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam mshtakiwa alitakatisha Sh. 8,000,000 huku akijua zimetokana na genge la uhalifu wa makosa ya kupanga.

Hakimu alisema mshtakiwa hatakiwi kujibu chochote kwa sababu mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Teknolojia hii ni mafanikio makubwa*

**KWA** miongo mingi tatizo la nyanda za malisho na ukosefu wa majani kwa mifugo nchini, limekuwa kubwa na kusababisha watu kupoteza maisha na mali.

Maisha, wanyama na mazao yalipotea kwenye migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji maeneo mengi nchini.

Kiini cha mgogoro ni ardhi, wafugaji hawana sehemu ya kulisha mifugo hivyo kuvamia mapori na hata kulazimika kulisha wanyama masuke mashambani muda mfupi baada ya mavuno ya wakulima.

Ni jambo la kuipongeza serikali kwa kuwa tatizo hilo sasa linaelekea kupata ufumbuzi wa kudumu baada ya kugundulika teknolojia mpya ya kisasa ya uzalishaji wa nyasi za mifugo.

Watafiti wanathibitisha kuwa kama ikitumiwa ipasavyo itamaliza changamoto ya ukosefu wa nyanda za malisho, nyasi za kulisha mifugo changamoto iliyotokana na kukosekana nyanda za malisho kwa miongo mingi.

Kwa mujibu wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (Taliri), mkoani Tanga, wasomi hawa wamegundua teknolojia hiyo na mbinu za usambazaji wa nyasi hizo na mbegu zake, lengo ni kuondokana na uhaba wa malisho.

Tunaipongeza Taliri kwa juhudi hizo za kuzalisha majani hayo ambayo yatawezesha kupata chakula cha mifugo kwa muda wote wa mwaka na cha kutosha.

Tunaamini kuwa tatizo la mifugo kufa kutokana na ukame litamalizika baada ya kupatikana nyasi hizo.

Tunapongeza hatua ya Taliri kwa kuwa upatikanaji wa vyakula vya uhakika vya mifugo na vyenye virutubisho utaongeza ubora na ladha ya nyama na maziwa ya Tanzania.

Tunaona ni jambo la kujivunia kwa sababu mifugo ya nchi hii ilikosa ubora kutokana na kukosa chakula au lishe bora.

Wanyama kama ng'ombe, mbuzi na kondoo walilazimika kutembea maelfu ya kilometa kutafuta nyasi na hata kula udongo na miti mikavu kwa kukosa chakula.

Hongera Taliri Tanga na wataalamu wanaohusika na mradi huo na tunachowaomba sasa ni maofisa ugani kuandaa mashamba darasa, mbegu, kuzisambaza na kuwafundisha wafugaji namna ya kuzalisha na kuyatumia majani hayo.

Kutokana na migogoro ya wakulima na wafugaji ujio wa nyasi hizo unatoa ufumbuzi wa kudumu ili kupatikana mafanikio, tunaishauri serikali izitambue na kuziwekea mipaka sehemu au nyanda za malisho ili kupanda majani hayo.

Kuna madai kuwa maeneo mengi ya wafugaji yapo jirani na hifadhi za taifa na mara nyingi yamekuwa yakitwaliwa au kuchukuliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Kutokana na madai hayo tunazishauri Wizara za Utalii na Mifugo kuangalia namna ya kuwarudishia wafugaji maeneo watakayoona yanafaa ili kuwe na sehemu ya kupanda malisho hayo na kuwe na majini ya kutosha muda wote.

Kupatikana kwa nyanda hizo kutaokoa sekta ya mifugo na kuondoa shida ya malisho ambayo imelitatiza taifa na kusababisha hasara nyingi ikiwamo vifo na uharibifu wa mali.

Tunawapongeza Taliri kwa kuwa wameondoa maafa kama vifo vilitokea kwa sababu ya mapigano baina ya wakulima na wafanyakazi wakigombea ardhi kwenye maeneo mengi mathalani, mikoa ya Morogoro na Pwani.


Kwa mujibu wa maelezo ya wataalamu hao malisho ya majani yataifanya mifugo kuwa na afya bora na kuongeza uzalishaji wa maziwa, nyama na ngozi bora.

Habari njema ni kwamba aina hiyo ya malisho ina sifa ya kustawi hata maeneo yenye ukame na kwamba wanaweza kupanda malisho hayo kwa mwaka mzima.

Tunaomba pia tafiti ziendelee zaidi ili kupata nyasi zenye maji mengi na kupunguza tatizo la maji ambalo pia ni changamoto kwa mifugo mingi nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Raphael Kibiriti

# *Wazazi/walezi, wanafunzi kutofanya mitihani kwa utoro hakukubaliki*

**MTIHANI** wa kumaliza darasa la saba ulifanyika wiki iliyopita kwa siku mbili mfululizo kuanzia Septemba 11 na kumalizika Septemba 12, ambapo jumla ya wanafunzi 947, 221 kutoka shule 17,051 za Bara, walitarajiwa kufanya mitihani hiyo.

Kwa mujibu wa Baraza la Mitihani la Taifa (Necta), wavulana waliotarajiwa kufanya mitihani hiyo walikuwa 451,235 sawa na asilimia 47.64, huku wasichana wakiwa 495,986, sawa na asilimia 52.36.

Muungwana anapongeza kwa ujumla kumalizika vyema mitihani hiyo bila ya kasoro kujitokeza na kuripotiwa, kama ilivyowahi kutokea huko nyuma kwenye mitihani ya kitaifa.

Kwa mfano mwaka jana, mitihani ilidaiwa kuvuja kwenye shule 11 za binafsi ikiwa ni pamoja na shule zote wilayani Chemba, hali iliyosababisha kufutwa kwa matokeo ya shule hizo na wanafunzi kurudia mitihani.

Wakati Muungwana akipongeza kazi nzuri ya wadau wote wanaowajibika katika suala zima la usimamizi wa mitihani wakiongozwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Necta kwa kumalizika kwa amani mitihani hiyo, amekwaza kidogo na taarifa iliyotolewa karibuni na Mkoa wa Dar es Salaam.

Kupitia kwa Ofisa Elimu wa Mkoa huo, Hamis Lissu, imeripotiwa kwamba jumla ya wanafunzi 618 wa darasa la saba walishindwa kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali zikiwamo za utoro, vifo na ugonjwa.

Lissu akabainisha kwamba katika idadi hiyo, wavulana walikuwa 385 na wasichana 233, na kati yao wanafunzi ambao hawakufanya mtihani huo kwa sababu ya utoro ni 557.

Ukiacha sababu za wale walioshindwa kufanya mtihani huo kwa sababu ya kupoteza maisha ambao walikuwa 22, wagonjwa 20 na sababu zinginezo ikiwamo ya kifungo 19, Muungwana, amevutika zaidi kuwazungumzia hao 557 ambao hawakufanya mitihani kwa sababu ya utoro.

Kimsingi idadi hiyo ni kubwa sana ukichukulia kuwa ni ya mkoa mmoja tu wa Dar es Salaam, kabla ya kuvinjali idadi ilivyo katika mikoa mingine nchini.

Kwa mujibu wa Lissu, wanafunzi 618 ambao hawakufanya mtihani huo ni sawa na asilimia 0.82, kwa maana kuwa jumla ya wanafunzi 75, 495 walisajiliwa kufanya mtihani huo katika Jiji la Dar es Salaam, lakini waliofanya ni 74,877.

Sasa twende kimahesabu na tuchukue takwimu hizi za mkoa wa Dar es Salaam za asilimia 0.82 za ambao hawakufanya mtihani huo kama kipimo chetu kwa nchi nzima.

Itabainika kwamba kwa wanafunzi 947,221 kutoka shule 17,051 za Bara waliotarajiwa kufanya mitihani hiyo, utakuta takribani wanafunzi 7,767 hawakufanya mtihani huo kwa nchi nzima kwa kipimo hicho cha asilimia 0.82 cha Jiji la Dar es Salaam, sababu kubwa ikiwa ni utoro.

Idadi hiyo ni kubwa kwani ni sawa na kuzungumzia takribani shule nane za msingi, zenye wanafunzi 1,000 kuanzia la kwanza hadi la saba.

Kwa ujumla suala la utoro halipaswi kuwapo katika zama hizi, iwapo wazazi na walezi watachukua nafasi zao za kimalezi kwa watoto wao.

Ni bahati mbaya kwamba kuna wazazi, na walezi ambao hawafanyi inavyopaswa katika suala zima la kufuatilia mahudhurio ya watoto wao shuleni na namna wanavyoendelea na masomo.

Wazazi/walezi wa aina hii ndio ambao hawajui kama watoto wao wanakwenda shule, kama wamepewa mazoezi ya nyumbani, hawajui mahitaji yao, kama kuna mikutano ya wazazi, hawana muda na maendeleo ya watoto wao shuleni.

Kwamba yote wameacha mikononi mwa walimu na matokeo yake ndiyo hayo ya kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi watoro mpaka wanashindwa kufanya mitihani ya kitaifa.

Muungwana anawaasa wazazi na walezi kuchukua wajibu wao wa kuhakikisha watoto wanahudhuria shule ili kuondokana na tatizo la utoro kiasi cha baadhi ya wanafunzi kutofanya mitihani ya kitaifa kama ilivyobainishwa na Ofisa Elimu wa Jiji la Dar es Salaam.

## BARUA / MJADALA

# *Wakati umefika kwa Malamba Mawili kuwa na kituo cha polisi*

***NDUGU Mhariri** pole na majukumu ya kila siku kwa ujenzi wa taifa letu changa, na pia ninashukuru kupata nafasi katika gazeti lako ili niweze kutoa dukuduku langu.*

*Kwanza kabisa mimi ni mkazi wa Malamba Mawili, jijini Dar es Salaam, eneo hili linakabiliwa na ukosefu wa huduma mbalimbali za muhimu ikiwa ni pamoja na kituo kidogo cha polisi.*

*Tulikuwa tukitegemea kituo cha polisi cha Kwa Yusuf kilichokuwa kando ya barabara ya Morogoro, eneo la Mbezi Mwisho, umbali wa zaidi ya kilometa mbili kutoka Malamba, lakini kimehamishiwa mbali zaidi baada ya bomoabomoa iliyofanyika kando ya barabara hiyo.*

*Kutokana na hali hiyo, tumejikuta tukiwa mbali zaidi na huduma za polisi, hivyo tukikumbwa na matatizo ambayo yanahitaji msaada wao inawezekana ikawa vigumu kuwapata kwa wakati kwa sababu ya umbali.*

*Kwa hali hiyo ndugu Mhariri, naomba zifanyike jitihada za makusudi za kuhakikisha eneo hili linapata huduma za polisi kuliko kutegemea maofisa wa polisi wale wa doria tu, ambao inawezekana likatokea tukio wakati hawapo eneo hili.*

*Nakumbuka sisi wakazi wa eneo hili tulikutana kwa ajili ya mkakati wa kutafuta eneo ambalo linaweza kutolewa ili kujenga kituo kidogo cha polisi ambapo eneo lilipatikana, lakini masharti yakawa ni magumu, hivyo ikashindikana kuwezesha ujenzi wa kituo hicho.*

*Kuna mtu alijitolea kutoa eneo, lakini ikaelezwa katika kikao kwamba siku hizi ili kujenga kituo cha polisi ni lazima eneo la kiwanja liwe kubwa, hivyo mpango wa ujenzi ukawa umeishia hapo kimsingi pamoja na mtu huyo kuwa tayari kutoa eneo lake.*

*Malamba Mawili kwa sasa imepanuka sana inahitaji kuwa na huduma hiyo, hivyo tunaomba ufanywe utaratibu ambao utasaidia kupata eneo la kutosha ili sisi wananchi tuchangie ujenzi.*

***Mkazi Malamba Mawili_Dar***




# TRA, Nida mnakwama wapi?

**Na Salome Kitomari**

VITAMBULISHO muhimu kwa ajili ya Mtanzania kupata huduma mbalimbali kwenye taasisi au kokote ndani na nje ya nchi, ni vile vinavyotambulika kitaifa.

Vitambulisho hivyo ni pasi ya kusafiria ambayo si Watanzania wote wanaweza kuipata kwani ili uwe nayo ni lazima kuwe na sababu ya kuwa nayo, ikiwamo ya safari za nje ya nchi.

Lingine ni kwamba, kitambulisho hicho kinapatikana kwa gharama kubwa na kwa sasa ili upate hati hiyo ni lazima ulipie Sh. 150,000, huku kukiwa na utaratibu mrefu wa kufuata mpaka ukaipate hati hiyo.

Kitambulisho kingine ni cha mpigakura ambacho kimsingi kinatumika maeneo mengi, na upatikanaji wake si mgumu kwani kila aliyeandikishwa kwenye daftari la kudumu la wapigakura, anacho.

Aidha, kutokana na maboresho yanayoendelea kwenye maeneo tofauti nchini, kila aliyepoteza au kuharibikiwa na kitambulisho chake atapata kingine.

Hata hivyo, katika sehemu tofauti za kiutendaji nchini, kitambulisho cha mpigakura kimekataliwa na baadhi ya taasisi, zikiwamo za watoa huduma za simu, ambao wanataka kitambulisho cha taifa kwenye usajili wa 'line' au kuwa wakala wa fedha mtandaoni.

Kwa mfano, ili upate pasi ya kusafiria ni lazima uwe na kitambulisho cha uraia au namba ya uraia, ambayo hutolewa baada ya kupitia mchakato wa kuomba na kusubiri kupatiwa kitambulisho.

**Kuonyesha kuwa upatikanaji wa vitambulisho vya utaifa ni changamoto kubwa, mamia ya wananchi wamejikuta wana namba za uraia, lakini hawana vitambulisho na kila wakifuatilia, wanaambiwa kuwa bado havijatengenezwa.**

Kutokana na hali hiyo, kila mwananchi analazimika kuwa na kitambulisho cha uraia, lakini mamlaka inayotoa huduma ya vitambulisho hivyo haijulikani imekwama wapi.

Mjadala unasema hivyo kutokana na ukweli kwamba kila siku kuna ahadi za maboresho za kuwezesha vitambulisho hivyo vya taifa vipatikane.

Kuonyesha kuwa upatikanaji wa vitambulisho vya utaifa ni changamoto kubwa, mamia ya wananchi wamejikuta wana namba za uraia, lakini hawana vitambulisho na kila wakifuatilia, wanaambiwa kuwa bado havijatengenezwa.

Hilo linafanyika pamoja na ukweli kwamba wakati mwananchi anapoomba kitambulisho hicho anaambiwa asubiri miezi mitatu, lakini kinachoshangaza ni kutopata kitambulisho hata baada ya miezi hiyo mitatu aliyoahidiwa kufika, na baadhi ya wananchi wakisubiri kwa zaidi ya miezi sita. Wanabaki wakitembea na namba ya uraia.

Ukija kwenye suala la upatikanaji wa leseni za udereva, nako ni shughuli nyingine nzito.

Kwamba madereva wengi wamejikuta wanatembea na karatasi na stakabadhi za kuonyesha kuwa wamelipia leseni mpya, lakini bado hawajapatiwa leseni husika.

Kwa ujumla si Nida wala Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), waliojitokeza hadharani kueleza ni kwanini kumekuwa na mkwamo katika upatikanaji wa nyaraka hizi muhimu.

Kwa umuhimu wa kitambulisho cha utaifa, ilitarajiwa wananchi wavipate mapema ili waendelee na shughuli zao za maendeleo, lakini wamejikuta wameachwa hewani wasijue lini hasa watapata nyaraka hizo muhimu.

Je, Nida na TRA wanakwama wapi kutoa vitambulisho hivyo muhimu? Ndiyo swali mjadala unajiuliza.

Unajiuliza hivyo ikitiliwa maanani kwamba, kukosekana kwa vitambulisho hivyo kunachelewesha maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Hiyo ni kwa sababu mwenye kitambulisho cha taifa moja kwa moja anaweza kusajili shughuli zake za kibiashara, kama wakala wa huduma zile za fedha mtandaoni.

Lakini kwa kukosa kitambulisho hicho anajikuta hawezi kufanya hivyo jambo ambalo ni kikwazo kwa maendeleo yake binafsi na uchumi wa nchi yake kwa ujumla.

Ni vyema Nida ikaeleza kwa uhakika inachukua muda gani mtu kupata kitambulisho cha taifa, lakini la muhimu zaidi ihakikishe watu wanapata vitambulisho kwa wakati uliopangwa na si kuwa na danadana nyingi ambazo zinazalisha mazingira yasiyoridhisha.

Aidha, mjadala unaigeukia TRA vilevile ukiuliza, inakwama wapi kwenye kutoa leseni?

Unauliza hivyo kwa sababu mtu anapofika katika ofisi za mamlaka hiyo atakuta kuna watu wengi wamekwenda kupata leseni mpya, lakini wote hupewa karatasi na kuahidiwa kupigiwa simu, lakini hupita miezi zaidi ya sita wakati mwingine kabla ya kupigiwa simu.

Hii si sahihi kwa sababu kwa tafsiri ya haraka, dereva anaweza kumaliza mwaka hajakamata leseni mkononi mwake, na kawaida leseni ya udereva huwa ni ya miaka mitano, hivyo kubakisha miaka minne ya uhai wa leseni hiyo.

Ni maoni basi ya mjadala kwa mamlaka hizi zihakikishe Watanzania wenye sifa wanapata kwa wakati nyaraka hizi muhimu kwa ustawi wao binafsi na taifa kwa ujumla wakati tukielekea kwenye Tanzania ya viwanda na ya kipato cha kati ifikapo 2025.

**KABWELA** NA FADHIL MOHAMMED




**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU
mhariri@nipashe.co.tz

# JPM aibua sakata ununuaji rada

INAENDELEA UK 2

kumshangilia). Kwa kweli wewe ni Johari kweli nasema kwa dhati bila unafiki nilifuatilia utendaji wake wa kazi yupo vizuri. Unamuona mtu anazungumza pointi ningekuwa na binti ningekupa ukaoa," alisema Rais Magufuli.

Alisema Johari alipoingia madarakani makusanyo TCCA yalikuwa ni Sh. bilioni 40 na sasa yamefikia Sh. bilioni 71.

Pia, Rais Magufuli alisema umuhimu wa rada siyo tu kuongozea ndege bali hata kuimarisha usalama wa nchi.

"Wote mnafahamu nchi yetu ina mipaka ya aina tatu, ardhini, majini na angani. Na mipaka yote hii lazima tuilinde, lakini huwezi kulinda anga kama huna rada."

Kabla ya kutekeleza mradi huo, Rais Magufuli alisema kulikuwa na rada moja ya kiraia iliyokuwa na uwezo wa kuona asilimia 25 pekee ya anga, asilimia 75 ilikuwa haiwezi kuona.

Alisema mradi huo utavutia mashirika ya ndege kuleta ndege zao, kuongeza idadi ya watalii, kuongezeka kwa idadi ya ndege katika anga la Tanzania na kuongezeka mapato, kuokoa gharama za fedha zilizokuwa zinalipwa kwa nchi jirani.

Naye, Mkurungezi Mkuu wa TCCA, Johari alisema gharama za ujenzi wa mradi huo ni Sh. bilioni 67.3 kati ya hizo Sh. bilioni 35.1 (asilimia 55) zilitolewa na serikali na Sh. bilioni 32.1 (asilimia 45) zilitolewa na TCCA.

"Eneo la kwanza ni shughuli zilizofanyika Ufaransa na Uingereza, zikihusisha uundaji mitambo, majaribio ya kiwandani na kusafirisha mitambo kuja nchini. Nyingine ni mafunzo kwa wahandisi na waongozaji ndege walioyapata nchini Ufaransa na Chuo cha kuongezea Ndege cha Afrika Kusini huku wataalam 53 wakipata mafunzo hayo kati yao 12 ya ukufunzi," alisema Johari.

Alisema shughuli zilizofanyika nchini ni ujenzi wa majengo katika kituo cha Dar es Salaam, Mwanza na Kilimanjaro na usimikaji wa mitambo kwenye vyumba vya kuongozea ndege ambao umeshakamilika.

Alisema mradi huo ulihusisha kuunganisha mfumo unaooanisha mifumo mingine ya kusimamia anga iliyopo na mfumo wa ukokotoaji wa ankara.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Dk. Fatma Mganga (katikati), akiongoza matembezi ya hisani kuchangia utanuzi wa Kituo Cha Afya Cha St Lukes Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma. Matembezi hayo yalifanyika jijini Dodoma na baadaye Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuzindua harambee ya kuchangia ujenzi huo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# ...Awalipua waliofurahia ndege kushikiliwa

INAENDELEA UK 2

ndiyo tatizo la Dar es Salaam, Coco Beach, tulisema pajengwe Vingunguti ameisikia muda mrefu, mkuu wa mkoa.

"Tumebembelezana sana karibu miaka 60 tukibembelezana sana hatutafika, ndiyo mambo hayaendi, mfukuze aje mwingine tupo milioni 45," alisema.

"Mimi nabembeleza,Waziri mkuu huwa habembelezi anafyatua tu, sisi ni dhamana wananchi waliotupigia kura wanafuatilia na watahoji tumefanya nini," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Sadiq Murad, aliwataka wafanyabiashara waache kulalamika kwa Rais mambo madogo madogo, mengine washirikishe kamati hiyo itasaidia katika kupata ufumbuzi, pia wawe waaminifu katika shughuli zao za biashara.

Mkurugenzi mwenza wa Kampuni ya Piper Industry Ltd, Seif Ali Seif, akizungumza kwa niaba ya wenzake alimpongeza Rais Magufuli kwa juhudi anazofanya katika kukuza uchumi wa nchi kupitia viwanda, na kuwa inawatia moyo.

"Ujenzi wa kiwanda hiki wa hatua ya kwanza umegharimu Sh. biloni 120, ujenzi umekwenda sambamba na dira ya kusambaza majisafi na salama ifikapo 2025," alisema Seif.

Alisema upatikanaji wa gesi nchini na mafuta ndiyo iliyowachochea kuanzisha tani 25,000 za mabomba PVC na kwa mwaka, lakini kwa sasa inazalisha tani 8,000 pekee kutokana na soko, imeajiri wafanyakazi 215 ikikamilisha ujenzi wa awamu ya pili itaongeza idadi yao itafikia 500.

# Tancoal kulipa bil. 23/- malimbikizo tozo mrabaha

INAENDELEA UK 3

Alibainisha kuwa kifungu hicho kinakataza mtu au kampuni yoyote isipokuwa mmiliki halali wa leseni ya madini au mfanyakazi wa wamiliki wa leseni hizo, kumiliki kusafirisha au kuuza madini bila kuwa na kibali cha kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria.

Prof. Manya alisema timu maalum iliyoundwa kwa ajili ya kuhakiki deni la mrabaha unaojumuisha usafirishaji wa makaa ya mawe kwa kipindi hicho ilibaini kampuni hiyo inadaiwa kiasi hicho cha fedha.

"Tancoal inatakiwa kulipa USD 1,103,594 ikijumuisha na adhabu ya asilimia 50 kwa kipindi cha Septemba 2011 hadi Juni 2014. Tancoal inapaswa kulipa USD 9,305,205 ikijumuisha adhabu ya asilimia 50 kwa kipindi cha Julai hadi Juni 2019, hivyo jumla ni USD 10, 408, 798," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Prof. Idris Kikula, alisema uamuzi huo ni kwa mujibu wa sheria hivyo kampuni hiyo ilipe mara moja madeni hayo kabla sheria kali hazijachukuliwa dhidi yake ikiwamo kushtakiwa.

Aliwaonya kutoongeza bei ya makaa hayo kwa sababu Tume imeweka bei elekezi ya madini yote na hutolewa kila mwezi.

"Wasichukue sababu hii ya kudaiwa wakaongeza bei tunawaonya tutawachukulia hatua. Tulitaka deni juzi liwe limelipwa kwa maana kwamba mapema, sasa wao watatuomba kama hiyo hela wataka walipe kwa awamu tutakubali, lakini waje tukubaliane hatuwalazimishi kulipa kwa mkupuo," alisema.

Aliagiza makubaliano ya ulipaji yawe kwa kipindi kifupi isifike miaka 10.


**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
16/09/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMANNE tarehe 17/09/2019 kampuni ya TARIMO REMI STANSLAUS** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MONDULI kuelekea MOSHONO, na kutoka MOSHONO** kuelekea **SAKINA** gari hilo lenye namba za usajili: **T155BJM/T916DCG.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 17.50**
   **Upana - mita 3.28**
   **Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika **MONDULI** hadi **MOSHONO** kupitia **MBAUDA ,FILIPS** na kurudi **SAKINA** kupitia FILIPS gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115421802



**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
16/09/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO** tarehe 18/9/2019 kampuni ya **LOGISTICS FOR SUB SAHARA** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TUNDUMA kuelekea MTUKULA** kupitia MIKUMI, gari hilo lenye namba za usajili zenye vipimo vyake:

   **TRUCK NO. 240 SSC FS / 262 SSC FS**
   ***VIPIMO: UREFU 22 UPANA 3.75***
   ***KIMO 4.75***

2. Gari hizo zinatoka **TUNDUMA kuelekea MTUKULA kupitia MIKUMI. Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115421702


# Maofisa kortini tuhuma nzito hasara Uhamiaji bil. 1/-

INAENDELEA UK 3

Kosa la pili ni kuisababisha hasara mamlaka, kinyume na aya ya 10 (1) ya jedwali na kifungu cha 57 (1) na kifungu cha 60 (2) pamoja na Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 ya Sheria iliyofanyiwa marejeo, mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa wa kwanza na wenzake wanane, walisababisha hasara ya Sh. 1,225,800,000.

Wakati kosa la tatu ni kudurufu malighafi za kutengenezea hati za kusafiria, bila kuwa na kibali cha mamlaka, jambo ambalo ni kinyume na kifungu cha 19 (2) cha Sheria ya Pasipoti na Nyaraka za Kusafiria, namba 20 ya mwaka 2002.

Pia katika tarehe isiyojulikana kati ya Januari mosi na Agosti 2, 2019, katika Uwanja wa Ndege wa KIA, kwa pamoja na bila kibali cha mamlaka, walidurufu stika za Visa bandia 10,800.

Kosa la nne ni utakatishaji wa fedha ambalo ni kinyume na kifungu cha 12 (c) na 13 (a) cha Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu, namba 12 ya mwaka 2006, ikisomwa pamoja na aya ya 22 ya jedwali na kifungu 57 (1) na 60 (2) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 ya sheria iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Kosa la tano ilidaiwa ni kutakatisha fedha, huku wakijua ni kosa kisheria, wakati kosa la sita ni kutengeneza stika bandia 10,800 za Visa, huku wakijua ni kosa.

Hata hivyo, maofisa hao walikana makosa yote na Hakimu Mkazi, Mazengo alisema kwa kuwa kesi hiyo haina dhamana, washtakiwa wataenda kukaa mahabusu hadi itakapotajwa tena Septemba 30, mwaka huu.

**Wakati kosa la tatu ni kudurufu malighafi za kutengenezea hati za kusafiria, bila kuwa na kibali cha mamlaka, jambo ambalo ni kinyume na kifungu cha 19 (2) cha Sheria ya Pasipoti na Nyaraka za Kusafiria, namba 20 ya mwaka 2002.**

**HABARI MIKOANI**

# Majaliwa: Tatizo la barabara Ifakara-Mlimba kuwa historia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema changamoto ya barabara ya kutoka Ifakara hadi Mlimba iliyokuwa inawakabili wananchi wa maeneo hayo kwa muda mrefu imepatiwa ufumbuzi baada ya serikali kupanga kuijenga kwa kiwango cha lami.

Amesema serikali imedhamiria kuboresha miundombinu ya barabara nchini ikiwamo barabara ya kutoka Ifakara hadi Mlimba yenye urefu wa kilomita 126.5.

Waziri Mkuu aliyasema hayo juzi, wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye uwanja wa Matangini, Mlimba wilayani Kilombero.

"Serikali imedhamiria kuimarisha barabara katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Ifakara-Mlimba kwa kiwango cha lami, lengo likiwa ni kurahisisha usafiri pamoja na kukuza uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla."

Alisema serikali inatambua umuhimu wa barabara hiyo kwa ajili ya kuboresha maendeleo ya wananchi na kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami, hivyo aliwataka wananchi hao waendelee kuiamini serikali yao.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu alimwagiza Kaimu Ofisa Elimu Mkoa wa Morogoro, Jackson Mpankuli, ahakikishe amepeleka walimu katika Shule ya Msingi Matangini na Mwangaza ambazo zinakabiliwa na upungufu wa walimu.

Waziri Mkuu alisema hadi Septemba 30, mwaka huu, kiongozi huyo awe ameshawahamishia walimu katika shule husika. Waziri Mkuu alitoa agizo hilo baada ya Mbunge wa Jimbo la Mlimba, Suzan Kiwanga kulalamikia upungufu wa walimu hao.

Mbunge huyo alisema katika jimbo kuna tatizo kubwa la upungufu wa walimu hali inayosababisha baadhi ya wazazi kukodi walimu kwa ajili ya kuwafundisha watoto wao, hivyo Waziri Mkuu aliagiza walimu wahamishiwe katika shule ndani ya wiki mbili.

Akizungumza na wananchi katika eneo la Mchombe alipokuwa njiani kuelekea Mlimba, Waziri Mkuu aliwataka wazazi, walezi na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro kuhakikisha wanadhibiti ongezeko la mimba kwa watoto wa shule.

"Lazima kuwalinda watoto wa kike ili wasipate mimba kwani watashindwa kuendelee na masomo, hivyo watashindwa kutimiza ndoto zao. Viongozi simamieni utekelezaji wa sheria kwa kuwachukulia hatua wote waliowapa mimba wanafunzi."

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Mbunge wa Jimbo la Kilombero, Lijualikali na Mbunge wa Mlimba, Suzan Kiwanga waliiomba serikali iwasaidie ujenzi wa barabara za kutoka Ifakara hadi Mlimba na barabara ya Ifakara hadi Kidatu ambayo ujenzi wake unasuasua.

Pia Suzan aliishukuru serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwa barabara ya Ifakara-Mlimba na baadaye kuwekwa lami kwa awamu na kusema kuwa serikali ya awamu ya tano ikiahidi kitu inatekeleza.

Waziri Mkuu anaendelea na ziara yake ya kikazi mkoani Morogoro, ambapo anatarajiwa kutembelea Halmashauri za Wilaya ya Ulanga na Malinyi kukagua miradi ya maendeleo ukiwamo mradi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya na kuzungumza na wananchi pamoja na watumishi.



Mitungi ya gesi ya kuchomelea ikiwa jirani na kibanda cha mamalishe ambaye anatumia moto wa mkaa kuandaa chakula cha wateja wake, katika Mtaa wa Bandi katikati ya Jiji la Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari endapo utatokea mlipuko. **PICHA: JOHN BADI**

# Adha ya wananchi, mifugo kusombwa na maji yaisha

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

WANANCHI wa kata za Kinamapula na Bulugwa katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameondokana na tatizo la watu na mifugo kufa maji kwa kusombwa na mto Mgaya baada ya kukamilika kwa daraja lililogharimu Sh. milioni 575.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kwandikwa, ambaye ni mbunge wa jimbo hilo, alisema wakati wa masika watu na mifugo wamekuwa wakipoteza maisha kwa kusombwa na maji ya Mto Mgaya, hivyo serikali iliiona tatizo hilo na iliamua kuondoa changamoto hiyo kwa kutoa fedha ambazo ziliwezesha ujenzi wa daraja hilo.

Hayo yalibainika mwishoni mwa wiki wakati Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Mibara Ndirimbi, alipokuwa akifanya ukaguzi wa barabara na daraja hilo.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wengine mkazi wa kijiji cha Mgaya, Juliana Ngombe, alisema kujengwa kwa daraja na barabara hilo kumewafurahisha na kuwatia moyo kila mwaka watu na mifugo waliokuwa wanakufa kwa kusombwa na mto huo.

"Kwa mwaka jana watu wawili walipoteza maisha kwenye mto huu, hali inayonifanya kila uchao nije kuliangalia daraja hili lililomaliza watu tangu ujenzi wake ulipoanza mpaka linamalizwa kujegwa," alisema Juliana Ngombe.

Petro Majebele, mkazi wa kijiji cha Butibu Kata ya Kinamapula, alisema tangu kuanzishwa kwa kijiji hicho, hakukuwa na barabara kutoka Butibu kwenda Mgaya, bali kulikuwa na kinjia tu cha watembea kwa miguu, na ilikuwa iwatuchukua saa zaidi ya sita kutoka Butibu Mgaya kwenda Bulugwa, lakini kwa sasa tunatumia saa moja.

Mhandisi Ndirimbi alisema daraja la Mgaya lipo mpakani mwa Kata za Kinamapula na Bulugwa na ujenzi wa daraja hilo umegharimu Sh. milioni 575 ikiwa ni pamoja na barabara ya kilometa nane, makaravati tisa, na ujenzi huo umechukua siku 180 mpaka kukamilika.

# Exim kuhamasisha matumizi ya huduma salama za kifedha

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania imezindua kampeni maalum inayolenga kuhamasisha wateja wake kuhusiana na matumizi ya mtiririko wa huduma maalumu za kiusalama kwenye masuala ya fedha zinazotolewa na benki hiyo.

Kupitia mtiririko huo imebainishwa kuwa wateja wa benki hiyo, wanapata huduma mbalimbali ikiwamo huduma ya usafirishaji wa fedha kwa usalama, huduma ya kiusalama ya malipo, huduma za kisasa za hundi, pamoja na huduma ya kuweka pesa kwenye akaunti ya benki hiyo, wakati wowote kwa kutumia mashine ya kuwekea fedha.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo uliofanyika jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Masoko na Uhusiano wa benki hiyo, Stanley Kafu, alisema kupitia huduma hizo wateja wa benki hiyo hawahitaji tena kupanga foleni kwenye matawi ya benki hiyo, ili kupata huduma za kifedha au hata kuhofia muda wa kufungwa kwa huduma za benki hiyo kwa kuwa wanaweza kupata huduma wakiwa kwenye maeneo ya kazi.

"Huduma hizi ni sehemu ya mkakati wa benki ya Exim Tanzania kutoa huduma kwa wateja bila kubanwa na muda wa kazi au umbali wa kijiografia," alisema Kafu.

Akifafanua kuhusu huduma ya usafirishaji wa fedha kwa usalama, Kafu alisema inamwondolea mteja hatari ya kuibiwa, kuvamiwa, kunyang'anywa pesa wakati anazitoa ofisini kwake kupeleka benki kwa kuwa atapatiwa huduma ya kusafirisha fedha hizo kuelekea na kutoka benki kwa kutumia usafiri maalumu ukiwa na walinzi wenye mafunzo maalum ya kulinda fedha.

Aidha, akizungumzia huduma ya 'corporate cheque capture' Kafu alisema huduma hiyo inayotumia 'scanner' inamwezesha mteja kuweka hundi zake (deposit cheque) wakati wowote bila kutembelea tawi lolote la benki.

**"Huduma hizi ni sehemu ya mkakati wa benki ya Exim Tanzania kutoa huduma kwa wateja bila kubanwa na muda wa kazi au umbali wa kijiografia," alisema Kafu.**

0000

# Upasuaji mkubwa kuanza Novemba hospitali rufani

**Na Happy Severine, SIMIYU**

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Simiyu ambayo kwa sasa inatoa huduma za wagonjwa wa nje tu, itaanza rasmi kutoa huduma za upasuaji mdogo na mkubwa Novemba mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Matoke Muyenjwa, alisema wana uhakika wa zaidi ya asilimia 100 kuwa huduma hizo zitaanza kutolewa muda huo.

Alisema tangu hospitali hiyo imeanza kufanya kazi baada ya kuzinduliwa na Rais John Magufuli ikiwa ni mwaka mmoja umepita, wamekuwa wakitoa huduma za wagonjwa wa peke yake.

"Wananchi wameendelea kuteseka na kutumia gharama kubwa kufuata huduma hizo mkoani Mwanza na mikoa mingine, baada ya majengo yetu kukamilika ya maabara, mionzi na upasuaji tutatoa huduma hizo hapa hapa," alisema Dk. Muyenjwa.

"Tunawahakikishia wananchi wa mkoa wetu hospitali hii inaenda kuwa mkombozi kwao na kuwapunguzia gharama, Novemba tunaanza rasmi, tayari tumeanza maandalizi ya vifaa tiba vyote vinavyohitajika zikiwamo mashine za upasuaji mkubwa na madaktari bingwa wapo wa kutosha," aliongeza Dk. Myunjwa.

Alisema ujenzi wa majengo hayo upo katika hatua za mwisho, ambapo alibainisha wamedhamiria hospitali hiyo kutoa huduma za kibingwa kutokana na kuwapo kwa madaktari bingwa wote huku wengine wakimalizia masomo yao.

"Kuanza kutolewa kwa huduma za upasuaji mkubwa na mdogo itapunguza kwa zaidi ya nusu ya rufani za wagonjwa kwenda Hospitali ya Bugando, tunao madaktari wa kutosha na wenye uzoefu, lakini wapo waguzi zaidi ya 60," alisema Dk. Muyenjwa.

Alieleza kuwa katika kuadhimisha mwaka mmoja wa hospitali hiyo tangu kuanza kazi, walifanya kampeni ya kutoa huduma za vipimo vya virusi vya homa ya ini pamoja na magonjwa yasiyoambukizwa.

Alisema katika huduma hiyo wananchi wengi walijitokeza ambapo watu 257 walipimwa na 33 waliopimwa virusi vya homa ya ini ni mmoja tu aliyekutwa na virusi hivyo huku 60 wakikutwa na tatizo la uzito uliopitiliza.

Janeth John, mmoja wa wananchi walioshirikia zoezi hilo, aliushukuru uongozi wa hospitali hiyo kwa vipimo na ushauri, ambapo alisema imesababisha atambue tatizo lake na kupewa ushauri pamoja na dawa.



Mbunge wa Iramba Magharibi, Mwigulu Nchemba, akizungumza na wananchi akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua shughuli za maendeleo na utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi, katika jimbo lake, mkoani Singida wikiendi. **PICHA: INNOCENT NATAI**

## AAR yatoa ushauri nasaha, kupima afya mawakala bure

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya kutoa bima ya afya Tanzania, AAR imewapima na kuwapa ushauri nasaha mawakala wao jijini Dar es Salaam ikiwa kama njia ya kuimarisha uhusiano wao.

Vipimo vilivyotolewa ni pamoja na kipimo cha sukari, shinikizo la damu, uwiano wa uzito na urefu huku wakiwapatia ushauri nasaha wa ustawi kama jinsi ya kukabiliana na msongo wa mawazo, lishe bora, utumiaji sahihi wa fedha pamoja na maradhi ya homa ya ini.

Meneja Masoko na Mauzo wa AAR Insurance Tanzania, Tabia Massudi, amegundua kuwa mawakala wao wanauhitaji wa elimu juu ya kutunza afya zao za mwili na akili kwa uboreshaji bora wa maisha yao na biashara.

Alisema: "Tukiwa kama wadau wakuu wa afya nchini tunaamini ni jukumu letu kuwapa wadau wetu taarifa sahihi na msaada wa matibabu ambao utanufaisha afya zao za mwili na akili."

"Tunatambua nafasi kubwa ya mawakala katika ukuaji wa bima ya AAR, hivyo tunalo jukumu la kujali afya zao na ndio maana leo tumetumia nusu ya siku kufanya zoezi hili sio tu katika kuwahimiza kuangalia afya zao mara kwa mara, lakini pia kuwapa mwongozo juu ya afya ya akili," alisema mwishoni mwa wiki.

Mmoja wa mawakala ambaye alipokea ushauri nasaha na kupata vipimo kutoka kampuni hiyo ya bima, Dk. Sara Nyero kutoka ARIS, alitoa shukurani kwa kampuni hiyo, huku akiwapongeza AAR kwa huduma zao za ustawi wa mfanyakazi.

"Kwa niaba ya mawakala wenzangu ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa kampuni ya bima ya AAR kwa ushauri nasaha na huduma zote za afya walizotupatia, tumejifunza vitu vingi sana ambavyo vitatusaidia sana katika kulinda afya zetu za mwili na akili.

"Ningependa pia kuwapongeza kwa hatua hii ya kuonyesha kutujali sisi kama mawakala wao...hii itasaidia kuimarisha uhusiano wetu na AAR na kutufanya kuwa mabalozi wazuri wa huduma yao ya ustawi wa mfanyakazi," alisema.

# Wanahabari wajikita elimu ya TB

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

KLABU ya Waandishi wa Habari Pemba (PPC) katika mwendelezo wake wa kutoa elimu ya kifua kikuu kwa jamii kisiwani Pemba, imegundua jumla ya watu 20 wanaougua TB kati ya watu 375 waliochunguza afya zao kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu.

Mratibu wa klabu hiyo, Mgeni Kombo Khamis, alisema kwa kipindi hicho wameshatoa elimu ya TB kwa watu 6,467 kupitia kila shehia.

Alisema wakati wanaendelea kutoa elimu hiyo kwa wananchi na kuwahamasisha wapime afya zao, waligundua watu 20 wenye ugonjwa wa TB kisiwani Pemba kati ya 375 waliochunguzwa.

"Klabu ya waandishi wa habari Pemba kwa kushirikiana na kitengo cha homa ya ini, ukoma, kufua kikuu na Ukimwi tunaendelea kutoa elimu kwa jamii na tunapomaliza mkutano tu watu wanakuja kupima, wengine wanatufuata ofisini kwa siku nyengine," alisema Mratibu.

Alisema wameshazifikia shehia 13 kisiwani Pemba, visiwa vinne, madago mawili, masoko matatu, dahalia tano, nyumba ya kurekebisha tabia (Sober House) moja.

"Tayari tumeshakwenda kutoa elimu ya TB kwenye visiwa vya Kojani, Makoongwe, Mwambe Shamiani na Kisiwa Panza, hii ni kuhakikisha tunawaibua wenye ugonjwa huu wapate tiba mapema," alisema.

Akizungumzia kuhusu mabadiliko kwa shehia na sehemu wanazotoa elimu ya TB, mratibu huyo alisema yapo makubwa, kwani kwa sasa watu wamehamasika na kushawishika kwenda kupima afya zao kwa wingi.

"Zamani wakati tunapita kwenye mashehia kutoa elimu ya TB watu walikuwa hawataki kupima, lakini kwa sasa tunashukuru wanakuja na wanatoa ushirikiano mkubwa," alifafanua.

Mgeni aliishauri jamii kuwa tayari kuchunguza afya zao, ili kupata tiba mapema kwa yule ambaye atagundulika, kwani TB ipo na inaambukiza.

"Jamii ni muhimu kuchunguza afya zenu, ili koitokomeza TB, matibabu yapo na dawa zipo zinatolewa bure mahospitalini na kwenye vituo vya afya," alisema.

Aidha, aliwashauri waandishi wa habari watoe elimu ya TB kwenye vyombo vyao, kwani ni jukumu lao kuielimisha jamii, jambo ambalo litasaidia sana kuwafikia wanajamii wengi kwa muda mfupi.

Mradi wa kuelimisha jamii kuhusu TB unatekelezwa na PPC kwa kushirikiana na kitengo shirikishi cha homa ya ini, ukoma, kifua kikuu na Ukimwi chini ya Ufadhili wa Mfuko wa Fedha ya Dunia (Global Fund).

# Kituo chatoa mafunzo kupambana na ukatili

**Na Allan Isack, ARUSHA**

KITUO cha utetezi wa haki za watoto na kinamama (CWCD) Mkoa wa Arusha, kimetoea elimu ya kuzuia ukatili dhidi ya mtoto kwa madereva bodaboda kwa lengo la kushiriki mapambano ya ukatili dhidi ya watoto yanayoendelea kushika kasi nchini.

Akizungumza wakati wa semina ya viongozi wa makundi mbalimbali ya Chama cha Waendesha pikipiki mkoani hapa (Uwapa), Mkurugenzi wa Kituo hicho, Hindu Mbwego, alisema shirika hilo limeamua kuunga mkono juhudi za serikali kuhakikisha watoto wote wanaotakiwa kusoma wanakuwa shuleni kutokana na serikali kugharamikia fedha kwenye shule ili watoto wasome.

Alisema mila potofu kwa kutokujua sheria na haki za watoto zimekuwa zikichangia ukatili dhidi ya watoto kwani jamii imekuwa ikikiuka haki hizo kwa kufanya matendo ya ubakaji, ukeketaji na kuwafanyisha kazi ndio maana wameamua kuwatumia madereva bodabada kuunga juhudi za serikali kupinga ukatili dhidi ya watoto.

Alisema madereva bodaboda ni mabalozi wazuri kama watatumia vyema mafunzo hayo, yatasaidia kuondoa ukatili dhidi ya mtoto kwani madereva hao wapo kwenye maeneo mengi katika jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha DC, Dk. Willson Mahera, alisema serikali itahakikisha kila mtu anaishi kwa amani, huku akiishukuru taasisi hiyo kwa kuandaa mpango wa kutoa mafunzo kupitia makundi mbalimbali ya kijamii.

"Napenda kuishukuru sana taasisi hii kwa kuandaa mpango huu wa kutokomeza ukatili dhidi ya watoto ambao umekuwa ukishika kasi siku hadi siku," alisema Mahera.

Mwenyekiti wa Uwapa, Godlight Rugemalira, alisema mafunzo hayo yametolewa wakati mwafaka kwao na yatawasaidia kuondoa changamoto ambazo baadhi ya madereva bodaboda wamekuwa wakituhumiwa kushiriki kufanya vitendo hivyo.

Alisema wamekuwa wakikutana na vitendo hivyo, maeneo mbalimbali na sasa wataweza kutoa taarifa kwa mamlaka husika. Baadhi ya madereva bodaboda walioshiriki mafunzo hayo walisema mafunzo hayo yamewajengea uelewa wa kupinga vitendo vya ukatili kwa watoto vinavyofanywa na baadhi ya madereva bodaboda, ubakaji na uendeshaji usio salama.



Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo (katikati), akikagua ujenzi wa makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, yanayojengwa Kata ya Dongobesh juzi. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Chelestino Mofuga. **PICHA: GIFT THADEY**

# Waziri: Serikali imejipanga kubadili mfumo wa utafiti

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto, imejipanga kuwa na mfumo mmoja wa takwimu za utafiti wa magonjwa ya binadamu ili kuondoa mkanganyiko wa takwimu na taasisi zingine za serikali.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk. Faustini Ndungulile, alisema hayo mwishoni mwa wiki jijini Arusha, wakati akifungua kongamano la udhibiti wa maambukizi ya ugonjwa wa Ukimwi lililoshirikisha taasisi za utafiti zikiwamo NIMR, AMREF, PERFAR pamoja na wadau wa masuala ya Ukimwi.

Ndugulile alisema kumekuwapo na takwimu tofauti tofauti ambazo zinachanganya watu na kushindwa kuelewa takwimu ni zipi ni za kweli kuhusu maambukizi mapya ya ugonjwa huo wa Virusi vya Ukimwi (VVU).

Aidha, alizitaka taasisi hizo za utafiti kutumia mfumo wa serikali kwa ajili ya kutoa taarifa sahihi kwenye jamii.

Alisema kuwa taasisi hizo, zimekuwa zikikusanya takwimu na kuzipeleka kwenye mashirika ya nje ya kimataifa bila idhini ya serikali na wanafahamu fika kufanya hivyo ni kinyume cha sheria kwani takwimu hizo ni mali ya serikali.

Hata hivyo, alisema zipo takwimu za utafiti nyingi zilizofanyika, lakini hadi sasa hazijafanyiwa kazi na hazijaisaidia serikali kutatua baadhi ya changamoto badala yake zimekuwa zinatumika kutolea taarifa kwenye makongamano tu .

Alizitaka taasisi hizo, kuweka utaratibu mzuri usiokinzana na mfumo wa serikali wa utoaji taarifa ambapo alisema kuanzia sasa lazima taasisi zote zinazojihusisha na utafiti wa Ukimwi zishirikiane na taasisi ya utafiti wa magonjwa ya binadamu, NIMR, ambayo itakuwa ikiratibu tafiti hizo na kuziingiza kwenye mfumo mmoja wa serikali.

Alisema serikali imefanya maboresho mengi ikiwamo kuwa na mfumo mmoja wa takwimu, kuongeza muda wa kuchukua dawa za kufubaza makali ya Ukimwi kutoka miezi mitatu hadi sita, kutoa dawa kinga kwa makundi maalumu yakiwamo wanaotumia dawa za kulevya, wanaofanya mapenzi ya jinsia moja na kwa wanawake wanaojiuza. Alisema serikali imejipanga kutekeleza malengo ya maendeleo ya kimataifa hadi kufikia mwaka 2030 maambukizi ya VVU yawe yametokomezwa.

Alisema hadi kufikia malengo ya kimataifa, wamejipanga kutekeleza lengo la kupima watu kwa asilimia 90 ambao watakao kuwa na maambukizi, na asilimia 90 nyingine ni kwa wale wanaotakiwa kupima afya zao pia asilimia 90 kwa wagonjwa wanatakiwa kutumia dawa.

Ndugulile alisema kwa mujibu wa itafiti, asilimia 40 ya mabinti nchini wana maambukizi ya ugonjwa wa Ukimwi hivyo, serikali hivi karibuni itaweka sheria inayoruhusu mtu binafsi kujipima mwenyewe maambukizi ya virusi vya ukimwi.

Aliongeza kuwa katika utafiti uliofanywa hivi karibuni umebaini kuwa wanaume ni wagumu sana kujitokeza kupima afya zao na pindi wanapojitokeza wanakuwa hawazingatii matumizi ya dawa tofauti na wanawake.

Aliagiza kupanuliwe wigo wa kushirikisha wadau wengi kwenye makongamano ya ukimwi ili kurahisisha kujadili matokeo ya sera.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Juma Nkamia, alisema pamoja na kazi nzuri inayofanywa ya kupunguza maambukizi ya VVU,

alidai lugha inayotumika sio rafiki kwa kuwa mabango yameandikwa kwa lugha ya kigeni ambayo kwa wananchi inakuwa ni ngumu kuielewa.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa magonjwa ya binadamu, Profesa Yunusi Mgaya, alisema mkutano ni wa kwanza kufanyika nchini ambao unashirikisha wataalamu wa utafiti, wahadhiri pamoja na wadau ili kuweka mpango mkakati wa pamoja wa kutokomeza maambukizi mapya hadi kufikia mwaka 2030.

## Wakulima 15,000 kunufaika pampu za umwagiliaji

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WAKULIMA zaidi ya 15,000 wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Singida, huenda wakaondokana na adha ya kusubiri kilimo cha msimu wa mvua baada ya kampuni ya IYO ya jijini Arusha, kuanza kusambaza pampu za umwagiliaji maji, zenye kutumia mwanga wa jua katika maeneo mbali mbali ya mikoa hiyo.

Mkurugenzi wa Masoko na Uendeshaji wa Kampuni ya IYO Solar Pump Group, Abdull Sariko, alisema Bodi ya Wakurugenzi ya kampuni hiyo, imelenga zaidi kumkomboa mkulima wa hali ya chini, kulima kisasa kwa kutumia pampu ya jua katika umwagiliaji shambani na gharama yake ni nafuu na imemlenga mkulima wa hali ya chini kabisa.

Sariko alisema uwezo wa pampu ni mkubwa, kwani ina uwezo wa kusambaza maji lita 40,000 na kilio cha wakulima kutegemea mvua kwa sasa, itakuwa historia na nchi itakuwa na mavuno ya kutosha ya chakula, katika maeneo mbalimbali ya mikoa hiyo na mingine nchini.

Alisema kwa sasa kampuni imejikita katika mikoa hiyo kaskazini, lakini lengo ni kutaka kusambaa mikoa mbalimbali nchini, ikiwa ni njia mojawapo ya kuisaidia serikali katika kuboresha kilimo nchini kuwa cha kisasa.

"Tumeshasambaza hizi pampu katika wilaya za Same, Mwanga, Simanjiro, Arumeru na Singida, na mahitaji ni makubwa sana na tutajitahidi kukidhi mahitaji hayo bila ya wasiwasi," alisema Sariko.

Obed Mawalla, alisema ameshanunua pampu hiyo na ameipeleka kijijini Marangu mkoani Kilimanjaro na inafanya kazi vizuri, ambapo mahindi na migomba imenawili tofauti na awali, alikuwa akitegemea mvua.

Mawalla alisema pampu hizo ni mkombozi wa mkulima, kuacha kutegemea mvua na zitamfanya mkulima kulima kila wakati kwa kutumia pampu hiyo. Elias Qarro, mkazi wa Karatu aliitaka serikali kuipa nguvu kampuni hiyo, ili iweze kusambaza pampu hizo kila wilaya zote nchini, ili ziweze kuwasaidia wakulima katika kilimo cha kisasa kuliko

## CCM yashauriwa usimamizi uchumi

**Na Mary Mosha, SAME**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri (Uwekezeji), Angellah Kairuki, amekitaka Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Same kuhakikisha pamoja na kufanya kazi za siasa, wanapaswa kusimamia ukuzaji wa uchumi wa wilaya hiyo.

Kairuki aliyasema hayo wakati akikabidhi vyerehani 45, kwa Jumuiya za Wazazi, Jumuiya ya Wanawake (UWT) na Jumuiya ya Umoja wa Vijana (UVCCM).

Kila jumuiya ilipewa vyerehani 15 na Chama Cha Mapinduzi (CCM), vyerehani 10.

Alisema ili kufanya siasa endelevu zitakazosaidia kukisimamisha chama ni lazima kuweka misingi ya kujitegemea pamoja kusimama kiuchumi.

"Vyerehani hivi tulivyovitoa leo ni utekelezaji wa uwekezaji kwa njia ya vitendo katika kuhakikisha kila jumuiya inaweza kujitegemea kiuchumi, ambapo utawasaidia katika chaguzi za serikali za mitaa unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwaka huu," alisema huku akiongezea kuwa:

"Hatutakuwa tayari kumvumilia mtu yeyote atakayeharibu au kufanya ubadhirifu kwa rasilimali zilizotolewa. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria na taratibu."

Alisema mashine hizo zinaweza kutumika kama kiwanda kidogo kitakachoweza kubadilisha maisha ya vijana wengi kwa kufika hapo na kupata mafunzo yatakayowawezesha kujitegemea katika kujiajiri.

"Kama mtapata zabuni ya pamoja, bila kuangalia ngapi zimetolewa kwa jumuiya gani na badala yake kuacha kubaguana na kufanya kazi kwa kujituma kwa hali na mali ili kujikwamua kiuchumi," alisema.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Rosemary Sinyamule, alisema utoaji wa vyerehani kunaweza kuleta mabadiliko katika uwekezaji kwa vitendo hasa katika kuunga mkono serikali katika kuelekea uchumi wa kati.

"Huu ni uwekezaji katika wilaya yetu na hii inatutia moyo. Tayari tuna viwanda 35 vitakavyosaidia kukuza uchumi wa wananchi wa Same, hata hivyo tumetenga zaidi ya ekari 4,000 kwa ajili ya uwekezaji.

Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya hiyo, Isaya Mngulu, alisema watahakikisha matumizi bora ya mashine ili kuleta mabadiliko ya kiuchumi.

Akipokea vyerehani hivyo, Mwenyekiti wa UWT wilaya hiyo, Zaina Heshima, alisema kupitia mashine hizo wataweza kuomba zabuni mbalimbali kwenye shule na taasisi nyingine.

# 48 wapewa siku 7 kuvunja makazi yao na kuondoka

**Na Godfrey Mushi, HAI**

WAKATI wananchi wengi wakifurahia amri ya siku saba iliyotolewa na serikali ya kuwaamuru watu 48 waliojimilikisha ardhi ya Shamba la Fofo/Foo Estates, Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro kuvunja makazi yao na kuondoka kabla ya kusubiri matumizi ya nguvu, kwa wengine ni majonzi.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, ametangaza uamuzi mgumu wa kuwaondoa wananchi hao wanaodaiwa kujimilikisha shamba hilo lenye ekari 46.6 wakiwa hawana haki ya umiliki kisheria.

Alitangaza kuwaondoa baada ya kuzungumza na pande zote katika uwanja wa Shule ya Sekondari Tunoma iliyopo Kata ya Narumu, Tarafa ya Lyamungo.

Shamba hilo lilifutiwa hati na Rais, baada ya kubatilisha miliki ya shamba la Fofo, kwa lengo la kulirudisha kwa wananchi wa vijiji vya Urori, Mulama, Usari na Tella, Novemba 22 mwaka 1993.

Baada ya watu hao 48 kudaiwa kuvamia shamba hilo, mgogoro mkubwa wa umiliki wake ulizuka kati ya watu hao 48 na wananchi wa vijiji vya Urori, Mulama, Usari na Tella ambao ni wanachama wa Chama cha Ushirika cha Narumu/Manushi.

"Naelekeza kama kuna ujenzi wowote umeendelezwa pale shambani wa kudumu, nendeni kabomoeni nyumba zenu wenyewe ndani ya siku saba. Nawaapia kama Mungu aishivyo, nitakuja kusimamia ubomoaji wa nyumba hizo kwenye mashamba ya wananchi na kama mnadhani natania, nisubirini baada ya siku saba.

"Kama kuna mazao ya msimu nataka yaondoke na si vinginevyo, kwa mujibu wa sheria hayo ndio mazao tunayoyatambua. Kama kuna nyumba mkabomoe, mali ya wananchi irudi mikononi mwa wananchi na hayo yalikuwa ndio maelekezo ya Mheshimiwa Waziri (Lukuvi) aliyekuja hapa kusimamia haki hiyo kwa niaba ya Rais John Magufuli."

Kumbukumbu zilizopo kwenye majalada zinaonyesha kwamba shamba hilo lenye mgogoro kati ya watu 48 na wanakijiji wa vijiji vinne, linatambulika kama Shamba la Fofo/Foo lenye namba 240 & 242, hati namba NP 405 EP LOT 661 likiwa na ukubwa wa ekari 46.6

Kabla ya kuzuka kwa mgogoro huo, mmiliki wa awali ambaye alikuwa Dk. Athony Phones, alikopa fedha kiasi cha Sh. 120,000 katika benki iliyojulikana The Land Bank of Tanganyika au National Development Credit Agency, Oktoba 18, mwaka 1961 na kuweka rehani shamba hilo.

Lakini inaelezwa kwamba Dk. Phones aliondoka nchini, akiwa anadaiwa deni hilo na hivyo shamba hilo kuuzwa na benki kufidia mkopo huo.

Mwaka 1977, Chama cha Ushirika cha Narumu (kilichoundwa na vijiji vya Urori, Mulama, Usari na Tella) kilifanikiwa kushinda zabuni hiyo na kutakiwa kulipa deni hilo.

Wakati anatoa amri ya watu hao 48 kuvunja makazi yao, Ole Sabaya alisema shamba hilo kwa mujibu wa ofa na kwa mujibu wa hati ya msajili, ni mali ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Zaidi alieleza: "Kama mtu amekwenda kujenga shambani, amejenga jengo la kudumu maana yake huyu amejitafutia matatizo mwenyewe. Mheshimiwa Rais ameelekeza hii ni mali ya wote, kikundi cha watu wachache kisichukue na kujimilikisha mali ya watu wote. Nina taarifa humu ndani kuna wanasiasa wanawasaidia miaka yote ndio maana mnapata kiburi."

Aidha, taarifa iliyotolewa katika mkutano wa hadhara na Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Hai, Jacob Muhumba, inaeleza kuwa chanzo cha mgogoro huo ni madai ya watu 48 kutaka kukabidhiwa Shamba la Fofo na benki, jambo ambalo lilipingwa na wanachama wa Chama cha Ushirika Narumu/Manushi.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akikabidhi cheti kwa mmoja wa wanafunzi waliohitimu darasa la saba, katika Shule ya Msingi ya Waja Springs, wakati wa mahafali ya saba yaliyofanyika katika shule hiyo, mkoani Geita wikiendi. **PICHA: WMU**

# Kampuni yashangaa kulipwa zaidi ya bil. 12/-

**Na Godfrey Mushi, ROMBO**

KAMPUNI ya Mashati Oil Investment, imeeleza kushangazwa kwake na taarifa ya kulipwa zaidi ya Sh. milioni 12.2 na Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ambazo ni deni la Shule ya Sekondari Mashati.

Imesema taarifa hiyo ililenga kumdanganya kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa.

Jana, mmiliki wa kampuni hiyo, Sabasi Shirima, alidai kuwa halmashauri ya wilaya hiyo, imedanganya kwamba imelipa fedha hizo lakini ukweli ni kwamba hajalipwa chochote mpaka sasa.

"Siku Mwenge wa Uhuru ulipokuja Wilaya ya Rombo, halmashauri iliweleza kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa kwamba wangenilipa deni hilo, lakini hadi leo bora kusema ukweli kuwa sijalipwa chochote," alisema Shirima.

Zaidi alieleza, walipompelekea barua ya kumtaarifu wameshamlipa na wakapeleka nakala kwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Rombo, hakuna salio alilolipwa.

Kwa mujibu wa Shirima, katika barua ya Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo ya Juni 21, mwaka huu, yenye kumbukumbu namba HWR/34/1.12 ambayo walimwandikia (Nipashe imeona nakala yake), wameeleza kwamba amelipwa, lakini amedai hakuna ukweli wowote.

Alisema katika barua hiyo iliyosainiwa na Mkurugenzi Mtendaji, ilikuwa ikimwarifu kwamba deni alilokuwa akiidai Shule ya Sekondari Mashati, kwa ajili ya kuwauzia vifaa vya ujenzi wa maabara limelipwa Juni 21, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Shirima, barua hiyo inaonyesha kuwa fedha hizo zimelipwa katika akaunti yake iliyopo benki moja iliyopo Rombo, namba 40410002045 kwa hati ya malipo, namba 753026V1903107.

Aidha, barua hiyo inaeleza kuwa ofisi hiyo ilichukua uamuzi huo, baada ya kuona michango ya wananchi ambao ndio wenye jukumu la kulipa deni hilo ikichelewa.

Kutokana na mkanganyiko huo, mmiliki huyo amemwomba Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo, kuingilia kati sakata hilo ili aweze kulipwa haki yake.

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 17, 2019
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 15



**Maktaba ya kimataifa UDSM, kisima cha maarifa**

Ukurasa 18



## JE, WAJUA?

Mwanafunzi ajinyonga baada ya 'kunangwa' shuleni akiwa hedhi



Ukurasa 17

## JIELIMISHE

## Huduma duni za afya ni kwa nchi tajiri, maskini




# Madereva serikalini wabebeshwa 'msalaba' wa ajali za barabarani

Ukurasa 16

ELIMU KUTOKA POLISI

# Fahamu Shirikisho la Wakuu wa Polisi Ukanda wa Afrika Mashariki



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro. **PICHA: MTANDAO**

SHIRIKISHO la Wakuu wa Polisi kwa nchi za Afrika Mashariki ni umoja wa Wakuu wa Polisi kwa nchi za kanda ya Afrika Mashariki ulioanzishwa na Wakuu wa Polisi wa Nchi hizo kwa lengo la kuimarisha ushirikiano.

Lakini pia kuweka mikakati ya pamoja, kubadilishana taarifa za uhalifu na wahalifu, kubadilishana uzoefu na kuoanisha sheria ili kuongeza uwezo wa vyombo vya dola ndani ya Ukanda wa Afrika Mashariki.

Ni katika kukabiliana na uhalifu unaovuka mipaka ikiwamo usafirishwaji haramu wa binadamu, bidhaa bandia, utakatishaji wa fedha pamoja na wizi wa magari.

Shirikisho hili la Wakuu wa Majeshi ya Polisi ukanda wa Afrika Mashariki lilianzishwa mwaka 1998, linaundwa na nchi 14 ambazo ni Burundi, Comoros, Djibouti, DRC, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Seychelles, Sudan ya Kusini, Sudan, Tanzania na Uganda.

Nchi za mwisho kujiunga na umoja huo ni Burundi, Congo ambazo zilijiunga Septemba 14, 2017. Ili kuhakikisha malengo ya kuanzishwa kwa shirikisho hili yanatelekezwa, kila mwaka wakuu hawa wa Polisi toka nchi hizo 14 hufanya mkutano mkuu kwa kupokezana na nchi inayokuwa mwenyekiti wa mkutano mkuu wa mwaka, Mkuu wa Jeshi la Polisi katika nchi hiyo huwa mwenyekiti wa shirikisho hilo kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Mundo wa shirikisho hilo la wakuu wa Polisi linaundwa na Baraza la Wakuu wa Polisi.

Hili ndilo baraza la juu katika maamuzi kwenye masuala yote ya sera na huratibu masuala yote ya ushirikiano kwa kuhakikisha kamati zote zinafanya kazi kwa mujibu wa muundo wa shirikisho.

Shirikisho hilo pia lina Kamati ya kudumu na Mipango, Kamati hii inajumuisha Wakurugenzi (Wakuu) wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai kutoka katika nchi zote 14.

Hii ndiyo kamati inayoratibu ushirikiano wa kikanda, wanapanga na kuratibu Operesheni zote za pamoja na nchi wanachama na kutekeleza maazimio yanayopitishwa na shirikisho.

Vilevile, shirikisho hilo lina Kamati ndogo ya sheria. Kamati hii inajumuisha wakuu wote wa kitengo cha sheria katika nchi wanachama.

Majukumu yao ni kushughulikia mambo yote ya kisheria yanayoeleza umoja huo na kufanya ushawishi wa kuoanisha sheria za nchi wanachama.

**KAMATI NDOGO YA MAFUNZO**

Hii ni kamati inayoundwa na wakuu wa mafunzo kutoka kila nchi mwanachama ambao wanajukumu la kuangalia mahitaji ya mafunzo na kutekeleza mahitaji kwa nchi wanachama.

Sambamba na kamati hizo, pia kuna Kamati ndogo ya Kijinsia. Kamati hii hushughulikia masuala ya unyanyasaji wa kijinsia ndani ya nchi wanachama pamoja na Kamati ya Kuzuia na Kupambana na Ugaidi.

Kamati hii inaundwa na Wakuu wa Kitengo cha Kuzuia na Kupambana na Ugaidi katika nchi wanachama. Katiba ya shirikisho hilo ndiyo inayowapa mamlaka Baraza la wakuu wa Polisi na Kamati ya Kudumu na Mipango kuteua kamati kama zilivyotajwa hapo juu.

Mbali na kamati hizo kwa mujibu wa Ibara ya 8 ya Katiba ya Shirikisho la wakuu wa Polisi, ukanda wa Afrika Mashariki wameteua Ofisi ya Interpol Kanda ya Afrika Mashariki, kuwa ndiyo Sekretarieti ya kudumu ya shirikisho hilo.

Hivyo wakati wa mkutano mkuu wa mwaka, ofisi hiyo ndiyo huwa sekretarieti pamoja na kuratibu utekelezwaji wa mambo mbalimbali yanayohusu shirikisho hilo.

Baada ya kufahamu muundo wa shirikisho la wakuu wa Polisi ukanda wa Afrika mashariki, ni vizuri tukaelewa kama nilivyosema awali wakuu wa shirikisho hilo hufanya mkutano mkuu kila mwaka.

Kwa mujibu wa Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi ( SACP) David Misime, mwaka huu Mkutano huu, utafanyika nchini Tanzania katika Jiji la Arusha na utakuwa ni mkutano wa 21 tangu shirikisho hilo lianzishwe.

Mwaka 2018 mkutano kama huu ulifanyika nchini Sudan ya Kusini na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini Sudan ya Kusini alikuwa Mwenyekiti.

Mkutano ambao utafanyika nchini utaanza Septemba 15 hadi Septemba 20 mwaka huu ambapo Inspekta Jenerali wa Polisi Tanzania, IGP Simon Nyakoro Sirro, atapokea Uenyekiti wa shirikisho hilo kutoka kwa Inspekta Jenerali wa Polisi wa Sudan.

Ujio wa ugeni huo ni fursa nyingine tena kwetu sisi Watanzania baada ya mkutano wa SADC ambao ulifanyika kwa ufanisi mkubwa mwezi Septemba tunapokea tena ugeni wa nchi 14 za Afrika Mashariki ambao utajumuisha Mawaziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi hizo, Wakuu wa Polisi, Wakurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Wakuu wa kamati zote tano kama nilivyozitaja hapo juu.

Pia, katika mkutano huo, atakuwepo Rais wa Interpol Duniani, Wakuu wa Interpol Kanda ya nchi za Kusini na Magharibi mwa Afrika, Mwenyekiti wa EAPCCO na Mkurugenzi Mtendaji wa AFRIPOL. Kama ilivyo kawaida yetu Watanzania, Jeshi la Polisi linatoa wito wa kudumisha amani na utulivu, kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kuzuia uhalifu wa aina yoyote.

Aidha kuitumia fursa ya ugeni huo katika shughuli za kiuchumi.

***Imetolewa na:***
***Ofisi ya Uhusiano***
***Makao Makuu ya Polisi.***
***S.L.P. 9141,***
***DAR ES SALAAM.***



TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Anayepandisha wengine ngazini ...

"ANAYEPANDISHA wengine ngazini, hupigwa teke menoni." Maana yake mtu anayewabeba na kuwapandisha wengine ngazini huishia kupigwa teke menoni na wanaopanda kwa kuwa hawaangalii nyuma.

Methali hii huweza kutumiwa kumpigia mfano mtu aliyemtendea mwingine hisani fulani kisha asipate shukrani au fadhila.

Najifananisha na anaowapandisha wengine ngazini kwa jinsi nisivyoeleweka na waandishi wenzangu. Ingawa napata wakati mgumu kusahihisha maneno ya Kiswahili yatumiwayo na waandishi wa magazeti ya michezo wasiofuata maelekezo niwapayo kila Jumanne katika gazeti hili, sitochoka kuitetea lugha yetu ya taifa.

"Taratibu ndio mwendo" kwani mwendo ulio sawa ni wa taratibu. Methali hii hutumiwa kumkanya mtu anayefanya mambo yake kwa pupa au vishindo na kuishia kuyaharibu.

Wahenga walisema: "Asiyesikia hujionea mwenyewe." Maana yake mtu asiyesikiliza ushauri wa anayemzidi maarifa hufikwa na balaa au hupatwa na matatizo. Ni methali ya kutumiwa kutunasihi tuyathamini mashauri tupewayo na wanaotuzidi maarifa.

Sithubutu kusema nawazidi maarifa waandishi wenzangu ila waendapo arijojo (hali ya kupotea; hali ya kupoteza mwelekeo) nawajibika kuwaonesha njia sahihi. Ninachopigania ni matumizi halisi (-enye dhati ya asili; kindakindaki) ya lugha ya Kiswahili. Pia mpangilio wa maneno ya sentensi zinazoeleweka kwa watu wa rika zote mijini na vijijini.

"Kagere kaanza balaa mapemaa" ni kichwa cha habari cha gazeti maarufu la michezo nchini. Nimeeleza mara nyingi kuwa 'balaa' au 'baa' maana yake ni janga lililoenea katika jamii au kwa mtu binafsi; beluwa. Pia ni jambo, kitu au mtu anayefikiriwa kuleta maafa, mkosi au hasara; jambo lenye kuleta hali ya kutoelewana; kizaazaa, mtafaruku.

Ibara (kifungu cha maelezo kinachojitosheleza; paragrafu) ya pili chini ya kichwa cha habari hiyo iliandikwa:

"Lakini wakati nyota wakiendelea kujifua waliwaacha nyuma mastaa wanne, akiwamo Meddie Kagere ambaye ndani ya siku mbili tu za mazoezi licha ya kuchelewa kujiunga na wenzake tayari ameanza mambo ya hatari." Yafaa waandishi watambue kuwa "tamu ikizidi tamu huwa si tamu tena." Twakumbushwa kwamba jambo lolote zuri huwa na mipaka.

Sentensi haianzwi na neno 'lakini' kama ilivyotumiwa na mwandishi wa habari ninayoikosoa. 'Lakini' ni tamko la kuonesha upungufu, kasoro ya jambo au hitilafu. Mfano: 'Saa mbili kasa (kasoro) robo) n.k.

'Fua' ni kitendo cha kusafisha nguo kwa maji na sabuni ukitumia mikono au mashine. 2) Toa makumbi kutoka kwenye nazi kwa kutumia kitu chenye ncha kilichokitwa chini. 3) Tengeneza kitu kwa kutumia chuma, dhahabu, fedha au metali (madini magumu yoyote yanayoweza kupitisha joto la umeme) nyingine. 4) Kitendo cha kumfanyia mtu dawa ili kumwondolea nuhusi (nuksi); kisirani. Je, wachezaji 'hujifuaje?' Nani aliyewasababishia kisirani hicho na kwa sababu gani?

Sentensi ingeandikwa: "Wakati wachezaji wakiendelea na mazoezi, nyuma walikuwa wanne akiwamo Meddie Kagere ambaye licha ya kuchelewa kujiunga na wenzake, mazoezi aliyofanya siku mbili tu alithibitisha umuhimu wake.

" ... (jina la gazeti husika) ambalo limepiga kambi hapa Rustenburg linafahamu Kahata ambaye ni miongoni mwa usajili uliokuwa mapendekezo ya Aussems alikuwa na maelewano na washambuliaji Kagere, John Boko na Wilker Henrique ambao walikuwa wakitumia vyema krosi na pasi ambazo alizokuwa akiwapatia. (maneno 38) .

Wahenga watwambia: "Chungu kiinjike (kiweke chombo cha kupikia juu ya jiko; teleka) moto ukishawaka." Maana yake ni vizuri kuwasha moto kwanza kabla ya kuteleka chungu mekoni. Methali hii yatufunza umuhimu wa kufanya mambo hatua kwa hatua, kwa mpango. Yafaa kujua mambo ya kutangulizwa au ya kupewa kipaumbele na yapi ya baadaye.

Kwa kuwa ukurasa huo una jina la mwandishi, picha yake na maandishi: "Kutoka kambi ya Simba Afrika Kusini" hakuwa na sababu ya kuandika "... (jina la gazeti) ambalo limepiga kambi hapa Rustenburg." Kwa kuwa yajulikana timu ya Simba ipo kambini Afrika ya Kusini, hakuna sababu ya kurejelea (pitia jambo au kitu kwa mara nyingine) maelezo hayo.

Ingeandikwa: "Kahata anaelewana vizuri na washambuliaji Kagere, John Boko na Wilker Henrique wakitumia vizuri krosi (upigaji wa mpira kutoka eneo la pembeni kuelekea golini) na pasi (kumpigia mpira mwenzako wakati wa mchezo) alizowapa."

**Methali: Asiyeuliza hana ajifunzalo.**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096 0784 334 096**

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA

# Maktaba ya kimataifa UDSM, kisima cha maarifa kwa wote



Mkurugenzi Mwandamizi wa Maktaba Mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Ernest Nyari, akiwaonyesha wanafunzi (hawapo pichani) moja ya vitabu vya Sayansi vinavyopatikana katika chumba cha Maktaba mahususi kwa ajili ya masomo ya Sayansi kiitwacho 'Science Collection' wakati wa ziara fupi iliyofanywa na Shule ya Sekondari ya Mt. John Paul II katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

NOVEMBA 27, 2018, Rais John Magufuli, alizindua maktaba kubwa na ya kisasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Maktaba hiyo ina uwezo wa kuhudumia watu 2100 kwa wakati mmoja pamoja na kuhifadhi vitabu takribani 800,000.

Ndani ya maktaba, kuna ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 600.

Imegharimu kiasi cha Sh. Bilioni 93.6 hadi kukamilika kwake, fedha ambazo zimetokana na ufadhili wa serikali ya China.

Ina kompyuta 160 zilizounganishwa na mtandao kwa ajili ya kusoma vitabu kwa njia ya kieletroniki (Online books).

Ni jengo lenye ghorofa mbili na eneo lake lina ukubwa wa mita za mraba 20,000.

Ndiyo maktaba kubwa kwa nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika kwa hivi sasa.

### MANUFAA YAKE

Kupitia maktaba hii, watakaoitumia watapata ujuzi na maarifa kutoka kwenye vitabu na machapisho mbalimbali yaliyoandaliwa na waandishi na wanazuoni na kuhifadhiwa katika maktaba hiyo.

Ni heshima kubwa kwa chuo kikongwe kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupata maktaba kubwa, ya kisasa na ya kimataifa katika kuandaa rasilimali watu kwa ajili ya kutumika kwenye shughuli za kimaendeleo za ndani na hata nje nchi.

Jambo zuri kuhusu maktaba hii ya kisasa ni utajiri mkubwa wa maarifa kupitia vitabu mbalimbali vinavyopatikana humo.

Wanafunzi wa chuo hicho na wengine kutoka taasisi mbalimbali za elimu wanaruhusiwa kwenda kuvuna maarifa yaliyomo ndani ya maktaba hiyo.

Hivyo basi, uwepo wake iwe njia ya kuongeza maarifa miongoni mwa Watanzania.

Wanafunzi wanapaswa kubadilisha mitazamo yao kwa kuwa na kiu ya kuongeza maarifa kupitia usomaji wa vitabu na machapisho tofauti ndani na nje ya maktaba.

### UVIVU

Kumekuwa na tatizo kubwa kwa Waafrika na Watanzania wakiwemo la kutopenda kusoma vitabu na machapisho.

Hii imesababisha wengi kukosa uelewa wa kutosha wa masuala tofauti kutokana na ukame wa kukosa maarifa kupitia vitabu na machapisho.

Maktaba hii ndani ya UDSM ni ya Kitaifa ambapo kila mwenye kiu ya kuchota maarifa anayo nafasi ya kufanya hivyo, kwa kufuata taratibu zilizowekwa na uongozi wa chuo.

> "Njia mojawapo ya mtu kuwa mwandishi mzuri wa machapisho na vitabu ni pamoja na kusoma vitabu vilivyoandikwa na waandishi wengine.

Enzi za uhai wake, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alisisitizia Watanzania kuwa na kiu ya kujielimisha kupitia shule na vyuo pamoja na kusoma vitabu.

Na kwa kuyasimamia maneno yake, alikuwa msomaji mzuri wa vitabu na machapisho, lakini alikuwa mwandishi wa vitabu mbalimbali.

Njia mojawapo ya mtu kuwa mwandishi mzuri wa machapisho na vitabu ni pamoja na kusoma vitabu vilivyoandikwa na waandishi wengine.

Hivyo, Baba wa Taifa alituachia kielelezo kizuri cha kupenda kusoma vitabu, ili kwa kumuiga yeye wapatikane baadaye waandishi bora wa vitabu, majarida, machapisho na magazeti.

Fedha nyingi zimetumika katika ujenzi wa maktaba hii kwa kuzingatia malengo ya serikali ya kupata vijana wenye maarifa ya kutosha, kupitia usomaji wa vitabu.

Hivyo, methali isemayo "Kwenye miti hakuna wajenzi" haipaswi kufanya kazi kupitia uwepo wa maktaba hii, badala yake wananchi wakitumie kisima hiki cha maktaba kuchota maarifa.

### TANZANIA YA VIWANDA

Tanzania ya viwanda na ya uchumi wa kati inahitaji rasilimali watu wenye maarifa ya kutosha waliyoyapata shuleni na vyuoni pamoja na kusoma vitabu mbalimbali.

Kwahiyo, vijana hawana budi kuwa na utamaduni mzuri wa kusoma vitabu wakati wakiwa shuleni na vyuoni, lakini hata baada ya kuhitimu masomo yao.

Utamaduni wa kusoma unapaswa kuwa endelevu kwani elimu haina mwisho. Ni katika vitabu ndipo kunapopatikana maarifa ya ziada tofauti na yale yanayofundishwa na walimu shuleni na vyuoni.

Mwanafunzi atakayetegemea maarifa yatolewayo na walimu wake tu bila kuwa na juhudi za kusoma vitabu vya ziada katika kujielimisha zaidi, atakuwa na maarifa yasiyotosheleza.

Kutokana na umuhimu wa elimu katika maendeleo ya viwanda, sayansi na teknolojia kwa ujumla wake, usomaji wa vitabu ni nyenzo muhimu ya kufanikisha juhudi hizo.

Wanafunzi wakitumia vizuri vitabu vilivyomo ndani ya maktaba ya kisasa ya Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, watapata maarifa ya ziada tofauti na yale wayapatayo kutoka kwa Wahadhiri wao wanaowafundisha.

Nihitimishe kwa kusema; kisima cha maji kilichotengenezwa hakiwezi kuwafuata watu ili wachote maji yake, badala yake watu watakifuata kisima kuyapata maji.

Ndivyo ilivyo kwa maktaba, mwenye kiu na maarifa ataifuata ilipo na kuchota maarifa yaliyomo kwenye vitabu.

Asiyeifuata maktaba ilipo ili ajipatie maarifa, ni sawa na mtu anayekisubiri kisima kimfuate ili achote maji.

Ni lazima tuyafuate maarifa yanapopatikana ikiwemo kwenye vitabu na machapisho ili kuwa na uelewa mkubwa wa masuala mbalimbali.

Maktaba ya UDSM ni kisima kwa wote wenye kiu ya kupata maarifa. Tafakari.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali, iliyo wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Maoni: (+255) 764 666349.***

ELIMU

NA WILLIAM CHARLES

# Madereva serikalini wabebeshwa 'msalaba' wa ajali za barabarani

LICHA ya madai kwamba baadhi ya 'mabosi' serikalini ndio huamrisha au kuelekeza madereva wao kuendesha kwa mwendokasi kinyume cha sheria, ajali inapotokea lawama na mzigo wa uwajibikaji ikiwamo kufungiwa leseni na kufikishwa mahakamani hubebwa na madereva peke yao.

Kimsingi, ajali za magari ya serikali zimekuwa ni jambo lisiloshtua tena kusikika. Kwa mfano katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, zaidi ya ajali 50 zimeripotiwa.

Haipendezi, lakini kusikia watumishi wawili hadi watano wa serikali wamekufa kwa ajali za barabarani ni kama vile jambo la kawaida wakati mwingine kwa hivi sasa.

Jeshi la Polisi linasema takribani ajali zote zinazotokea zikihusisha magari ya serikali, zinatokana na mwendokasi pamoja na uchovu wa madereva.

"Hakuna sababu zingine za ajali hizi, ni kujiamini kupitiliza kwa madereva kwamba hawawezi kuchukuliwa hatua pale wanapovunja sheria ikiwemo ya kuzidisha mwendo unaokubalika kisheria," anabainisha Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP), Deus Sokoni ambaye ni Mkuu Kitengo cha Sheria cha Kikosi cha Usalama Barabarani kwa mwandishi wa makala haya.



Moja ya ajali iliyohusisha magari matatu eneo la Mkata mkoani Tanga na kusababisha vifo huku watu wengine wakibaki vilema wa maisha

### MWENDO SAHIHI

Mwendo sahihi wa gari kisheria unatajwa na Kifungu cha 51 cha Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002, kwamba ni kilometa 50 kwa saa katika maeneo ya makazi ya watu.

Hata hivyo, maeneo yenye vibao vinavyoelekeza mwendo, madereva wanalazimika kufuata maelekezo hayo.

Aidha, katika maeneo yasiyo ya makazi na yasiyo na vibao, dereva wa gari chini ya uzito wa tani 3.5 anaruhusiwa kwenda mwendo wowote autakao, lakini si kwa magari yaliyo juu ya uzito huo.

Magari ya aina hiyo yanatakiwa kutozidisha kilometa 80 kwa saa.

Baadhi ya ajali za magari ya serikali zilizotokea na kuzua mjadala mkali kutokana na mazingira ya ajali hizo, ni ile iliyomhusisha Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kingwangalla.

Ajali hii ilitokea Agosti 4, 2018 eneo la Magugu, mkoa wa Manyara na kusababisha kifo cha ofisa habari wa wizara hiyo, huku waziri akijeruhiwa vibaya.

Baada ya ajali hiyo, Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, alijitokeza kwa wanahabari akisema:

"Sheria imewekwa ili kumlinda kila raia na ndiyo maana leo hii mtu akinywa sumu akanusurika kufa anashtakiwa... hivyo kama wewe kiongozi upo na dereva wako akasababisha ajali kizembe, atachukuliwa hatua kali kama ilivyo kwa watu wengine bila kumwonea huruma."

> "…Polisi waende wakafanye utafiti tena… lawama kwa dereva wa serikali hazistahili maana taarifa zinasema dereva wa lori ndiye aliyeingia barabarani pasipo utaratibu, jambo lililosababisha ajali hiyo.



Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Fortunatus Musilimu. **PICHA: MTANDAO**

### MPIGA PICHA

Akiizungumzia ajali hiyo iliyomhusisha Waziri Kigwangalla, Mpiga picha wa wizara hiyo Michael Mlingwa ambaye alikuwa miongoni mwa watu wanne walionusurika, alibainisha kuwa ilitokea wakati wakiwa katika eneo lenye wanyama.

Anabainisha kwamba Twiga alikatiza ghafla barabarani na wakati dereva akijaribu kumkwepa ndipo magurudumu ya gari yalipasuka na gari kupinduka zaidi ya mara tatu.

Eneo la mbuga au hifadhi ya wanyamapori, ni eneo ambalo dereva anatakiwa kwenda mwendo wa wastani, huku akizingatia maelekezo ya vibao vya mwendokasi ili kuepuka madhara mbalimbali, ikiwemo ya wanyama kukatiza barabarani.

### NYINGINE

Oktoba 21, 2018 ajali ya gari la serikali Na. STK 8925 iliyogongana na lori ilisababisha vifo vya watumishi watano wa serikali, wakiwemo wataalamu wanne wa wizara ya kilimo na dereva. Hakuna aliyenusurika.

Mkuu wa Polisi Mkoa wa Singida (RPC), Sweetbert Njewike, ambako ajali hiyo ilitokea alisema chanzo cha ajali ni dereva kutokuwa makini na kuendesha gari kwa mwendo kasi.

Lakini siku mbili baadaye aliyekuwa Waziri wa Kilimo Dk. Charles Tizeba, alijitokeza na kupinga taarifa ya polisi kwamba si za kweli na kutaka uchunguzi zaidi ufanyike.

"...Polisi waende wakafanye utafiti tena...lawama kwa dereva wa serikali hazistahili maana taarifa zinasema dereva wa lori ndiye aliyeingia barabarani pasipo utaratibu, jambo lililosababisha ajali hiyo," alisema Dk. Tizeba.

Hata hivyo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, alisema polisi itaendelea kuchukua hatua za kisheria kwa wanaosababisha ajali, bila kujali vyeo vyao serikalini.

### TAKWIMU

Takwimu za polisi zinaonyesha kwamba watumishi wa serikali 34 wamefariki katika matukio mbalimbali ya ajali za magari ya serikali yaliyotokea mwaka mmoja na nusu uliopita.

Hiyo ni wastani wa watumishi wawili wa serikali wanaopoteza maisha kila mwezi kutokana na ajali za barabarani.

### ORODHA

Ipo orodha ndefu ya ajali za magari ya serikali ikiwemo ya Mei 21, 2018 Chalinze mkoani Pwani, iliyosababisha vifo vya watumishi watatu wa kituo cha uwekezaji nchini (TIC), baada ya gari Na. STK. 5923, Toyota Land Cruiser mali ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kugongana na gari aina ya Scania.

Julai 14, 2018 ilitokea ajali ya gari la Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, ambalo liliacha njia na kupinduka mkoani Singida na hivyo kusababisha vifo vya watu wawili na majeruhi watano.

Polisi walisema chanzo cha ajali kilikuwa mwendokasi uliosababisha kupasuka kwa gurudumu la mbele na gari hilo kupinduka.

Julai 30, 2018 huko Katoro mkoani Geita, gari la serikali lilipinduka likimkwepa mtembea kwa miguu, na kusababisha kifo cha ofisa habari wizara ya viwanda, huku Naibu Katibu Mkuu wa wizara na maofisa wengine watano wakijeruhiwa.

Novemba 3, 2018, ajali ya magari mawili ya serikali ilisababisha vifo vya watu saba, wakiwemo watumishi wa ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Kongwa, mkoani Dodoma.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma, Gilesi Muroto alisema chanzo cha ajali kilikuwa mwendokasi wa gari.

Februari 23, 2019 ajali ya gari la serikali iliua maofisa ardhi tisa, Ifakara mkoani Morogoro.

Jeshi la polisi lilisema gari hiyo ya serikali ilikuwa kwenye mwendo kasi kabla ya kutumbukia mtoni, baada ya kumshinda dereva.

Julai 27, 2019 gari la polisi PT 3822 lilipasuka gurudumu la nyuma na kupinduka Mkuranga, mkoani Pwani, huku askari watatu wakipoteza maisha.

Juni 25, 2019 pia gari Na. STL 3807 Toyota Hilux la Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Mkoa wa Songwe ilisababisha vifo vya watu wawili na majeruhi watatu katika kata ya Izazi Tarafa ya Isimani, Barabara Kuu ya Iringa - Dodoma mkoani Iringa.

Julai 25, mwaka huu askari watatu wa Jeshi la Polisi walifariki, huku wawili wakijeruhiwa katika ajali iliyotokea kijiji cha Kilimahewa, Mkuranga mkoani Pwani.

Ajali ilitokea baada ya gari lao Na. PT 3822 aina ya Toyota Land Cruiser kupasuka gurudumu la upande wa nyuma na kupinduka.

### UTATUZI

Katika Mkutano aliouitisha Kamanda wa Polisi mkoani Mbeya, Ulrich Matei, uliohusisha madereva wote wa serikali mkoani humo wakiwamo wakaguzi wa magari kutoka jeshi la polisi na wakufunzi kutoka chuo cha ufundi (VETA), ili kuzungumzia ajali za magari ya serikali, madereva hao walitoa malalamiko.

Walibainisha kwamba wamekuwa wakisafiri umbali mrefu bila kupumzika, kuamriwa kwenda mwendokasi, magari kutokaguliwa na kutengenezwa (service) mara kwa mara.

"Niliwaambia madereva wa magari ya serikali kwamba hawatakiwi kwenda mwendokasi kwa kisingizio cha kuamriwa...wao ndio wanaoendesha na ni wataalamu wanaotakiwa kuchukua jukumu la kuhakikisha wanafika salama pamoja na viongozi wanaowaendesha," anasema Kamanda Matei.

Anadokeza kwamba mwaka 2017, zilitokea ajali 10 za magari ya serikali na mwaka 2018 ajali 14 mkoani Mbeya.

### HATUA ZIPI ZINAWAKUMBA MADEREVA WA SERIKALI?

Nilipomuuliza ASP Sokoni kuhusu hatua zinazochukuliwa dhidi ya madereva au viongozi wanaoamrisha madereva kwenda mwendokasi na kusababisha ajali za magari ya serikali alisema:

"Tunawafungia leseni madereva wanaosababisha ajali hizo, kisha tunawafikisha mahakamani."

Aidha anabainisha kwamba, ingawa wanafahamu wapo madereva wa serikali ambao huamrishwa kuendesha gari wakiwa wamechoka ama kwenda mwendokasi, lakini kukubali kwao kufanya hivyo huku wakijua si sahihi ni uzembe na ujinga, ndiyo maana huchukuliwa hatua stahiki za kisheria.

ASP Sokoni anabainisha kuwa wakishawafungia madereva wa serikali, huandika barua kwenda kwa waajiri wao kuwajulisha kuwa dereva wao hatakiwi tena kuendesha gari kwasababu hana leseni, hivyo watafute dereva mwingine.

### MDAU

Augustus Fungo, mdau wa usalama barabarani akitoa mtazamo wake kuhusu ajali za magari ya serikali anasema:

"Ajali haijali kama upo kwenye gari la serikali wala la jeshi...ikishatokea unakufa tu...askari wanatakiwa kusimamisha na kukamata magari ya serikali kama wanavyofanya kwa raia wengine."

Fungo anasimulia kisa cha gari moja ya serikali iliyosimamishwa mara tatu na ikakataa kusimama mpaka yaliposimamishwa magari mengine njiani na yenyewe kukosa pa kupita.

"Huo ni mfano hai na halisi wa viburi vya madereva wa magari ya serikali...askari wamekuwa wakilalamika kuwa baadhi ya magari ya serikali hayakubali kusimama," anasema."

Fungo anasema, kiongozi anayeendeshwa ana wajibu wa kuhakikisha ajali haitokei kwasababu inaweza kugharimu maisha yake na wananchi kukosa huduma na utaalamu wake.

> Ajali haijali kama upo kwenye gari la serikali wala la jeshi… ikishatokea unakufa tu… askari wanatakiwa kusimamisha na kukamata magari ya serikali kama wanavyofanya kwa raia wengine.

### WAZIRI UTUMISHI NA UTAWALA BORA

George Mkuchika ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Nilipomuuliza kuhusu hatua zilizochukuliwa kwa watumishi wa ngazi za juu serikalini wanaoamrisha madereva kwenda mwendokasi au kuwafanyisha kazi bila kupumzika madereva, alisema hawezi kulizungumzia jambo hilo.

"Siwezi kulizungumzia kwa kuwa hakuna malalamiko ya aina hiyo niliyopokea, na kama yametolewa na madereva wanaokamatwa, basi wizara ya Mambo ya Ndani au Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ndizo zinazohusika," anasema.

### RIPOTI

Ripoti ya Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), ya mwaka 2018 inaitaja Tanzania kama miongoni mwa nchi zinazotumia kiasi kikubwa cha pato lake la Taifa kukabiliana na madhara yatokanayo na ajali za barabarani.

Ripoti hiyo inabainisha kwamba zaidi ya asilimia 3 ya pato la Taifa, sawa na Sh. trilioni 4 hutumika kwa mwaka kukabiliana na madhara ya janga hilo.

JIELIMISHE

## Huduma duni za afya kwa nchi tajiri, maskini



Mhudumu wa afya akimhudumia mmoja ya watoto, Kasai, DRC. **PICHA: MTANDAO**

HUDUMA duni za afya zinakwamisha maendeleo ya kuboresha afya katika nchi bila kujali vipato vyao, inasema Ripoti mpya iliyotolewa na Umoja wa Mataifa (UN) na wadau wake.

Ikiwa ni ubia wa Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo na Uchumi (OECD), Shirika la Afya Duniani (WHO) na Benki ya Dunia (WB), ripoti inasema kwa sasa, uchunguzi usio sahihi ni mambo yaliyo kwenye nchi zote maskini na tajiri.

Lakini pia kupatiwa dawa zisizo sahihi, matibabu yasiyofaa au yasiyohitajika, vifaa duni vya kliniki au watoa huduma wasio na mafunzo na stadi za kutosha. Hali ni mbaya zaidi katika nchi maskini na za kipato cha kati, ambapo asilimia 10 ya wagonjwa wakiwa hospitalini wanaweza kuambukizwa magonjwa, ikilinganishwa na asilimia saba katika nchi za kipato cha juu.

Hii ni pamoja na maambukizi ya hospitali yanayoweza kuepukwa kwa usafi bora na kubadili mazoea ya kudhibiti maambukizi na matumizi sahihi ya viuavijidudu.

Ripoti hiyo yenye jina 'Kutoa Huduma bora za Afya, suala la lazima katika utoaji huduma kote ulimwenguni' pia inasisitiza kuwa ugonjwa unaohusishwa na huduma duni za afya, hugharimu zaidi familia na mifumo ya afya.

Aidha, huduma ya afya ya uzazi katika nchi nane zenye kiwango cha juu cha vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano ni duni, huku asilimia 28 ya wanawake ndio wanapata huduma wakati wa ujauzito.

Katika mataifa ya kipato cha juu ripoti imesema, asilimia 15 ya matumizi ya hospitali ni katika kushughulikia maambukizi yatokanayo na makosa ya utunzaji mgonjwa akiwa hospitalini.

Hata hivyo, ripoti inataja maendeleo fulani katika kuboresha ubora ikiwemo ongezeko la muda wa kuishi kwa wagonjwa wa saratani na moyo.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus, amesema shirika lake linajitolea kuhakikisha kuwa watu wote kila mahali wanaweza kupata huduma bora za afya kwa wakati na mahali wanapohitaji, kwa kuwa bila huduma bora hakuna upatikanaji wa huduma za afya kwa wote.

**HABARI UN**

UTAFITI

# WHO yahimiza hatua kuzuia vifo vya kujiua



Inashauriwa kuwasikiliza watu walio katika msongo wa mawazo na kuwasaidia mapema, kwani jambo hili lisipofanyika mapema husababisha wachukue hata maamuzi ya kujiua. **PICHA: MTANDAO.**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limesema karibu watu 800,000 hujiua kila mwaka, ikiwa ni zaidi ya idadi ya watu wanaouawa katika vita na mauaji yanayofanywa na mtu dhidi ya mwingine au saratani ya matiti.

Katika ripoti yake mpya, shirika hilo la afya duniani limesema viwango vya kujiua duniani vimepungua kwa kiasi fulani kati ya mwaka 2010 na 2016, lakini idadi ya vifo imeendelea kuwa pale pale kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu duniani.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Tedros Adhanom Ghebreyesus, alisema katika taarifa kuwa licha ya hatua zilizopigwa, kuna mtu anafariki kila sekunde 40 kutokana na kujiua.

Data za mwaka 2016, ambazo ndizo za mwisho kutolewa kwa takwimu za vifo vinavyotokana na kujiua, zilionyesha kuwa kwa kila watu 100,000, kulikuwa na vifo 10.5 vinavyotokana na kujiua.

Kwa ujumla viwango vya kujiua duniani vilipungua kwa karibu asilimia 10 kuanzia 2010 hadi 2016, lakini kanda ya Amerika ilionyesha kuongezeka kwa viwango hivyo kwa asilimia 6 katika kipindi cha miaka sita.

Mtaalamu kutoka kitengo cha afya ya akili cha WHO, Alexander Fleischmann, anasema mauaji ya kijiua ni tatizo kubwa la afya ya jamii, na kutoa wito wa hatua kuchukuliwa kushughulikia tatizo hilo.

"Ni muhimu wakati wote kuzuia vifo vya kujiua, kwamba tuwasikilize watu wanaotuzunguka. Tunapaswa kuchukulia kwa uzito mtu anaposema hataki tena kuishi au hata wanaposema kwa uthabiti kwamba wanata kujitoa uhai wao," anasema na kuongeza:

"Kila mmoja wetu ana jukumu katika kuzuia mauaji ya kujiua, hivyo sote tunaweza kujitolea kuwasikiliza watu wanaotuzunguka wanapokuwa kwenye huzuni au wanataka msaada wetu."

**WITO KWA SERIKALI**

Ripoti hiyo ya WHO inasema idadi ya mataifa yaliyo na mikakati ya kuzuia watu kujiua imeongezeka katika kipindi cha miaka mitano tangu kuchapishwa kwa ripoti yake ya kwanza ya dunia.

Lakini idadi jumla ya mataifa yaliyo na mikakati hiyo, ambayo ni 38, bado ni ndogo sana na kuongeza kuwa serikali zinahitaji kujifunga na kuanzisha mikakati hiyo.

Kujiua kulishika nafasi ya pili kwa kusababisha vifo vingi miongoni mwa vijana wenye umri kati ya miaka 15-29, baada ya majeraha yanayotokana na ajali za barabarani. Mbinu zinazotumiwa zaidi katika kujiua ni pamoja na kujinyonga, kujipiga risasi na hususani katika maeneo ya vijijini, kunywa dawa za sumu za kuulia wadudu.

Ripoti hiyo imebainisha kuwa mauaji zaidi yanatokea katika mataifa maskini na yale yenye maendeleo ya kati, ambako idadi kubwa ya wakazi wa dunia wanaishi, lakini viwango ni vikubwa zaidi katika mataifa tajiri.

Baada ya Guyana, Urusi ilikuwa ya pili kwa idadi kubwa ya watu wanaojiua. Mataifa mengine yaliyo kwenye orodha hiyo ni pamoja na Lithuania, Lesotho, Uganda, Sri Lanka, Korea Kusini, India na Japan pamoja na Marekani.

Na karibu katika kila taifa, wanaume wana uwezekano mkubwa zaidi wa kujiua kuliko wanawake.

Ni katika mataifa matano tu ya Bangladesh, China, Lesotho, Morocco na Myanmar ambako wanawake zaidi wanajiua kuliko wanaume. **DW**

JE, WAJUA?

# Mwanafunzi ajinyonga baada ya 'kunangwa' shuleni akiwa hedhi

MWANAFUNZI mmoja nchini Kenya, amejiua baada ya kudaiwa kuzomewa darasani kwa kuwa sare yake ya shule ilichafuka na madoa ya damu, alipokuwa kwenye hedhi.

Mama wa Mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka 14, alisema binti yake alijinyonga baada ya kudhalilishwa na mwalimu wake, vyombo vya habari vya Kenya vimeripoti.

Polisi walitumia gesi ya kutoa machozi kutawanya kundi la wazazi takribani 200, waliokuwa wamepiga kambi nje ya shule, taarifa zinasema.

Kenya ilipitisha sheria mwaka 2017, kugawa taulo za kike bure kwa wanafunzi wa kike shuleni.

Mama wa binti huyo alisema mwalimu alimuita mwanafunzi huyo "mchafu" na kumtaka atoke nje shuleni Kabiangek, Magharibi mwa mji mkuu Nairobi, wiki iliyopita.

"Hakuwa na pedi na damu ilipochafua nguo zake, aliambiwa atoke darasani na asimame nje," mama yake alinukuliwa akiongea kwenye vyombo vya habari.

Alisema binti yake alirejea nyumbani na kumwambia mama yake kilichotokea shuleni, lakini alipokwenda kuchota maji alijinyonga.

Wazazi wake waliripoti tukio hilo polisi lakini inadaiwa hakukuwa na hatua zozote zilizochukuliwa, Gazeti la Daily Nation limeripoti.

Wasichana wanatumia vikopo vya hedhi kujisitiri.

Pamoja na wazazi wengine, walikusanyika nje ya shule Jumanne iliyopita. Polisi walifika na kuwakamata watu watano wakati waandamanaji walipofunga barabara na kuvunja geti la shule, ripoti zinasema.

Polisi wa mkoa, Alex Shikond, amesema mazingira ya kifo cha binti huyo yanachunguzwa.

Mkuu wa shule hiyo alikataa kuzungumza kuhusu tukio hilo.

Nchini Kenya na kwingineko, wasichana wengi hawawezi kumudu gharama za pedi.

Ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN) ya mwaka 2014, inasema kati ya wasichana 10 waishio Kusini mwa Jangwa la Sahara, mmoja hukosa masomo wakati wa hedhi.

Baadhi ya wasichana hupoteza asilimia 20 ya masomo yao kwa sababu ya hedhi. **BBC**



Wanafunzi wa kike wakiwa shuleni, ambapo wanahitaji kusaidiwa ili waweze kuendelea vyema na masomo yao hata wakiwa katika siku zao za hedhi
**PICHA: MTANDAO**

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Mashambulizi dhidi ya wageni yapunguza raha ya Kiswahili

WAKATI 'wino haujakauka' tangu kutiwa saini makubaliano kati ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na ziara ya siku mbili ya Rais Cyril Ramaphosa zilizotangulia mkutano wa wakuu wa nchi na serikali wa SADC, mkasa umetokea nchini Afrika Kusini.

Ni mashambulizi ya nguvu, kupora na kusomba bidhaa katika maduka na kuwapiga raia wa nchi za Afrika walio na biashara nchini humo, na hasa katika jiji la Durban, na kwingineko ambako makundi ya vijana wa Kizulu ni wengi.

Ni wazi kuwa wageni hawahitajiwi nchini humo, au tuseme kabila kubwa zaidi nchini humo limeamua kuwa wageni wafungashe waondoke; sasa watazungumza lugha ya wageni?

Mashambulizi hayo yamethibitisha sura ya jamii ya Afrika Kusini ambayo si ngeni, lakini itikadi ya mshikamano kati ya nchi za Afrika ilihakikisha kuwa wanalaumiwa tu vijana wanaojitokeza na magongo na mitarimbo kuwapiga na kuwapora wageni.



Washiriki wa Kongamano la Kwanza la Kiswahili la Kimataifa Zanzibar, lililoandaliwa na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. **PICHA: MTANDAO**

Ila kutokana na kuboreshwa zaidi kwa teknohama, kila mwenye 'simu janja' ameweza kuangalia kwa karibu nini kilikuwa kinatokea, watawala huko (kuanzia polisi hadi serikali) wanasema nini, na Waafrika wanaolengwa na vurugu wamesikia nini na wameona nini.

'Kudanganywa' kupitia misimamo ya kisiasa inayojitahidi kuwalinda viongozi wa ANC ikakwama.

Eneo linaloendana na huko kulindana na hisia kuwa kwa sababu sisi sote ni Waafrika, tungependa kuwa na lugha moja ya kutuunganisha kama Waafrika, na wapo wengi hapa nchini wanaoapa kuwa lugha hiyo ni Kiswahili.

Inatajwa kuwa lugha ya nne inayotambuliwa kutumiwa katika kuendesha shughuli za Umoja wa Afrika, iwe ni katika ngazi ya Tume ya AU, Baraza la Mawaziri au mkutano wa wakuu wa nchi.

Sasa kuenea kwa Kiswahili kunahitaji dhana halisi na sahihi kuwa Afrika inajipenda vya kutosha na watu wake wako tayari kutumia lugha za jadi kwa masuala ya nchi, hata lugha za jadi za kimataifa kama Kiswahili.

Unaweza kusema kuwa mkasa wa Afrika Kusini umeingiza changamoto ya wazi katika dhana hiyo, kwani huwezi kutenga matumizi ya Kiswahili na kuwakubali Waafrika wengine kwa mfano nchini Afrika Kusini.

Ukigusa suala hilo unakuta linavuta mlolongo wa masuala mengine yanayofanana na hilo, kuwa licha ya kuwa katika nchi zilizoendelea Kiswahili kinathaminiwa, barani Afrika labda kutafuta katika taasisi zenye uhusiano wa jadi na mapambano ya ukombozi Kusini mwa Afrika.

Kiswahili kina thamani katika nyanda au anga hizo kwa sababu za kiitikadi, ni lugha ya wenyeji wao wakati wa harakati.

Isitoshe, kuna tahadhari kadhaa nyingine ambazo zingetumika ipasavyo zingepunguza hamasa ya kuomba matumizi ya Kiswahili barani Afrika, iwe ni SADC au AU.

Moja ni ile ya 'ukoloni mamboleo'amb ayo inatoa mwanga wa kuelewa kuwa nchi za Afrika kwa jumla hazina lugha za kitaifa, ila lugha kadhaa za kitaifa na lugha ya kigeni ambayo ndiyo muhimu zaidi.

Hata hapa nchini ambako juhudi za kukiweka Kiswahili kuchukua maeneo ya ziada ya mawasiliano hata kitaaluma ni kubwa kuliko kwingineko Afrika, bado mfumo wa elimu umebaki kujikita katika Kiingereza.

Tunajua hasara ya kupoteza uelewa fasihi wa lugha hiyo, kwani wachache watakaojielimisha lugha hiyo kwa njia zao wenyewe ndio 'watairithi nchi.'

Dhana nyingine ni ile ya utegemezi, kuwa Mwafrika anaona aibu kukosolewa katika lugha ya kigeni na siyo katika lugha ya ndani ya nchi, hivyo tunaona aibu 'kuvunja' lugha ya Malkia na hakuna aibu yoyote mtu akiongea atakavyo katika Kiswahili.

Kwa maana hiyo, itakuwaje ambaye hajali anaongea vipi lugha mojawapo kati ya zile za Afrika Kusini, ahangaike kuongea Kiswahili vizuri?

Ni wazi kuwa hakuna msukumo wa kitamaduni katika mfumo tegemezi kuwa mtu anaongea lugha hiyo ya Kiafrika au hapana, hata kama inatumiwa katika ukanda wa nchi tano au zaidi.

Ni suala tu la kuelewa kuwa wakati Kiswahili hapa nchini kinapewa hadhi kuliko lugha za kikabila, katika upana wa bara hili Kiswahili kinakuwa kama lugha mojawapo ya kikabila yenye wazungumzaji katika nchi kadhaa wa kadha.

Zipo nyingine kama Kisomali (Somalia, Kenya, Tanzania, Ethiopia, Eritrea, Djibouti), na hata Marekani kwani mamia ya maelfu ya Wasomali wamehamia huko miaka mingi.

Sasa wanaye mbunge (katika Baraza la Wawakilishi) mwanamke, Ilhan Omar aliyezaliwa Somalia na kukulia Marekani; anaicharanga Israel.

Katika mfumo tegemezi kila mtu anazungumza lugha yake mwenyewe na ile ya 'bwana mkubwa,' hivyo hapa tutazungumza Kiswahili na Kiingereza licha ya kuwa na lugha zetu za makabila ambazo tangu uhuru zimekandamizwa na Kiswahili, wakati wenzetu nchi za jirani wana lugha za kikabila na Kiingereza.

Kujaribu kueneza matumizi ya Kiswahili ni kama kugeuza kibao katika utegemezi, kana kwamba sasa kuna taifa kubwa linalofanya maamuzi kuhusu maisha ya watu wa bara au ukanda huu, na kwa vile taifa hilo linazungumza lugha ya Kiswahili, kila mmoja inabidi atii.

> “Kwa maana hiyo, itakuwaje ambaye hajali anaongea vipi lugha mojawapo kati ya zile za Afrika Kusini, ahangaike kuongea Kiswahili vizuri?

Hakuna nchi kama hiyo, kwani hata China ambayo imejiinua kwa utamaduni wake na kupata tu mitaji kutoka nje, inaeneza lugha yake kwa mahitaji ya utalii wa kibiashara, kwenda kununua bidhaa nchini humo na kuweza kusalimia wenyeji. Siyo zaidi.

Ndiyo maana inabidi wapanga sera watambue kuwa lugha ni utambulisho wa kuzaliwa kama ambayo binadamu anakuwa, na taifa vivyo hivyo, na kwa maana hiyo kila nchi na kila mtu anazaliwa katika mandhari ya lugha fulani iliyo kuu na labda nyingine kwa mahitaji tofauti.

Kuongeza lugha nyingine ni suala la utashi binafsi kama kujifunza chombo cha muziki au kucheza sinema, riadha, n.k.

Huwezi kuwa na sera ya kufanya lugha iwe utambulisho wa nchi endapo watu wake hawakuzaliwa katika lugha hiyo, na masuala kama ukombozi au mshikamano hayabadili chochote hapo. Hivyo Afrika haitajifunza Kiswahili.

Pia kuna dhana ya utandawazi, ambayo hasa ni kupanuka kwa mawasiliano kwa upana wa dunia na siyo kuwasiliana na nchi za jirani kama ilivyokuwa zamani.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

UTEKELEZAJI wa miradi mbalimbali ya maendeleo bila kutumia mkandarasi maarufu kama 'Force Account' umeonyesha mafanikio makubwa. Wadau wanasemaje?



### DISMAS LYASA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

KIMSINGI unapokuwa kiongozi wa nchi au wa sehemu yoyote, ambacho unatakiwa kuwa nacho ni ubunifu, na ajenda kubwa ambayo viongozi wanatakiwa kuwa nayo ni kuzingatia yale ambayo wametoa ahadi kwa wananchi.

Kwamba watakapokuwa madarakani, watafanya moja, mbili, tatu...kwa hiyo kama katika kufanya kazi ikaonekana kuna mfumo fulani, ambao unaleta tija zaidi kwa maendeleo ya taifa, kwa ustawi wa taifa kwa ujumla wake, unatakiwa utumike.

Unajua katika mambo ya uongozi ni kwamba unaweza kuwa na mtu anayetumia njia tofauti, labda za kiuongozi, na wengine wakawa wanafuata zile taratibu za kwenye vitabu. Kuna uongozi wa aina nyingi, uongozi wa kufuata msingi ya demokrasia, yaani kwa kila kitu unachokifanya ni lazima ushirikishe watu ili waseme ndiyo.

Sasa kuna tatizo pia wakati mwingine kufuata aina hii mfumo wa kusikiliza maoni ya kila mtu. Kwa sababu inatakiwa ufahamu pia uelewa wa wale watu, ambao unawashirikisha, kwani wakati mwingine wanaweza wakaona jambo fulani kuwa si zuri wakati ni zuri.

Ninachotaka kusema ni kwamba ni vizuri viongozi wakaangalia tu wenyewe yale, ambayo wanaona yanaweza kuleta mabadiliko kwa nchi.

Mtindo ambao unaonekana unafaa, basi ni vizuri ukaendelezwa au ukatumika, kwani wanachohitaji Watanzania kushuhudia ni maendeleo yakionekana. Kwa sababu hicho ndicho wananchi wanataka kukiona na siyo kuangalia mfumo.

Kwa hiyo niwapongeze hao wanaotumia mfumo huo, ambao unaonekana kuwa na tija kwa taifa, kwa kuzingatia lengo kuu ni maendeleo, hivyo sioni tatizo kama mfumo umeleta tija kwa umma.



### THOMAS NGAWAIYA (MKURUGENZI WA TAASISI YA UTAWALA BORA NA MAENDELEO)

MAENDELEO tunayoyaona sasa yanatokana na mfumo huo, hivyo Watanzania hatuna budi kujivunia hatua iliyochukuliwa na rais wetu, kwani wajanja wachache walikuwa wakinufaika sana kwa kuongeza cha juu, ambacho sasa hakipo tena.

Fedha zinazotumika ni zile zilizokusudiwa kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. Mimi ninaamini kwamba miradi mikubwa inayotekelezwa sasa inatokana na utaratibu huo wa kutumia force account, ambayo imewanyima mwanya walaji.

Mimi kama mtu ninayeshughulika na suala la utawala bora nikiwa na taasisi yetu ambayo kifupi chake ni CEGODETA, ninajua kile ambacho rais ameamua kukifanya. Ninamuunga mkono kwa hilo, kwani bila kuchukua hatua kama hizo tungeendelea kurudi nyuma, lakini sasa tunasonga mbele.

Barabara zinajengwa, ndege zinanunuliwa na pia kuna mradi mkubwa wa umeme wa mto Rufiji.

Watanzania hatuna budi kujivunia hatua hiyo, ambayo imekuja kusaidia vitu kufanywa kwa viwango na kwa gharama halali, tofauti na miaka ya nyuma ambako fedha za umma ziliiwa sana.

Unaweza kukuta hata jengo la darasa ambalo labda gharama yake ingekuwa Sh. milioni 20, lakini linajengwa kwa Sh. milioni 40 hadi 50. Maana yake ni kwamba fedha nyingine zinaingia katika mifuko ya wajanja wachache, hali ambayo kwa kweli ilichangia kukwamisha maendeleo ya nchi yetu.



### ISSA NJINJO (MKAZI WA RUANGWA MKOANI LINDI)

MIRADI ya maendeleo bila kutumia mkandarasi, ambayo ni maarufu kwa jina la 'Force Account ', lengo lake ni kuhakikisha kwamba wananchi wa eneo la mradi wanapata manufaa ya ujenzi ule na kufanya ujenzi huo kuwa ni wa kwao na kujivunia.

Kama ujenzi wa majengo, basi wajivunie kwamba wameshiriki tangu mwanzo wa ujenzi huo kuanzia ngazi ya kuchimba msingi hadi kumalizika kwa jengo au majengo.

Binafsi ninaona mfumo huo una manufaa sehemu mbili, kwa serikali na kwa umma pia, kwani serikali inatumia kiasi cha fedha kilichokusudiwa na pia wananchi wa maeneo ya mradi nao wananufaika kwa kushiriki kama vibarua na kujipatia chochote.

Lakini kikubwa zaidi ni kwamba hata kile kinachojengwa kinakuwa imara siyo kuchakachuliwa kama ambavyo miaka ya nyuma kulikuwa na usanii mwingi. Unaweza kukuta jengo limetumia gharama kubwa hadi kukamilika, lakini likawa chini ya kiwango.

Kimsingi ni kwamba sioni tatizo kwa uamuzi wa serikali wa kufanya mambo yake kwa kutumia hiyo akaunti, kwani imeonyesha mafanikio makubwa.

Ninaweza kusema kuwa kwa njia hiyo, miradi mingi imekuwa na tija kwa jamii, kwa kutengeneza ajira kwa vijana, kutokana na ukweli kwamba wamekuwa ni nguvukazi, katika kufanya shughuli zote za ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa na serikali.



### ARAFA TUMBO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

KILICHOFANYWA na Rais John Magufuli ni maamuzi magumu ambayo kwa kweli yanataka roho ngumu, hasa mtu anapoamua kusimamia maendeleo ya nchi.

Ninaamini kwamba kuna changamoto zake ikiwamo ukosoaji kutoka kwa watu mbalimbali wanaoamini kwamba amekosea, lakini pia ni vyema jamii ikatambua kuwa lengo lake siyo baya.

Anachofanya ni kuokoa fedha za walipa kodi ambazo zilikuwa zikiingia katika mifuko ya wasanii wachache wanaopenda kujinufaisha kwa vitu ambavyo si jasho lao.

Hebu fikiria mifano ambayo rais amekuwa akiitoa mara kwa mara kuhusu upigaji wa fedha za Watanzania, kwamba unaweza kukuta kazi fulani inatakiwa kufanyika labda kwa gharama ya Sh.milioni 10, lakini watu wanaongeza hadi kufikia milioni 20 au na zaidi.

Lakini sasa mianya hiyo imezimwa kupitia Force Account ili kuokoa fedha na kuzipeleka kwenye shughuli nyingine za maendeleo. Sasa kama kuna watu wanalalamikia hatua hiyo inayolenga kuleta maendeleo, basi watakuwa na lao jambo na inawezekana ndio waliokuwa wakinufaika kwa jasho lisilo lao.

Serikali imeamua kutekeleza miradi ya maendeleo kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kuwabana waliokuwa wakinufaika kwa kuongeza cha juu.

Binafsi kama Mtanzania nisiye mwanachama wa chama cha siasa, ninasema bila kificho kwamba hatua alizochukua kiongozi wa nchi ni za kutupeleka pazuri na kila mtu anakula kwa urefu wa kamba yake.



### WINIFRIDA ELIAS MKAZI WA DAR ES SALAAM

HATUA hii ya serikali ya awamu ya tano kutumia utaratibu huu wa kutekeleza miradi mbalimbali ya serikali bila ya kutumia mkandarasi katika ujenzi wa majengo ya shule, zahanati, mabweni na mingineyo (force account ) ni ya kupongeza kwa sababu inaokoa fedha nyingi ambazo hatimaye huelekezwa katika utekelezaji wa miradi mingine yenye tija kwa wananchi.

Binafsi ninaunga mkono kwa sababu unakuta darasa ambalo lilikuwa linatumia Sh. milioni 50 kwa kumtumia mkandarasi, sasa linatumia Sh. milioni 20 kupitia mfumo huu wa force account.

Unakuta bweni la kulala na vitanda vyake lililokuwa linagharimu Sh. milioni 150 hadi 170 kupitia kwa mkandarasi sasa linajengwa kwa viwango vinavyotakiwa kwa gharama ya Sh. milioni 70.

Maana yake ni kwamba tofauti hii kubwa ya gharama ilikuwa inatokana kimsingi na mambo ya rushwa, ubadhilifu ama kuweka cha juu kwa kuongeza gharama za manunuzi kwa mfano ya vifaa vya ujenzi. Kwamba unakuta pengine nondo milimita 18 inayouzwa kwa Sh.18,000 imewekewa gharama ya Sh. 30,000.

Ndiyo maana ninasema iwapo wakandarasi hawatabadilika na kuweka gharama halisi, basi ni bora serikali hii ikaendelea kutekeleza miradi yake kwa kutumia mfumo huu kwani unahusisha gharama ndogo kwa kazi ya viwango vinavyotakiwa na hivyo kuokoa fedha ambazo zinaelekezwa kwenye miradi mingine yenye ustawi kwa wananchi.





# Vifaa vya kupimia saratani kupelekwa Mbeya

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WANANCHI wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wanatarajia kuondokana na adha ya kusafiri kwenda kupata vipimo vya ugonjwa wa saratani katika Hospitali ya Ocean Road jijini Dar es Salaam, kufuatia serikali kuahidi kupeleka vifaa vya kupimia ugonjwa huo katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila kwa nyakati tofauti alipokuwa akizungumza na wananchi kwenye mikutano ya hadhara katika Kata za Forest na Maendeleo jijini Mbeya uboreshaji wa sekta ya afya unavyofanywa na serikali mkoani humo.

Alisema serikali ilitoa zaidi ya Sh. bilioni saba kwa ajili ya ujenzi wa vituo 14 vya afya pamoja na upanuzi wa baadhi ya vituo mkoani humo kwa ajili ya kusogeza huduma kwa wananchi.

Alisema vilevile serikali imetoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya upanuzi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya Kitengo cha Wazazi (Meta) ili kuondoa msongamano wa wagonjwa katika hospitali hiyo inayohudumia mikoa saba.

Chalamila alisema katika hospitali hiyo pia serikali imenunua vifaa mbalimbali vya kisasa kwa ajili ya vipimo vikubwa ikiwamo CT- Scan pamoja na vipimo vingine vya mionzi ambavyo vilikuwa havijawahi kuwapo.

"Pia tumeahidiwa mwakani kuletewa vifaa vya kupimia saratani ili wananchi waachane na kusafiri mpaka Hospitali Ocean Road jijini Dar es Salaam, vipimo hivyo vitapatikana katika hospitali yetu ya kanda ambayo kwa sasa ni muhimu na inaangaliwa kwa jicho la pekee," alisema Chalamila.

Alisisitiza kuwa kutokana na maendeleo hayo yanayoletwa na serikali ya awamu ya tano mkoani hapa, ndio maana aliwahi kusema baadhi ya watu wanaodai kuwa hawaoni maendeleo wanatakiwa kuchapwa viboko ili wayaone.

Alisema kuna baadhi ya watu ambao wao wanapinga kila kitu na kuikosoa serikali wakati hata wao hakuna wanachochangia kwenye maendeleo ya taifa kitu ambacho alidai kuwa ni upuuzi na hauwezi kuvumilika.

# Kuvunjika daraja kwakosesha mawasiliano

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAKAZI wa vijiji vya Idugumbi, Iwala na Iwanga vilivyopo Kata ya Utengule Usongwe, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamekosa mawasiliano ya barabara baada ya daraja la Mto Nzovwe linalounganisha vijiji hivyo na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kuvunjika.

Kufuatia hali hiyo wameiomba serikali kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), kuwajengea daraja la kudumu kutokana na kila mwaka kuharibika na kukwamisha shughuli zao za maendeleo ikiwamo biashara.

Walidai kuwa huduma nyingi za kijamii wanategemea katika Mji Mdogo wa Mbalizi ikiwamo za afya ambazo zinapatikana katika Hospitali Teule ya Ifisi hali inayowafanya kuhofia maisha yao kufuatia mawasiliano kukatika.

Mmoja wa wananchi hao, Kinanda Sanga, alisema baada ya daraja hilo kuvunjika, maofisa wa Tarura walipewa taarifa na wakaifunga barabara hiyo na sasa hawana njia mbadala.

"Sisi mazao tunayozalisha huku tunayauza Mbalizi, tukitaka kwenda halmashauri kupata huduma za serikali lazima tupite hapa na hata huduma za afya tunazipata Ifisi, hospitali ya mkoa au hospitali ya kanda ambazo ili kufika lazima tupite hapa, lakini kwa sasa tunahofu akitokea mgonjwa wa dharura hatuwezi kumkimbiza," alisema Sanga.

Mfanyabiashara wa Mbalizi, Elia Nyika, alisema pamoja na barabara hiyo kufungwa, wanalazimika kupita kwa madai kuwa barabara mbadala ni hatari zaidi kutokana na kutofanyiwa matengenezo.

Aliiomba serikali kuharakisha matengenezo ili kuokoa mitaji ya wakulima wa eneo hilo ambao wanazalisha mazao yanayoharibika haraka zikiwamo mbogamboga, nyanya na ndizi.

Diwani wa Kata ya Utengule Usongwe, Elia Mkono, alisema daraja hilo limekuwa likiwatesa wananchi kila mwaka na kwamba bahati nzuri kwa sasa limeharibika kiangazi wakati mto huo hauna maji mengi tofauti na miaka mingine.

Alisema akiwa Diwani wa Kata hiyo, aliwahi kuwasilisha ombi maalumu kwenye Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kuomba daraja hilo lijengwe, lakini akaambiwa kuwa serikali haina fedha.

"Kutokana na hali ilivyo sasa, naiomba serikali ilijenge daraja hilo kwa kutumia fedha za vyanzo vingine ili kuwaokoa wananchi hawa ambao kwa sasa wamekuwa kama wapo kisiwani," alisema Mkoano.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Mbeya Vijijini, Akimu Mwalupindi, alipotembelea daraja hilo alisema kwa sasa ni hatari kwa wananchi na hivyo serikali inatakiwa ichukue hatua za haraka kuwanusuru wananchi.

Alisema vijiji vinavyotegemea kulitumia daraja hilo ndivyo vinavyoongoza kwa uzalishaji wa chakula katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, alisema serikali imeshaahidi kuanza kuchukua hatua za haraka kukarabati daraja hilo mara moja pamoja na kuikarabati barabara mbadala wakati likitafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

Alisema mbali na daraja hilo pia anaendelea kufuatilia fedha zilizoahidiwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi mingine ya barabara ikiwamo ya Shigamba – Isongole yenye urefu wa kilomita 50.



Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Jerome Ngowi (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini humo jana, kuhusu kukamatwa kwa watu wanaotuhumiwa kwa wizi wa bajaji (pichani kutoka kushoto), baada ya kuwanasa katika msako unaoendelea. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watano wanaswa tuhuma wizi wa Bajaj, bodaboda

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

JUHUDI za Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, kukomesha wizi wa vyombo vya usafiri hasa Bajaj na pikipiki, zimeanza kuzaa matunda baada ya kuwanasa vijana watano wanaodaiwa kuhusika kwenye matukio hayo huku likiendelea kuwasaka wengine.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juzi, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Jerome Ngowi, aliwataja vijana waliokamatwa kuwa ni dereva wa bajaji Yusuph Husein (20), fundi bajaji Francis Simon (31), Anold Valelian (24), Denis Ade (28) na Khalfan Said (19), wote wakazi wa Mbeya.

Alisema awali jeshi hilo lilimnasa Yusuph akiwa na bajaji moja ya wizi aina ya Tvs King yenye namba za usajili MC. 341 BZT na namba ya Sumatra 2597, akiwa ameitoa magurudumu yote, kioo cha mbele na vifaa vingine.

Kamanda Ngowi alisema baada ya kumkamata na kumbana, alikiri kuiba bajaji hiyo katika eneo la Kabwe akiwa na wenzake ambao aliwataja na kusaidia kunaswa kwa wenzake wanne. Alisema walimkamata Francis ambaye ni fundi bajaji katika eneo la Uyole akiwa na vifaa vyote vilivyokuwa vimetolewa kwenye bajaji hiyo.

Alisema waliendelea na msako na kufanikiwa kuwanasa wengine watatu ambao wanadaiwa kushirikiana na Yusuph kuiba bajaji hiyo na kwamba wanaendelea na msako.

"Tunaendelea na juhudi za kuwasaka wengine waliohusika kwenye wizi huu pamoja na mtandao wote unaojihusisha na wizi wa vyombo vya moto hapa Mbeya na mikoa jirani, lakini pia tunaendelea kumtafuta mmiliki wa bajaji hii," alisema Kamanda Ngowi.

Aliwatahadharisha vijana wote wanaojihusisha na matukio ya wizi na uhalifu wa aina nyingine kuacha tabia hiyo kwa kuwa watashughulikiwa.

Vilevile aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kwa kusaidia kuvibaini vikundi mbalimbali vya uhalifu na kutoa taarifa ili vishughulikiwe kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Kama wewe ni mhalifu uliyejipenyeza na kuingia katika Mkoa wa Mbeya kibahati bahati, subiri 'mtiti' wake uko kisogoni mwako, tunaendelea na operesheni nyingine za kupambana na uhalifu na wahalifu, lazima tutokomeze vitendo hivyo," alisema Kamanda Ngowi.





# Sababu 7 zinazochangia vifo vya kinamama

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imeeleza sababu saba zinazochangia vifo vitokanavyo na uzazi kwa kinamama Mkoa wa Dodoma ikiwamo uzazi pingamizi na matumizi ya dawa za miti shamba.

Kufuatia hali hiyo, mkoa huo umezindua Mpango Mkakati wa miaka mitano wa kuboresha huduma ya mama na mtoto ambao unalenga kuondokana na vifo hivyo utakaogharimu Sh. bilioni 43.

Akitoa taarifa ya hali ya afya ya mama na mtoto mkoani humo, Mratibu wa Huduma ya Afya ya uzazi, vijana, mama na mtoto, Mary Shedrack, alisema kwa mwaka 2018 kulikuwa na wanawake 74,579 waliojifungua na waliojifungua kwa njia ya kawaida ni 63,943 huku kwa njia ya upasuaji 7,405.

Pia waliojifungulia njiani, majumbani na kwa wakunga wa jadi ni 5,396.

Licha ya vifo vitokanavyo na uzazi kwa kinamama kupungua kutoka 85 kwa mwaka 2010 hadi 67 kwa mwaka 2018, bado kuna sababu saba zinazochangia.

Alitaja sababu hizo kuwa ni kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua, kifafa cha mimba, upungufu wa damu, kuchanika kwa mfuko wa uzazi, uambukizo, matatizo ya dawa ya usingizi na uzazi pingamizi.

"Licha ya mwelekeo kuonyesha kuwa kuna kushuka kwa vifo, lakini zipo sababu mbalimbali zinazochangia hali hiyo," alisema.

Alisema kuna changamoto ya umbali wa kufika kwenye vituo vya kutolea huduma na ukosefu wa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya uzazi.

Naye Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Options ambaye ni kiongozi wa timu ya mradi wa WISH, Dk. Moke Magoma, alisema wamejipanga kuhakikisha mpango huo unatekelezeka na wapo tayari kutoa ushirikiano.

"Kwa mfano nimeangalia kwa vifo vya kinamama mwaka 2018 ambavyo vilikuwa 67 ni sawa na kinamama wawili wanafariki kila wiki, ni sawa na abiria 67 wote wa ndege yetu (ATCL) pendwa, watu wengi wanaangamia na kusababisha simanzi," alisema.

Akitoa maelezo kuhusu mpango huo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Best Magoma, alisema mkakati huo wa miaka mitano kuanzia 2019 hadi 2024, unakwenda kujibu matatizo yatokanayo na uzazi na maeneo 14 yamepewa kipaumbele.

Alisema mpango huo utagharimu Sh. bilioni 43 na miongoni mwa mambo yaliyopewa kipaumbele ni huduma za uzazi wa mpango, mimba, rufani, kujifungua, huduma za dharura kwa kinamama na watoto wachanga na ushiriki wa wanaume kwenye huduma za uzazi.

Akizindua mkakati huo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema vifo vitokanavyo na uzazi ni janga kubwa na kutokana na hali hiyo mkoa kwa kushirikiana na wadau wa afya wameandaa mkakati huo ili kuhakikisha hakuna kifo kitokanacho na uzazi.

Alisema fedha nyingi zinatumika kwenye eneo hilo, lakini bado kuna tatizo kubwa na kwamba kama mkakati huo ukisimamiwa vyema hakuna sababu ya kuwa na vifo.

"Haiwezekani mahala pengine mama ameenda hospitali amewahi kabisa amepokelewa, kila kitu kipo, lakini mtu anapoteza maisha, menejimenti tusimamie uwajibikaji kila mtu akitimiza wajibu wake na inawezekana," alisema.

Alisema kuna sababu zinazochangia vifo hivyo na matumizi na dawa za miti shamba.

"Kinamama 556 kati ya 100,000 wanafariki kila mwaka kutokana na uzazi na vinatakiwa kushuka kufikia 292 ifikapo mwaka 2024," alisema.



Kaimu Mkurugenzi Idara ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Kemilembe Mutasa, akizungumza na wakazi wa Wilaya ya Mpwapwa jana, kwenye tamasha la ufunguzi wa mradi wa shirika lisilo la kiserikali la Kisiki Hai. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Taasisi zaelekezwa elimu vijijini ukatili kijinsia

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

NAIBU Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago, amezitaka taasisi zinazojihusisha na kupinga ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na ndoa za utotoni kutoa elimu vijijini ili wazazi na walezi waweze kukabiliana na hali hiyo.

Chibago aliyasema hayo katika ufunguzi wa mdahalo wa kuchangia mimba za utotoni uliofanyika jijini hapa ambao ulihusisha jamii mbalimbali wakiwamo wanafunzi.

Chibago alisema elimu vijijini dhidi ya kupiga vita ukatili kwa watoto ikiwamo ndoa za utotoni inahitajika kwa kiasi kikubwa, kwa sababu wengi wa wazazi walioko maeneo hayo hawana uelewa.

"Naomba mpanue wigo wa utoaji elimu kwa wazazi dhidi ya uzuiaji wa ndoa za utotoni msipofanya hivyo tutazidi kupoteza taifa la kesho ambao ni vijana," alisema Chibago.

Alisema ni vema taasisi hizo zikaweka mikakati ya kutembelea vijiji mbalimbali ili kusaidia kutoa elimu hiyo kwa wazazi na walezi ambao wengi wamekuwa wakimaliza kesi za mimba kienyeji badala ya mtuhumiwa kuchukuliwa hatua stahiki za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine.

Alisema anaamini elimu hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa jamii ya maeneo hayo kupata uelewa wa jambo hilo ikiwamo kulikemea.

"Naomba wekeni mikakati ya kuzunguka vijiji mbalimbali mkifanya hivyo mtakuwa mmewasaidia watoto kutimiza malengo yao na taifa kwa ujumla," alisema Chicago.

Alisema ni vyema kuanza kujikita vijijini kutoa elimu hiyo ambayo itatoa manufaa makubwa kwa jamii. Amina Mzee kutoka Dawati la Jinsia la Kituo cha Polisi Kati jijini Dodoma, alisema wazazi wanapaswa kutoa ushirikiano pale wanayopewa elimu dhidi ya kupinga ukatili na ndoa za utotoni ili kuwarahisishia taasisi husika kupambana nalo.

# Watakiwa kukabiliana na lishe duni

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

MAOFISA watendaji wa kata katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma wametakiwa kusimamia utekelezaji wa afua za lishe katika kata zao ili kukabiliana na hali duni ya lishe.

Kauli hiyo ilitolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Balthazar Ngowi, alipokuwa akifungua mafunzo maalum ya kuwajengea uwezo maofisa watendaji wa kata ili waweze kusimamia afua za lishe katika kata zao leo jijini Dodoma.

Alisema suala la lishe ni ajenda ya kitaifa na kwamba halmashauri ya jiji inalipa suala ya lishe umuhimu mkubwa ili kuondokana na tatizo la udumavu na mwelekeo wa taifa wa kufikia uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Haliwezi kuendelea iwapo watu wake wanakabiliwa na tatizo la udumavu, kwa maana hiyo maofisa watendaji mna wajibu wa kuhakikisha tatizo la lishe linapatiwa ufumbuzi katika kata zenu kwa kushirikiana na maofisa watendaji wa mitaa na vijiji," alisema Ngowi.

Akiongelea zoezi la kusaini mikataba baina ya maofisa watendaji wa kata na watendaji wa mitaa na vijiji, Ngowi alilitaja zoezi hilo kuwa linalenga kufikia dhamira moja ya kukabiliana na tatizo la lishe katika halmashauri hiyo.

"Katibu Tawala mkoa amesaini mkataba na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji kuhusu utekelezaji wa masuala ya lishe. Pia amesaini mkataba na maofisa watendaji wa kata, ambao nanyi mtasaini mkataba na maofisa watendaji wa mitaa na vijiji," alisema.

Alisema serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais Dk. John Magufuli, inataka matokeo ya kazi, hivyo kila mtumishi anatakiwa apime utendaji wake kulingana na matokeo ya kazi," alisisitiza.

Aliwataka pia kutekeleza matakwa ya mkataba wa lishe vizuri na kuwataka kutoa taarifa mapema watakapokutana na changamoto wakati wa utekelezaji wake za kuwakwamisha kufikia malengo.

Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Semeni Juma, alisema hali mbaya ya utapiamlo inasababishwa na ulishaji duni, maradhi ya mara kwa mara na huduma hafifu za malezi na makuzi ya awali ya watoto wadogo.

"Utapiamlo unachangia maradhi, vifo na uchelewaji wa ukuaji wa mwili na maendeleo ya akili kwa watoto," alisema.

Kuhusu malengo ya mkataba baina ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji na watendaji wa kata, alisema lengo kubwa ni kufanikisha suala la kuboresha hali ya lishe na kupunguza athari za utapiamlo katika jamii.

Pia malengo mengine ni kuhakikisha jamii kupitia uongozi wa kata inashiriki ipasavyo katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mpango wa halmashauri na afua za lishe.

Alisema maofisa watendaji hao wa kata watawajibika kuwasilisha taarifa za utendaji kazi kuhusiana na mkataba huo kwa robo mwaka, nusu mwaka na mwaka katika ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji.

"Tunaomba wakati mwingine wa mafunzo kama haya yaratibiwe kwa wigo mpana ili tuwe na siku mbili au tatu. siku hizo zitatupa urahisi wa kwenda kutekeleza changamoto kwenye kata zetu ni kubwa mno usipoiva vizuri ni shida, hatimaye tunajiamini tutayafanyia kazi yote tuliyofundishwa," alisema Mongo.

Mkataba baina ya mkurugenzi na watendaji wa kata utakuwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai mosi, 2019 hadi Juni 30, 2021 na utakuwa ukipimwa kila baada ya miezi sita ya utekelezaji.



# 500 wachunguzwa, kutibiwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAGONJWA 562 kutoka maeneo mbalimbali ya Zanzibar wamepima afya na wengine kupatiwa tiba ya maradhi yanayowasumbua.

Magonjwa hayo ni pamoja na kisukari, shinikizo la damu na ngozi katika tiba iliyotolewa kwenye kambi maalumu ya uchunguzi.

Kambi hiyo ilifanyika katika Shule ya Sekondari Kijini mkoa wa Kaskazini Unguja.

Akizungumza na wanahabari kuhusu yaliyojiri kwenye kuchunguza afya na kutoa tiba, msimamizi wa kambi hiyo, Kassim Faki Khalid, alisema iliratibiwa na Taasisi ya Zanzibar Outreach Programme kwa kushirikiana na mradi wa Best of Zanzibar.

Alisema wagonjwa waliojitokeza wapo wa maradhi ya kisukari, shinikizo la damu, macho, masikio, pua, koo, vidonda vya mdomoni pamoja na vya ngozi.

"Wagonjwa 42 waling'olewa meno na wagonjwa saba wenye matatizo ya kinamama wametakiwa kwenda Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja kwa uchunguzi zaidi," alisema Khalid.

Wagonjwa takribani 369 waliojitokeza walikuwa wakisumbuliwa na matatizo ya ngozi pamoja na vidonda vya pembezoni mwa mdomo wakiwamo watoto.

Kwa upande wake Sheha wa Shehia ya Mbuyutende, Khamis Simai Khamis, aliwaomba waratibu wa mradi huo kufanya kambi za kuchunguza afya wananchi kila baada ya miezi sita badala ya mwaka mara moja.

Alisema wananchi katika vijiji vya shehia hiyo wanakabiliwa na maradhi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo lishe duni, kutumia maji machafu na salama pamoja na vumbi inayotokana na uchakavu wa barabara kuu na kusababisha kuongezeka kwa matatizo ya maradhi ya macho na ngozi.

"Tatizo la majisafi ni changamoto kubwa pamoja na mavumbi yanayotokana na uchakavu wa barabara kuu ya Kijini mpaka Matemwe Mbuyutende," alisema Sheha Khamis.

Ofisa Afya na Mazingira wa Mradi wa Huduma za Jamii Best of Zanzibar, Nahya Khamis Nassor, alisema mwamko wa usafi wa afya na mazingira umeanza kuongezeka kwa wanafunzi na wananchi tangu kuanza kupatiwa mafunzo ya afya na mazingira.

Hata hivyo, alisema kutokana na ardhi katika vijiji hivyo kuwa ya mawe pamoja na kukosekana kwa huduma ya maji ya uhakika familia nyingi zinakabiliwa na tatizo la lishe bora.

Alisema kuwa wakati umefika kwa wadau wa maendeleo kusaidia kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii ikiwamo kusaidia kambi za wananchi za kupima afya na tiba pamoja na kutoa mafunzo juu ya umuhimu



Ofisa Afya wa mradi wa huduma za jamii wa Best of Zanzibar, Nahya Khamis Nasoor, akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu umuhimu wa wananchi kupima afya katika kambi ya uchunguzi wa afya na tiba iliofanyika katika Kijiji cha Kijini na kuratibiwa na Zanzibar Outreach Programe (ZOP) jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Aagiza polisi kukamata wasanii wa Bongo Fleva

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Ayoub Mahamed Mahmoud, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kuwakamata wasanii wa Bongo Fleva kwa madai ya kukiuka maadili.

Watuhumiwa hao ni Jamillah Abdallah (Baby) na Maulid Husein Abdallah (Mauzinde).

Mahmoud aliagiza jeshi hilo kuwakamata wahusika hao ndani ya siku tatu kwa ajili ya kuhojiwa zaidi na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Agizo hilo la Mkuu wa Mkoa limekuja kufuatia video zinazosambaa katika mitandao ya kijamii zikionyesha vitendo vya mmomong'onyoko wa maadili na aibu.

Vitendo hivyo vilifanywa Septemba 8, huko Kiembe Samaki katika sherehe iliyoandaliwa na msanii mmojawapo.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Vuga, Mkuu wa Mkoa, alisema kuwa vitendo hivyo vilivyofanyika katika sherehe hiyo ni uvunjifu wa sheria na utaratibu wa nchi na kwenda kinyume na mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari.

Aidha, alisema serikali Mkoa wa Mjini Magharibi itaendelea na kusimamia utamaduni, maadili na nidhamu za wananchi wa mkoa huo kwa nguvu zote ili kuimarisha ustawi wa jamii na kwamba vitendo vya mmomonyoko wa maadili haviwezi kuvumiliwa.

"Naendelea kuwakumbusha wenzetu wa Jeshi la Polisi kupitia taarifa hii na kuwaomba wananchi kutusaidia taarifa za watu hawa ili wakamatwe na kuwaweka ndani kwani walisababisha kutokea kwa vitendo hivi vya uvunjifu wa maadili vinavyopelekea kutia dosari mkoa wetu na Zanzibar," alisema.

Aliongeza kuwa ni mlezi wa vijana na yupo karibu na vijana wengi, lakini kwa kitendo kilichofanywa na msanii huyo na wenzake katika sherehe aliyoiandaa hakivumiliki na wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Alieleza kuwa kuna taarifa ambazo amezipokea kuwa mmoja kati ya watuhumiwa ameonekana usiku bandarini akiwa anaondoka Zanzibar.

Katika hatua nyingine mkuu huyo wa mkoa aliwaomba wananchi kushirikiana na serikali kutoa taarifa panapotokea uvunjifu wa maadili na amani.

## Wasaidizi wa kisheria waonywa wasibague

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKURUGENZI wa Idara ya Msaada wa Kisheria, katika Wizara ya Sheria na Katiba, Hanifa Ramadhan Said, amesema kuwa kila mwananchi anayo haki ya kupata msaada wa kisheria bila ya ubaguzi kwa mujibu wa sheria na katiba ya Zanzibar.

Aliongeza kuwa katiba ya mwaka 1984 inasisitiza kulindwa kwa haki za binadamu na kwamba kila mmoja anastahili, haki na kulindwa utu wake.

Alisema kuwa azma ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma stahiki za msaada wa sheria kutoka kwa wanasheria ambao wana sifa zinazohitajika kwa mujibu wa sheria.

Aliyasema hayo wakati alipokuwa akifungua mafunzo ya kujenga uelewa kwa wasaidizi watoaji huduma za msaada wa kisheria kutoka taasisi mbali mbali.

"Uwepo wa Idara ya Msaada wa Kisheria Zanzibar, unafungua ukurasa mpya katika kuwahakikishia wananchi haki pamoja na usimamizi mzima wa huduma za msaada wa kisheria," alisema. Mkurugenzi Hanifa aliiomba jamii kuwa tayari kuitumia Idara ya Msaada wa Kisheria pamoja na wasaidizi wake kwa utaratibu maalum uliowekwa kwani si watu wote watapewa huduma hiyo isipokuwa kwa yule asiye na uwezo kama sheria na kanuni zinavyoelekezwa.

Aidha, alisisitiza kuwa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 inatambua na inahakikisha haki na inajumuisha suala la msaada wa kisheria kama msingi wa haki za binadamu kwa watu wote hivyo ni wajibu wa watoaji wa msaada wa kisheria kuifuata miongozo iliyowekwa ili kuweza kuisaidia jamii kupata msaada wa kisheria kwa ufanisi na kwa wakati.

Kwa upande wao wawezeshaji wa mafunzo hayo na maofisa sheria kutoka Idara ya Msaada ya Kisheria, Ali Haji Hassan na Hajar Idrisa Haji waliwataka washiriki hao kufanya tathmini na kuwa waangalifu pale mdai anapopeleka maombi yake ikiwamo kutoa vipaumbele kwenye maeneo muhimu.

Alitaja kuwa ni pamoja na masuala ya watoto, wazee, wenye ulemavu, unyanyasaji wa kijinsia udhalilishaji, migogoro ya ardhi, urithi, huduma za mtoto na masuala ya uvunjifu wa haki za binadamu.

# Waziri Mkuu achukizwa mgongano wa DC, DED

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amechukizwa na mgongano uliopo kati ya Mkuu wa Wilaya ya Malinyi, Majura Kasika na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Mussa Mnyeti, hivyo kumwelekeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora kwenda kuchunguza weledi wa utendaji kazi wao.

"Ni aibu Mheshimiwa Rais amewateua vijana wawe viongozi, lakini leo hadi wananchi wa kawaida wanajua mgongano wenu maofisini. Ni aibu Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi mnagombana tena wakati mwingine mnagombania miradi, mmesahau kutekeleza majukumu yenu."

Waziri Mkuu ametoa maelekezo hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa Wilaya ya Malinyi pamoja na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye uwanja wa Toboa, akiwa katika siku ya tatu ya ziara yake ya kikazi mkoani Morogoro. Alisema serikali imewapa nafasi hiyo ili wakasimamie maendeleo ya wananchi na inapeleka fedha kwa ajili ya kuboresha maendeleo ya jamii kama kuimarisha huduma za afya, elimu, maji na miundombinu ya barabara lakini wao wanagombania miradi na mingine wanaichakachua.

Waziri Mkuu alisema mbali na CAG na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora kwenda kuchunguza utendaji wa viongozi hao, pia ameuelekeza uongozi wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) wakakague miradi ya ujenzi inayotekelezwa kwenye wilaya hiyo kama ubora wake unalingana na thamani halisi.

"Baada ya kupata majibu ya uchunguzi na kubaini kiini cha tatizo ndani ya wilaya hii hatua zitachukuliwa."

Awali, Mbunge wa Jimbo la Malinyi, Dk. Haji Mponda, alimweleza Waziri Mkuu kwamba kwenye wilaya hiyo kuna matatizo ya mahusiano kati ya serikali na halmashauri jambo linalosababisha kukwama kwa shughuli za maendeleo.

Alisema kutoelewana kwa viongozi wa wilaya hiyo, Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi kumesababisha mgawanyo mkubwa kuanzia katika Baraza la Madiwani hadi kwa wananchi mitaani, hivyo alimwomba Waziri Mkuu awasaidie kulipatia ufumbuzi suala hilo.



Mkufunzi kutoka Bunge la Zimbabwe, Dk. Isaiah Munyoro, akitoa mada mbele ya watumishi wa Ofisi ya Bunge kutoka Idara ya Maktaba na Utafiti, kuhusu masuala mbalimbali yakiwamo ya jinsia, katika mradi wa awamu ya pili ya kuwajengea uwezo wabunge na watumishi wa Bunge, unaodhaminiwa na UNDP, jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Wadau bima waisubiri Sept. 26 kwa hamu

**Na Beatrice Moses**

SEPTEMBA 26 mwaka huu inasubiriwa kwa hamu na wadau wa sekta ya bima nchini, kwa kuwa itahusisha kutangazwa kwa kampuni zinazotoa huduma hizo kwa umahiri na zitazawadiwa tuzo maalum.

Hatua hiyo inafanywa kwa mara ya kwanza kwenye sekta ya bima Tanzania, ikilenga kuleta ushindani kwenye sekta ya bima nchini.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kuhusu hatua hiyo Katibu wa Taasisi ya Bima Tanzania (IIT), Ernest Kilumbi, alisema wanaandaa tuzo hizo wakishirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA), zitatolewa Septemba 26 mwaka huu mkoani Mwanza.

Alisema wanaamini hatua hiyo ya kuambua na kuzawadia watendaji wenye ufanisi katika uendeshaji, uongozi na utawala wa wadau katika sekta ya bima nchini itasaidia kuboresha huduma hiyo muhimu.

"Dhumuni kuu la tuzo hizi ni pamoja na mambo mengine ni kutambua na kuhamasisha uvumbuzi kwenye sekta ya bima, kuhamasisha ukuaji endelevu wa michango ya bima na kuleta ushindani katika sekta ya bima," alisema Kilumbi.

Alisema Julai mwaka huu, walifanya kampeni ya kuhamasisha umma na wadau mbalimbali wa sekta ya bima ili waweze kushiriki kwenye mchakato wa uwasilishaji wa maombi.

Kilumbi alisema matokeo ya mchakato huo yaliwazawadia kupata ushiriki mzuri, kwa kuwa kulikuwa na mchujo awamu ya kwanza kila kipengele cha tunzo hizi kilipitia hatua tatu.

"Tulipokea maombi sabini na mbili, kati ya hayo maombi 32 yalipitishwa wakati maombi arobaini yalikataliwa kwa sababu mbalimbali," alisema.

Alisema vigezo vya utoaji wa alama zilitegemea hati zilizo wasilishwa na waliotuma maombi kuhusiana na mambo yaliyofanywa na mwombaji, mafanikio aliyopata pamoja na kuonyesha ushahidi wa vitu hivyo.

Akizungumza kwa niaba ya jopo la majaji Frank Kitende alisema kuwa wote walifanya kazi kwa umakini kupitia maombi ya washiriki wote na kuhakiki taarifa zilizowasilishwa.

Alibainisha kuwa alama za ufaulu zitawekwa kwenye mtandao baada ya sherehe ya utoaji wa tunzo hizo ambazo zitahusika kampuni bora ya bima.

Kamishna wa Bima Tanzania na mlezi wa Taasisi ya Bima Tanzania, Dk. Musa Juma, alisema Wiki ya Bima au hufanyika kila Septemba na ni jukwaa sahihi Kwa ajili ya kuhamasisha na kuratibu shughuli mbalimbali za bima.

Dk. Juma alitaja baadhi ya shughuli hizo kuwa ni pamoja na kutoa elimu ya ufahamu wa bima na afya, kushirikiana na jamii kwa niaba ya wadau wa sekta ya bima ikiwamo kutembelea kituo cha wazee wasiojiweza, na watoto yatima na kushiriki kwenye uchangiaji wa damu na michezo kwa ujumla.

"Pia imekuwa ikitumika katika kubadilishana maarifa na utaalamu wa bima, kutoka kwa wataalamu wa ndani na nje ya nchi, taasisi ya bima hutoa vifaa muhimu kwa maendeleo, uboreshaji wa maarifa ya bima na mazoezi na kuongeza mtandao wa kibiashara," alisema.

# Wapigwa 'stop' kuajiri wasio na mafunzo kijeshi

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amepiga marufuku kampuni za ulinzi kuajiri walinzi ambao hawajapitia mafunzo ya kijeshi, pamoja na kuwakabidhi silaha za moto kuzitumia, kwa kuwa ni kuhatari usalama.

Alisema mlinzi ambaye hajapitia mafunzo yoyote ya kijeshi kupewa silaha ya moto kuitumia kwenye rindo lake ni hatari, lakini kampuni hizo za ulinzi zimekuwa zikiajiri walinzi wasiyo na sifa na kuwapatia silaha hizo kinyume cha taratibu.

Mboneko alibainisha hayo juzi kwenye kikao kazi na wamiliki wa kampuni ya ulinzi wilayani humo, kilichokuwa na lengo la kutoa maelekezo kwao juu ya kuajiri walinzi ambao walishapitia mafunzo ya kijeshi.

Alisema kwenye Wilaya ya Shinyanga kuna jumla ya kampuni za ulinzi 34, lakini kampuni ambayo inaajiri walinzi wenye sifa ambao walishapitia mafunzo ya kijeshi ni moja tu, na kuyataka ambayo hayajafanya hivyo yatekeleze maagizo ya serikali, tofauti na hapo wahame kufanya kazi wilayani humo.

"Kwenye wilaya yangu nilishapiga marufuku kampuni za ulinzi kuajiri walinzi ambao hawajapitia mafunzo ya kijeshi, tuna vijana wengi tu wa Jeshi la Akiba hawana ajira na wamekuwa wakirandaranda mitaani, watumieni hao ikiwa wana uwezo wa kutumia pia silaha za moto," alisema Mboneko.

Naye Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga Richard Abwao, alisema kampuni hizo za ulinzi zina mchango mkubwa sana kwenye suala la ulinzi na usalama, lakini walinzi ambao wamekuwa wana waajiri hawana sifa kabisa na kushindwa kumudu kutumia silaha za moto, na hata ubebaji wa silaha hizo ni hatari.

## HABARI KIMATAIFA

# Mafuta yapanda bei Saudia ikishambuliwa

**RIYADH,** Saud Arabia

GHARAMA ya mafuta imepanda kwa kiwango cha juu kuwahi kushuhudiwa katika miezi minne baada ya mashambulio mawili dhidi ya vituo vya mafuta Saudi Arabia yaliosababisha kumwagika kwa asilimia tano ya mafuta duniani.

Kiwango cha mafuta ghafi kilipanda kwa asilimia 19 kwa thamani ya Dola za Marekani 71.95 kila mtungi, huku viwango vingine, West Texas Intermediate, vikipanda asilimia 15 kwa thamani ya Dola za Marekani 63.34.

Bei zilishuka kidogo baada ya Rais wa Marekani, Donald Trump kuagiza kufunguliwa kwa akiba nchini Marekani.

Huenda ikachukua wiki kadhaa kabla ya vituo hivyo Saudia kurudi katika hali ya kawaida.

Mashambulio hayo dhidi ya vinu katika shina la viwanda vya mafuta Saudia vinajumuisha kituo kikubwa duniani cha usafirishaji mafuta.

**Saudi Arabia inatarajiwa kutumia akiba ili usafirishaji mafuta uendelee kama kawaida wiki hii.**

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, alisema, Tehran imehusika na mashambulio hayo.

Rais Trump kwenye akaunti yake ya mtandao wa Twitter alisema kuwa Marekani inafahamu mhusika wa uhalifu huo ni nani na ipo tayari ila inasubiri kusikia kauli ya serikali ya Saud Arabia kuhusu namna ambavyo inataka kulifuatilia hilo.

Katika ujumbe mwingine kwenye twitter, Rais Trump alisema kuna mafuta mengi! Wasaudi hawajaeleza kwa kina kuhusu mashambulio hayo, kando na kusema kwamba hakuna aliyeathirika, lakini imetoa ishara kidogo kuhusu utengenezaji mafuta.

Waziri wa Nishati, Mwanamfalme Abdulaziz bin Salman alisema kupungua kwa utengenezaji mafuta kutafidiwa kwa kutumia akiba kubwa iliyopo.

Saud Arabia ndio wauzaji wakuu wa mafuta duniani, ambapo wanasafirisha zaidi ya mitungo milioni saba ya mafuta kwa siku.

Mkuu wa Takwimu katika Shirika la Interfax Energy mjini London, Abhishek Kumar, alisema: "Maofisa wa Saudia wamedai kudhibiti moto huo, lakini sio kuwa umezimwa kikamilifu, na huenda ikachukua wiki kadhaa kabla ya usambazaji mafuta ukarudi katika hali ya kawaida."

Saudi Arabia inatarajiwa kutumia akiba ili usafirishaji mafuta uendelee kama kawaida wiki hii.

Hata hivyo, Mkurugenzi Msimamizi wa Mipango ya Nishati katika soko la RBC Capital Markets mjini New York, Michael Tran, alisema: "Hata iwapo tatizo hilo litatatuliwa kwa haraka, tishio la kutenga asilimia sita ya mafuta yanayotengenezwa duniani sio fikra tu. Kutahitajika faida ya ziada inayohitajika kwa mwekezaji kujilipa."

Waziri Mkuu wa Mambo ya Nje ya Marekani, Mike Pompeo, alisema Tehran imehusika na mashambulio hayo ya uharibifu lakini hakutoa ushahidi maalum kuunga mkono tuhuma zake.

Alipinga tuhuma za waasi wa Houthi nchini Yemen wanaoungwa mkono na Iran kwamba wao ndio waliotekeleza mashambulio hayo.

Iran imeishutumu Marekani kwa uongo na waziri wake wa Mambo ya Nje, Javad Zarif alisema kuwa kuituhumu Iran hakutomaliza janga nchini Yemen.

Yemen imekumbwa na vita tangu 2015 wakati Rais Abdrabbuh Mansour Hadi alipolazimishwa na waasi hao wa Houthi kutoroka Mji Mkuu Sanaa.

Saudi Arabia inamuunga mkono Rais Hadi, na anaongoza muungano wa mataifa ya kieneo dhidi ya waasi hao.

Wakati huo huo, Marekani imeituhumu Iran kwa mashambulio mengine katika vituo vya mafuta katika eneo hilo mwaka huu. **BBC**

## Ameza pete ya harusi usingizini

**WASHINGTON,** Marekani

MWANAMKE mmoja nchini Marekani, Jenna Evans, amefanyiwa upasuaji baada ya kuivua pete yake ya ndoa kutoka kwenye kidole chake na kuimeza wakati alipokuwa amelala fofofo.

Jenna, mwenye umri wa miaka 29, alisema kuwa mchumba wake Bobby alikuwa katika treni ya mwendokasi na akalazimika kumeza pete ili kuilinda dhidi ya watu wabaya.

Alipoamka katika nyumba yake mjini California aligundua kuwa alichofikiria kilikuwa ni ndoto tu, lakini akagundua kuwa pete yake haipo kidoleni.

Alisema kuwa alipogundua hilo alimwamsha mpenzi wake na kumweleza ndipo wapenzi hao wakaenda hospitalini.

Jenna alisema alihangaika kukumbuka kisa hicho ili kuwaeleza madaktari kwa sababu alikuwa anacheka na kulia sana.

Picha za X-ray zilibaini kuwa pete hiyo ilikuwa ndani ya tumbo lake, na madaktari wakakubaliana kuwa lingekuwa si jambo la busara kuiacha ijiondoe tumboni yenyewe kwa njia ya choo.

Jenna ambaye ni mkazi wa San Diego, Marekani baadaye alifanyiwa upasuaji wa kuiondoa pete hiyo, lakini alitakiwa kusaini fomu za kukubali kufanyiwa upasuaji huo, ikiwa kifo kingetokea.

"Halafu nikalia sana kwa sababu ningekuwa mjinga sana kama ningekufa, niliisubiri sana pete hii ya uchumba na nitaolewa na Bobby Howell," alisema Jenna.

Taarifa zinaeleza kuwa upasuaji ulikuwa wa mafanikio na Jenna alivyozinduka baada ya upasuaji alianza kulia.

"Nilifurahi sana kwa sababu siwezi tena kuiangalia na kuithamini kama ilivyokuwa awali," alisema Jenne. **BBC**



Wananchi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo wakiwa wamedandia treni katika Mji Mkuu wa Kinshasa. **PICHA: REUTERS**

# Askari wa AU wauawa Somalia

**MOGADISHU,** Somalia

ASKARI zaidi 12 wa Kikosi cha Kulinda Amani cha Umoja wa Afrika (AMISOM) kutoka Burundi wameuawa na wengine kadhaa kujeruhiwa katika shambulio la kuvizia nchini Somalia.

Shumbulio hilo lilitokea juzi na liliendeshwa na wanamgambo wa Kiislamu wa kundi la Al Shabab lenye mafungamano na al-Qaeda nchini Somalia.

Msafara wao ulishambuliwa wakati ulipokuwa ukirudi kwenye kambi yao kwenye barabara muhimu inayounganisha Mji Mkuu Mogadishu na Jimbo la Shabelle. Kikosi hicho cha Jeshi la Amisom kilikuwa kinarudi kutoka Mogadishu.

Kikosi hicho kilikuwa kinasindikiza malori yaliyokuwa yanasafirisha chakula kutoka Jowhar, mji mkubwa, unaopatikana kilomita 90 Kaskazini Magharibi mwa Somalia kwenda kwenye masoko ya Mji Mkuu Mogadishu.

Karibu na kijiji cha Balcad, katikati ya miji hiyo miwili, msafara huo wa kikosi cha AMISOM ulishambuliwa na wanamgambo wa Al Shabab. Kwa mujibu wa mashahidi, mapigano hayo mabaya yalidumu kwa muda wa dakika 20. Barabara hiyo, na kijiji hicho cha Balcad, vinajulikana kuwa hatari.

Juzi asubuhi, maofisa wawili wa serikali za mitaa na dereva wao waliuawa baada ya gari lao kukanyaga kifaa cha kulipuka karibu na eneo la shambulio lililotokea Jumamosi.

Machi 2018, wanajeshi watano wa Burundi waliuawa sehemu hiyo katika shambulio kama hilo lililotekelezwa na kundi la wanamgambo wa Al Shabab.

Licha ya juhudi za AMISOM, vita kwa ajili ya kulinda barabara hiyo haijazaa matunda.

Barabara hiyo ni muhimu kwa mamlaka ya Somalia kwani inaunganisha mkoa wa kilimo wa mji mkubwa wa Jowhar na Mogadishu. **RFI**

# Wizara yaandaa sera mpya ya kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Japheti Hasunga, amekutana na menejimenti ya wizara, wakuu wa taasisi na wenyeviti wa Bodi za Mazao zilizopo chini ya wizara.

Lengo la mkutano huu wa siku mbili kuanzia jana jijini Dodoma ni kujadili maandalizi ya sera mpya ya kilimo ya mwaka 2019 na kuondoa mapungufu yaliopo katika sera ya mwaka 2013.

Waziri Hasunga alisema umuhimu wa kuwa na sera mpya ya kilimo ni kufanya kilimo kuwa na tija na cha kibiashara, hivyo kuleta maendeleo makubwa katika sekta ya kilimo.

"Tunataka sera mpya ya kilimo ilenge kukifanya kilimo kuwa shughuli kuu ya kiuchumi itakayochangia kukuza uchumi wa nchi na kuongeza ajira," alisisitiza Waziri Hasunga.

Waziri Hasunga alibainisha kwamba sera mpya inatakiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu ili kutoa fursa kwa Bunge kutunga sheria na kanuni za kilimo.

Pia katika mkutano huu Wizara ya Kilimo itajadili na kupitia taarifa ya utekelezaji wa shughuli kwa mwaka 2018/2019 na kuweka mkakati madhubuti wa utekelezaji mipango utendaji kazi ya wizara kwa mwaka 2019/2020.

Kikao hicho kinahudhuriwa na Manaibu Waziri Hussein Bashe na Omary Mgumba, Katibu Mkuu, Mhandisi Mathew Mtigumwe na Naibu Katibu Mkuu Prof. Siza Tumbo.

## KKKT yashauri kozi shahada uzamili uongozi

**Na Romana Mallya**

MSAIDIZI wa Askofu Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Chediel Lwiza, ameishauri serikali, mashirika, taasisi za umma na binafsi kuhakikisha watu wao wanasoma programu ya Shahada ya pili ya uongozi katika utumishi wa watu ili waweze kutatua changamoto za wanaowatumikia.

Askofu Lwiza aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizindua programu hiyo mpya katika Chuo Kikuu Tumaini Kampasi ya Dar es Salaam (Tudarco). Alisema programu hiyo siyo tu itawanufaisha watu wa kanisa, pia kutoka serikalini, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa sababu lengo lake ni watumishi kuwatumikia wananchi kwa kuwawezesha kutoka katika hali walizonazo sasa.

Alisema Shahada hiyo ya pili kwa lugha nyingine 'Utawala wa Diakonia' inalenga kuwatumikia watu na kuisaidia jamii ya kawaida kutoka katika hali walizonazo.

"Malengo siyo kumtumikia mtu bali pia ni kumtoa mtu katika hali ya chini aliyonayo na kumpeleka hali nyingine. Ni aina ya taaluma ambayo itamwezesha yeyote anayeisoma siyo tu kwenda kutumikia watu na kuwaacha na hali zao, ni kuwawezesha kuondokana na hali zao," alisema.

**NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kampuni ya **ANDAN GROUP COMPANY LIMITED kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited** tunatoa Notisi na tangazo la mnada kwa mali zilizowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili,Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada . Mnada utafanyika sehemu dhamana husika zilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| N/S | TAWI HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KAHAMA | MAYALA/MOZES,SAMWEL | MAYALA/MOZES,SAMWEL | NYUMBA | MWENDAKULIMA | 26/9/2019 SAA 4 ASUBUHI |
| 2 | KAHAMA | KADO,KIZITO | KADO,KIZITO | NYUMBA | SEGESE | 26/9/2019 SAA 4 ASUBUHI |
| 3 | KAHAMA | MANG'UNG'ULA/J,FROLIDA | MGEMA/L,PROTUS | NYUMBA | MASUMBWE | 19/9/2019 SAA 4ASUBUHI |
| 4 | KAHAMA | MSAFIRI/S,KAPELA | MSAFIRI/S,KAPELA | NYUMBA | ITWANGI | 20/09/2019 SAA 4 ASUBUHI |
| 5 | KAHAMA | SAIMONI/N,STEVEN | SAIMONI/N,STEVEN | NYUMBA | LUNGUYA | 30/09/2019 SAA 4 ASUBUHI |
| 6 | KAHAMA | PETRO/J,MAKOYE | PETRO/J,MAKOYE | NYUMBA | KAYENZE | 27/09/2019 SAA 4 ASUBUHI |
| 7 | KAHAMA | JULIUS/M,EMMANUEL | JULIUS/M,EMMANUEL | NYUMBA | KAHAMA MJINI | 27/9/2019 SAA 4 ASUBUHI |
| 8 | KAHAMA | CHAPAULINGE/J,DAUD | CHAPAULINGE/J,DAUD | NYUMBA | NYIHOGO | 26/9/2019 SAA 4 ASUBUHI |
| 9 | KAHAMA | KAOZYA/J,PETER | KAOZYA/J,PETER | NYUMBA | SARAWE | 30/9/2019 SAA 4 ASUBUHI |
| 10 | KAHAMA | CHARLES/MASANJA,STEVEN | CHARLES/MASANJA,STEVEN | NYUMBA | ISELAMAGAZI | 30/9/2019 SAA 4 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNAD**

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA UKISHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

**Kwa maelezo na ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na**

**Mratibu wa MIKOPO,**
**AccessBank Tanzania Limited-Makao Makuu**
**S.L.P. 95068,**
**Dar Es Salaam.**
**Simu: 022 2774355, Nukushi: 022 2774340**
**Barua pepe: info@accessbank.co.tz**
**0684078494 - ANDAN GROUP COMPANY LIMITED**

215422102



Wachungaji wakiswaga ng'ombe kwenda malishoni katika kijiji cha Kusenyi, Musoma Vijijini mkoani Mara jana. Kipindi hiki cha kiangazi wachungaji huenda maeneo ya mbali kutafuta malisho. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Costech yaeleza umuhimu ushirikiano watafiti, waandishi

**Na Futuna Seleman**

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Costech) imewataka watafiti nchini kushirikiana na waandishi wa habari kuuhabarisha umma kuhusu masuala mbalimbali ya matokeo ya utafiti wanafanya ili kuwanufaisha wananchi yakiwamo makundi ya wafugaji na wakulima nchini.

Ofisa Mtafiti Kiongozi wa Costech, Dk. Bakari Msangi, aliyesema hayo nyakati tofauti jijini Tanga katika mafunzo ya siku mbili yaliyowakutanisha waandishi wa habari na watafiti ambao pia walitembelea Taasisi za Utafiti wa Mifugo Kilimo na Magonnjwa ya Binadamu (NIMR).

"Shirikianeni kutoa habari na uandikaji utakaoleta tija kwa jamii bila kuwapo na upotoshaji masuala ya utafiti yanatakiwa kuwa na umakini sana waulizeni watafiti ambacho hamjaelewa ili umma unufaike kwa faida ya wote ifahamike tu hamuingiliwi kwenye taaluma yenu ila umakini unahitajika katika kuhabarisha umma," alisema Bakari.

Alisema nchi ina habari nyingi zinazohusu utafiti, lakini zimekuwa haziandikwi ikilinganishwa na habari nyingine zikiwamo za burudani na michezo.

Pia alisema wakati umefika kwa waandishi kujikita kuandika habari za kitafiti na watafiti nao watoe ushirikiano kwa waandishi wa habari wanapohitaji kupata taarifa mbalimbali ili mradi miiko izingatiwe.

"Serikali imekuwa ikitoa fedha kwenye miradi mbalimbali ya kitafiti hivyo lazima utekelezaji wake uonekane kwa kuleta matokeo chanya katika jamii kama ilivyokusudiwa," alisema.

Vile vile, alisema baadhi ya watafiti waliozungumza na Nipashe licha ya kuipongeza serikali kusaidia taasisi mbalimbali za utafiti nchini kutelekeza kazi zake, wameipongeza Costech kuwashirikisha na waandishi wa habari kuwa kitu kimoja katika kuuhabarisha umma kuhusu utafiti wa kisayansi na teknolojia.

Nao baadhi ya waandishi walioshiriki mafunzo hayo, Raisa Said, Gustavus Haule, Haroud Shemsanga, kwa nyakati tofauti walisema wamejifunza umuhimu wa utafiti unaofanywa na watafiti nchini katika kusaidia jamii kuondokana na matumizi ya teknolojia za zamani ili kuendana na wakati na kuahidi ushirikiano baina yao katika kuandika habari hizo kwa umakini.

"Nimejifunza ushirikiano baina yetu na watafiti na umakini wa kuandika habari za utafiti, lakini pia nimefurahi kuona namna utafiti wa kisayansi unavyowasaidia wananchi katika masuala ya ufugaji na kilimo naahidi kuzipa kipaumbele habari za kisayansi zitazowahusisha watafiti ili wananchi waweze kunufaika na matokeo ya tafiti zinazofanywa na watafiti wetu ambazo asilimia 100 zimeonyesha mafanikio makubwa," alisema Haule.

Mafunzo hayo na ziara hiyo iliyojumuisha waandishi kutoka Tanga, Pwani na Morogoro yaliratibiwa na Costech.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA LENYE NYUMBA NDANI LINAUZWA,** Liko eneo la Lumumba Pangani mkoa wa pwani. Lina ukubwa wa heka mbili. Kwa Mawasiliano 0767332830, 0686137871, 0686807366


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHARIFU ABDUL MNOLLA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0432/0144** kilichotolewa na JABAL HIRA SEMINARY mwaka 2003. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MOR/MOR/RB/268481/2019.**

115420102

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARIAM A. JUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1840/087** kilichotolewa na KIMASEKI SEKONDARI mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **AR/RB/0607/2015.**

115420002


## CHETI KIMEPOTEA



**ANNA MYOVELA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Chenye **INDEX NO. S0219-013** kilichotolewa na SONGEA GIRLS SEC. SHOOL, mwaka 1992. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/296704/2019.**

115421302

## VYETI VIMEPOTEA



**ERICK L. LOHAY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0156/0087/2013** kilichotolewa na TANGA TECHNICAL SEKONDARI mwaka 2013. Cheti cha Diploma chenye namba **140126123987** kilichotolewa na Dar es salaam Institute of Technology mwaka 2017. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi IV: **DAR/CHA/RB/296963/2019.** Taarifa ya polisi chuo: **DAR/CHA/RB/296976/2019.**

115420502

## KUPOTEA KWA CHETI



**RACHEL JAMES** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0226/0069** kilichotolewa na KAGUNGULI GIRL'S SEKONDARI mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **AR/RB/10169/2015.**

115420602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TAWAQAL AND CO.LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Tractor Volvo yenye namba za usajili **T. 449 BDE.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **SMT/RB/6866/2019**

115421102

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**WU ZHOU INVESTMENT COMPANY LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **T 778 CES SANLG**. Chassis namba **LBRSPKB52C9003132.** Engine namba **12941478.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAG/RB/3628/2019.**

115420402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ALICE APOLINARY** KUNDI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 348 CTD TOYOTA HARRIER**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: Control No. **991089582890.**

115420202

## Taarifa ya Kufungwa/ Kufutwa kwa Kampuni

**INATOLEWA TAARIFA KUWA** katika mkutano wa ziada wa **SHODEN DATA SYSTEMS (TANZANIA) LIMITED** uliofanyika siku ya 1st day of February 2019, azimio maalum lilipitishwa kwa pamoja na wamiliki/wanahisa wa kampuni la kufunga kampuni kwani haikuweza endelea kufanya shughuli zake.

Ikiwa mtu ana madai yoyote au maslahi dhidi ya kampuni, wanashauriwa kuwasiliana na kampuni kwenye anwani iliyo chini ndani ya siku 7 za taarifa hii.

**Karimjee Attorneys**
**P.O. Box 76421**
**Dar es Salaam.**

115420802

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**STEVEN NGOZI NDAREMYE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 825 ADF.** Aina Yake **TOYOTA MARK II.** Yenye chassis namba **SX805082856** na Engine namba **4S103820.** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MOR/MOR/RB/223598/2019.**

115421402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 64/2019**

**Ombi la ABEDI MZEE HASARA Msimamizi wa Mirathi Marehemu MZEE ABEDI HASARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 30/10/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamni waweza kukaguliwa. Tarehe 10/9/2019

115421202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: CHAMWINO-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 53/2019**

**Ombi la NGALUMA HUSSEIN NGALUMA kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HUSSEN MOHAMED NGALUMA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/09/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 12/07/2019.

115421502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 177/2019**

**Ombi la MWANTUM OMARI MVUNGI NA RASHID MUSSA OMARI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SALUM SAID MGOMBE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/09/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 10/09/2019.

115421602

*The land Disputes Courts (The District land and Housing Tribunal) Regulations GN. No. 174/2003*

**FORM No. 2B**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**

**MAHALI: TEMEKE**

**MAOMBI NA 120 MWAKA 2018**

**FATMA KERMAI..................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MOHAMED IDDY...............MJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: MOHAMED IDDY**

Mdai/wadai amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba dhidi yako/yenu. Shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 14 Mwezi 11 mwaka 2019 saa 3:00 asubuhi mbele ya Mh. AMINA Mwenyekiti wa Baraza. Unatakiwa/mnatakiwa ufike/mfike wewe mwenyewe/nyinyi wenyewe au Wakili wako/wenu, mwakilishi wako/wenu pasipo kukosa na ulete/mlete utetezi wako/wenu ndani ya siku ishirini (21) toka tarehe ya kupokea kuitwa shaurini.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 12 mwezi 09 mwaka 2019.

115421002

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# BENCHI LAMKERA MATIC MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester United, Nemanja Matic amebainisha kwamba, anakerwa na kuwekwa benchi msimu huu.

Matic alianza kwa mara ya kwanza msimu huu 2019-20 wakati United ikiibuka na ushindi dhidi ya Leicester City kwenye mchezo wa Ligi Kuu Jumamosi baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia aliingia kwa sababu ya Paul Pogba kuwa majeruhi hapo Old Trafford, hata hivyo, Matic alicheza kwa dakika 22 tu kwenye mchezo huo dhidi ya Leicester.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer ameamua kuwatumia Pogba na Scott McTominay kwenye safu ya kiungo na Matic amesema: "Bila shaka inanikera na kunichanganya. Nataka kucheza, mara zote najitoa kwa ubora wangu wote kwa timu.

"Kocha ndiye mtu anayechagua timu na unapokuwa kwenye benchi hauwezi kuwa na furaha, lakini nataka kujaribu kushawishi kubadilisha uamuzi wake na kunipa nafasi ya kucheza.

"Msimu ni mrefu. (dhidi ya Leicester) kama ulivyoona nilicheza, na tulishinda mchezo.

"Nina furaha, hivyo tutaangalia kwa siku za usoni nini ambacho kocha ataamua. Nipo tayari. Kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita nimecheza kwenye daraja la juu na kila mchezo nilijaribu kucheza kwa ubora wangu wote kuisaidia timu, sababu nafikiri mimi ni mchezaji wa timu na naweza kuisaidia zaidi."

# Dzeko ambakisha Mkhitaryan AS Roma

**ROME,** Italia

EDIN Dzeko amesema ana matumaini Henrikh Mkhitaryan atabaki AS Roma kwa "muda mrefu" baada ya kufunga bao katika mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu ya Italia Serie A.

Mkhitaryan aliwasili kwenye mji huo mkuu wa Italia kwa mkopo wa muda mrefu akitokea Ligi Kuu ya England katika Klabu ya Arsenal kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili la Ulaya.

Na Mkhitaryan katika mchezo wake wa kwanza kwa Roma alifunga bao katika dakika ya 22 wakati Giallorossi walipowafunga wageni Sassuolo mabao 4-2 Jumapili.

Dzeko, ambaye pia alikuwa kwenye ubao wa wafungaji katika mchezo huo kwenye dimba la Olimpico, alimsifia mchezaji mwenzake huyo baada ya mechi hiyo.

"Nilitarajia hilo kutoka kwake. Namjua kama mchezaji mkubwa, na ni mzuri na yupo kwenye hali nzuri kwenye safu yetu ya ushambuliaji ambaye anataka kucheza soka," alisema Dzeko.

"Nina uhakika kwa asilimia 100 atakwenda kutusaidia sisi. Nina uhakika nilikuwa na furaha kuona usajili wake unatokea.

"Baada ya kuzichezea timu zetu za taifa na alifunga bao dhidi yetu, nilimuambia 'rafiki yangu, mchezo unaofuata unatakiwa kuifungia pia Roma'

"Ni mchezaji wa kiwango cha juu. Namkumbuka pia wakati akiwa Borussia Dortmund na atakuwa mchezaji mkubwa kwetu. Matumaini yangu atabakia hapa kwa muda mrefu."

Roma haijafungwa katika mechi tatu chini ya kocha, Paulo Fonseca – imepata ushindi mmoja na sare mbili ikipitwa pointi nne na vinara Inter Milan.





# *Giampaolo aitaka Milan kushambulia kama nyuki*

**MILAN,** Italia

KOCHA wa AC Milan, Marco Giampaolo ameeleza "vitu" vya kuvifanyia kazi kwenye kikosi chake baada ya kuishuhudia wakiifunga Verona bao 1-0 kwenye mchezo ambao umemuacha afanye tathimini ya kuimarisha safu ya ushambuliaji ya Rossoneri hao.

Matokeo ya mchezo huo yaliamualiwa na penalti ya Krzysztof Piatek ya kipindi cha pili, ambapo ilipatikana baada ya mchezaji wa Verona, Mariusz Stepinski kutolewa nje kabla ya Davide Calabria kupewa nafasi ya kuipiga na Giampaolo akabainisha ushindi huo ulikuwa mwembamba.

Aliinyoshea kidole safu ya ulinzi ya Verona na kusema kwamba ilicheza vizuri na ndio sababu ya wao kuwa na wakati mgumu wa kupata mabao na kubainisha kuwa kikosi hicho ambacho alikirithi kutoka kwa mtangulizi wake, Gennaro Gattuso, hakikucheza kwa umoja.

"Timu inafanya vizuri, tunatafuta uwiano na najua kuna sehemu ziko imara na nyingine dhaifu, lakini nafanyia kazi kuwaimarisha mchezaji mmoja mmoja na timu yote kwa ujumla," alisema Giampaolo akiiambia Sky Sport Italia.

"Kila mmoja ana uimara wake na udhaifu; hakuna timu ambayo ipo bora kila sehemu. Napenda jitihada na ari walioionyesha kwenye mchezo, lakini makosa yanatokea.

"Timu ambayo ina wachezaji 10 katika robo ya mwisho ya mchezo

## HABARI MICHEZO

# Bayern majanga, Alaba aumia paja

**MUNICH,** Ujerumani

DAVID Alaba anatarajia kukosa mwanzo wa kampeni ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wa Bayern Munich baada ya kuumia paja la mguu wake wa kushoto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, aliumia wakati akijinoa kabla ya Bayern kutoka sare ya 1-1 na RB Leipzig Jumamosi.

Jerome Boateng alichukua nafasi yake ya kuanza kwenye kikosi cha kwanza, huku Lucas Hernandez akipelekwa kucheza beki ya kushoto.

Bayern haijathibitisha muda wa Alaba kurudi dimbani, lakini kocha, Niko Kovac hataweza kumtumia kwenye mchezo wa kwanza wa makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano dhidi ya Red Star Belgrade.

"Bayern itakuwa bila David Alaba baada ya kuichezea nchini yake ya Austria na alijitonesha wakati wa mazoezi kuelekea mchezo wa Jumamosi wa Bundesliga dhidi ya RB Leipzig," klabu hiyo imethibitisha katika taarifa yake.

Akiwa amehusishwa na mpango wa kwenda Barcelona wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto, Alaba ameanza katika kila mchezo wa ufunguzi kati ya mitatu ya Bayern ukiwamo ule wa ushindi wa 6-1 dhidi ya Mainz mwezi uliopita.



# MARADONA ARUDI UKOCHA KWA KIPIGO



**BUENOS AIRES,** Argentina

MCHEZO wa kwanza wa Diego Maradona akiwa anarudi tena kwenye ukocha katika klabu ya Gimnasia y Esgrima La Plata ya hapa Argentina ulimalizika kwa kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Racing Club.

Gwiji huyo mwenye umri wa miaka 58, aliteuliwa na klabu hiyo ya Superliga Septemba 5, mwaka huu baada ya muda mfupi kuwa nje ya mchezo huo kutokana na matatizo ya kiafya.

Hiyo ilikuwa ni kazi ya kwanza kwa gwiji huyo wa Argentina kuinoa timu katika ardhi ya nyumbani kwake tangu mwaka 2010 alipoinoa timu ya taifa.

Racing ambao ni mabingwa watetezi wa ligi walipata ushindi huo kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Juan Carmelo Zerillo.

Ariel Matias Garcia alisawazisha bao la Diego Gonzalez la kipindi cha kwanza na kuwapa matumaini vijana hao wa Maradona kubakia na pointi, lakini bao la Matias Zaracho la dakika ya 54 likafuta kabisa matumaini hayo.

Baada ya mchezo huo, Maradona alisisitiza kwamba kikosi chake kilikuwa imara na kilistahili kupata pointi.

"Tulikuwa tunapigania kusawazisha. Vitu kama hivi vinatokea kwenye soka na unatakiwa kufunga ukurasa na kuendelea na mwingine," alisema.

"Moyo wangu unaniuma kwa sababu nafikiri mabingwa wa Argentina walikuwa bora kushinda sisi. Hakuna muda, sisi tulionyesha ubora wetu.

"Lakini wana wachezaji wenye ubora ambao wanacheza soka kwa kasi muda wote na kusukumiza mashambulizi mbele."

# *Mane: Kuhusu Salah? Tushamalizana mbona*

**LIVERPOOL,** England

SADIO Mane amesisitiza 'bifu' yake na Mohamed Salah imeshasahaulika baada ya kubwatuka kwa ghadhabu wiki mbili zilizopita.

Mshambuliaji huyo wa Liverpool alionyesha hasira kwa Salah kwa kushindwa kumpasia mpira wakati wakiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Burnley Agosti 31, mwaka huu.

Baada ya kutolewa nje, mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal alitupa jezi yake ya mazoezi sakafuni na kuonyesha ishara dhidi ya wachezaji wenzake, lakini amesafisha hali ya hewa kupitia kituo cha televisheni cha Canal+ kwamba wameshazika tofauti zao.

Alisema: "Kuhusu Salah? Imeshasahaulika.

"Kuna wakati unatakiwa kuzungumza vitu ana kwa ana. Hivi ni vitu vinavyotokea kwenye soka.

"Lakini tumeyamaliza na kubakia kuwa marafiki wazuri kama ilivyokuwa hapo kabla."

Mane, ambaye alifunga mabao mawili kwenye ushindi wa 3-1 wa Wekundu hao dhidi ya Newcastle Jumamosi, sasa ana mabao sita katika mechi sita msimu huu, wakati Salah ana mabao manne katika mechi saba.






# XHAKA: WOGA UMEIUA ARSENAL KWA WATFORD

## ●●● Hakuna aliyehitaji mpira, tulijificha kukwepa pasi, tunashukuru kupata...

**LONDON,** England

NAHODHA wa Arsenal, Granit Xhaka, amekiri kuwa kikosi chao hakikutulia kiakili vya kutosha na woga ndiyo uliyochangia kuruhusu wapinzani wao, Watford kutokea nyuma wakiwa wamelala kwa mabao mawili na kupata sare ya 2-2.

**'Gunners' walionekana kuutawala mchezo huo wa Ligi Kuu England juzi, Jumapili uliopigwa katika Uwanja wa Vicarage Road baada ya Pierre-Emerick Aubameyang kutupia mara mbili katika tofauti ya muda wa dakika 11 kwenye kipindi cha kwanza.**

Lakini Tom Cleverley alirudisha bao moja mapema kipindi cha pili kufuatia pasi fyongo kutoka kwa Sokratis na mtokea benchi Roberto Pereyra akasawazisha kwa mkwaju wa penalti dakika tisa kabla ya kipenga cha mwisho baada ya kuangushwa ndani ya eneo la hatari na David Luiz.

Na mwishoni Arsenal ilipaki 'basi' kupigania kupata pointi moja na Xhaka anakiri "walikuwa na hofu sana", wakati pia akiwatuhumu wachezaji wenzake kwa kujificha.

"Tumekatishwa tamaa sana. Tulikuwa na kipindi kizuri cha kwanza na kisha tulitokea nje na kucheza vibaya sana katika kipindi cha pili na tukaadhibiwa kwa hilo," aliiambia BBC Sport.

"Tulijua hawakuwa na la kupoteza na wangekuja kwetu, lakini hatukuonyesha mchezo wetu. Tulikuwa waoga sana. Hakuna aliyehitaji mpira.

"Kila timu kwenye Ligi Kuu England ni imara vya kutosha kufunga hivyo unapaswa kuwa mpole, kuwa imara kiakili na hatukuwa hivyo."

Arsenal walikuwa wasanifu kwa kushindwa kwao wenyewe kufuatia Sokratis kutoa 'boko' kwa Watford kupata bao la kwanza kutokana na mfumo wao wa kuanzia mpira nyuma, licha ya kuhimili kipindi cha kwanza.

Xhaka, ambaye anatarajiwa kutangazwa nahodha wa kudumu wa Arsenal wiki hii, aliiambia Sky Sports: "Makosa yanatokea lakini si msamaha.

"Wakati mwingine tunapaswa kuwa bora. Haikuwa katika hali kama hii tu tuliyopoteza mchezo. Tumepoteza mchezo wote kipindi cha pili.

"Unapaswa kusema tuwenye furaha kupata pointi.

"Tulijua watakuja sana kwetu na kutusukuma sana kurudi nyuma, lakini tulipaswa kuonyesha uimara sana na si kuogopa.

"Tumezungumza hukusu hilo. Hatuwezi kupoteza kiwango kama hivi kipindi cha pili."

Arsenal itasafiri kuelekea Ujerumani kuifuata Eintracht Frankfurt kwenye mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya Europa League itakayopigwa Alhamisi kabla ya kurejea kwa mechi ya Ligi Kuu England nyumbani dhidi ya Aston Villa Jumapili ijayo.

## ZISIKUPITE

### KLOPP, VAN DIJK LULU HISPANIA

REAL Madrid na Barcelona wanajiandaa kwenda uso kwa uso kutoa ofa ya kumnasa kocha Jurgen Klopp na beki Virgil van Dijk, 28, kutoka Liverpool. ***(AS, via Star)***

### DE GEA KUFUNIKA EPL

MANCHESTER United imetoa ofa kwa kipa Mhispania David de Gea, 28, ya kumfanya kuwa mchezaji anayelipwa zaidi Ligi Kuu England lengo likiwa ni kumshawishi kusaini mkataba wa muda mrefu. ***(Times)***

### ERIKSEN BADO AITESA SPURS

KIUNGO Christian Eriksen, 27, amekuwa akitolea nje kila ofa mpya ya mkataba anayopewa Tottenham, lengo likiwa ni kuwezesha mpango wake wa kwenda kujiunga na Real Madrid majira ya joto yajayo. ***(Express)***

### HAZARD AMTAKA KANTE REAL

MSHAMBULIAJI Eden Hazard, 28, na kipa Thibaut Courtois, 27, wanamtaka Mfaransa N'Golo Kante kujiunga naye Real Madrid baada ya kiungo huyo wa Chelsea, 28, kuhusishwa na kutimkia Hispania. ***(Sun)***

### KROOS CHAMBO YA POGBA

REAL Madrid wanaweza kumtoa kiungo Mjerumani Toni Kroos, 29, kwa Manchester United kama sehemu ya kubadilishana kumpata kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26. ***(FourFourTwo)***

### ARSENAL MGUU SAWA KWA PYE

ARSENAL inajiandaa kushinda mbio za kuinasa saini ya kinda wa Sunderland, Muingereza Logan Pye baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 15, kuhusishwa na kukipiga Ligi Kuu majira ya joto. ***(Sun)***

### MATIC MTEGONI JUVENTUS

KIUNGO wa Man United, Nemanja Matic, 31, anawindwa na Juventus kuelekea usajili wa Januari. ***(Mirror)***

### ABRAHAM AIFIKIRIA NIGERIA

STRAIKA wa Chelsea, Tammy Abraham, 21, bado hajaweka kando uwezekano wa kuichezea Nigeria badala ya England. ***(Times)***

### MANE, SALAH WASULUHISHWA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Sadio Mane, 27, alikasirika wakati mchezaji mwenza Mohamed Salah, 27, alimpotezea kumpa pasi kwenye mechi dhidi ya Burnley lakini amesema suala hilo "limeshamalizika" na wawili hao "wameshasuluhishwa". ***(Canal+, via Star)***

### AMTAJA GRACIA WATFORD

KOCHA Unai Emery amefunguka kuwa alikuwa pamoja na Javi Gracia wakati Watford ilipomtimua. ***(Metro)***

### NEVILLE NA MZUKA KUINOA UTD

NGULI wa Manchester United, Gary Neville amesema "atatembea maili moja" kama anepewa ofa ya kuinoa miamba hiyo ya Old Trafford. ***(Manchester Evening News)***

### YAKOMAA NA AINSWORTH

LINCOLN City imefungua milango upya ya mazungumzo na kocha wa Wycombe Wanderers, Gareth Ainsworth baada ya kuikataa ofa ya awali ya kuinoa. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

## Kocha Malindi alia na mastraika

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya timu yake kufungwa mabao 4-1 na Al Masry kutoka Misri, Kocha Mkuu wa Malindi FC, Mohammed Machupa, amesema "kichapo" hicho walichopokea hakimaanishi kuwa kikosi chake ni dhaifu.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Machupa, alisema timu yake ilicheza vizuri katika kipindi cha pili, lakini washambuliaji wake walishindwa kutumia vema nafasi ambazo walizitengeneza.

Machupa alisema soka ni mchezo wa makosa, na hali hiyo ilitokea kwa wachezaji wake katika kipindi cha kwanza na kusababisha kupata kichapo hicho.

"Timu yangu ilijitahidi kucheza vizuri katika kipindi cha pili, lakini walishindwa kutumia vizuri nafasi walizokuwa wakizipata, hali hii ilisababisha tushindwe kurudisha mabao kama ambavyo wenzetu walifanikiwa kutumia nafasi walizopata," alisema Machupa.

Kocha huyo alisema wachezaji wake walicheza kwa hofu katika kipindi cha kwanza, lakini walipofunga bao, walianza kuimarika na kuonyesha wanaweza kupambana na kutafuta mabao mengine zaidi.

Bao pekee la Malindi katika mchezo wa juzi lilifungwa na Ibrahim Ali wakati waliopachika kwa upande wa wageni hao walikuwa ni Mahmoud Wadi aliyefunga mawili, Hassan Ibrahim na Saiduu Simpory.

## Maxime afunguka uzoefu umewabeba

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema uzoefu na umakini ndio umeisaidia timu yake kupata ushindi katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Alliance FC uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Katika mechi hiyo ya juzi, Kagera Sugar ilipata ushindi wa mabao 2-1 na kufikisha pointi sita sawa na vinara wa ligi hiyo, Simba, Lipuli FC ya Iringa na Namungo FC ya mkoani Lindi.

Akizungumza na gazeti hili, Maxime, alisema wachezaji wake walipambana kuhakikisha wanapata ushindi, na haikuwa kazi rahisi kwa upande wao kuvuna pointi hizo tatu.

Maxime alisema ushindani umeongezeka zaidi katika msimu huu kutokana na kila timu kujiimarisha kwa kusajili wachezaji wenye uwezo na kufanya maandalizi yanayotakiwa.

"Haikuwa kazi nyepesi, mechi ilikuwa na ushindani sana, lakini wachezaji wangu walipambana, ili upate ushindi, ni lazima uonyeshe vitu tunavyovifanyia mazoezi katika mechi, ushindani ni mkubwa sana msimu huu, timu zote zinaonekana zimejiandaa," alisema Maxime.

Naye Kaimu Kocha Mkuu wa Alliance FC, Kessy Mziray, amesema kuwa umaliziaji mbovu ndio uliochangia kikosi chake kishindwe kufanya vema katika mchezo huo wa raundi ya pili wa ligi hiyo ya juu nchini.

# WACHEZAJI AZAM WAAHIDI KUPINDUA MEZA ZIMBABWE

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya timu yao kupoteza mechi ya kwanza ya raundi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, wachezaji wa Azam FC wamesema kuwa watahakikisha "wanapindua meza" katika mchezo wa marudiano dhidi ya Triangle United utakaochezwa nchini Zimbabwe.

**Azam FC juzi ilifungwa bao 1-0 na wageni hao na inahitaji ushindi wa kuanzia mabao 2-0 katika mchezo wa marudiano ili iweze kusonga mbele katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).**

Akizungumza na gazeti hili jana, mshambuliaji, Obrey Chirwa, alisema matokeo waliyopata katika mchezo huo wa kwanza hayajawakatisha tamaa na wanaahidi watajituma ili kuhakikisha wanashinda katika mchezo wa marudiano na hatimaye kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Chirwa alisema mchezo huo wa juzi ulikuwa mgumu, lakini sasa tayari wameshawasoma wapinzani wao.

"Mchezo ulikuwa mgumu, tulijitahidi kupambana lakini haikuwa siku yetu nzuri, tutajipanga kuhakikisha mchezo ujao tunafanya vizuri ili timu yetu ifike mbali, tunazidi kuomba ushirikiano kutoka kwa mashabiki wetu," alisema Chirwa.

Naye kiungo wa timu hiyo, Frank Domayo, aliliambia gazeti hili kuwa watajipanga vizuri kwa ajili ya mechi ijayo na anaamini benchi la ufundi litayafanyia kazi upungufu walioubaini ili waweze kupata ushindi huko ugenini.

"Tumetengeneza nafasi, lakini hatujazitumia, tumemaliza dakika 90 za kwanza, tumebakiwa na dakika nyingine 90 za ugenini, tulijituma kadri ya uwezo wetu ili kupata ushindi, lakini bahati haikuwa upande wetu," alisema kiungo huyo wa zamani ya Yanga, Domayo.

Aliongeza kuwa kila mchezaji anaahidi kujituma ili waweze kuipeperusha vema bendera ya Tanzania pamoja na kutomwangusha kocha wao Mrundi Etienne Ndayiragije.




Mkuu wa Kombania ya Muziki, Meja Nimroad Kitinya, akipokea udhamini wa jezi kutoka kwa Mwakilishi wa Smart Gin, Forgiver Tito, wakati wa sherehe ya uzinduzi wa jezi mpya za Timu ya Green Warriors, inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza katika hafla iliyofanyika Club 361 Mwenge jijini Dar Es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mchenga, Dribllers kazi ipo nusu fainali*

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa michuano ya Sprite Bball Kings, Mchenga Bball Stars watakutana na Flying Dribllers katika hatua ya nusu fainali ya Sprite Bball Kings 2019 baada ya droo ya hatua hiyo kupangwa jana jijini Dar es Salaam, mchezo ambao utakumbushia fainali ya msimu uliopita.

Mchenga, mabingwa mara mbili mfululizo wamefanikiwa kutinga hatua hiyo baada ya kuwafunga TMT katika robo fainali iliyochezwa Jumapili katika Uwanja wa Ndani wa Taifa kwa vikapu 91- 67 huku Flying wakiwanyuka Dream Chasers kwa vikapu 90-77.

Akizungumza mara baada ya droo hiyo kupangwa, Kocha wa Mchenga, Mohamed Yusuph, alisema amefurahia kuona anapangwa na timu ambayo amecheza nayo katika misimu yote ya michuano hiyo na anaamini watapata upinzani lakini timu yake itaandika historia ya kucheza fainali nyingine.

Kwa upande wa nahodha wa Flying, Hebilmana Mayeye, alisema timu yao imejifunza kutokana na makosa hivyo ni muda muafaka wa kulipa kisasi kwa mchenga ambao wamekuwa wakiwapa wakati mgumu katika mechi zao walizokutana.

Mechi nyingine ya nusu fainali itazikutanisha Tamaduni dhidi ya KG Dallas.

Tamaduni imetinga hatua hiyo baada ya kuinyuka Ukonga Hitmen kwa alama vikapu 102-67 huku KG Dallas wakifika nusu fainali kwa kuitandika Water Instiitue kwa vikapu 91-84.

Mechi hizo za nusu fainali zitaanza kupigwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Ndani wa Taifa kuanzia saa kumi jioni ambapo Tamaduni na KG Dallas zitaanza kucheza na baadaye Mchenga Bball Stars itashuka dimbani dhidi ya Flying Driblers.

Mechi za pili zitapigwa Jumatano Septemba 25, mwaka huu katika Uwanja wa Don Bosco Oysterbay na endapo matokeo yatakua sare basi mechi za mwisho zimepangwa kupigwa septemba 28 katika viwanja vya Don Bosco.

# Michezo

Jumanne Septemba 17, 2019

Nipashe




Xhaka: Woga umeiua Arsenal kwa Watford

UKURASA 30

PENALTI?...



Beki wa Kati wa Arsenal, David Luiz, akimchezea madhambi mshambuliaji wa Watford, Roberto Pereyra, kwenye mstari wa 18 ambapo mwamuzi aliamuru ipigwe penalti iliyozamishwa kimyani na mchezewa madhambi huyo, hivyo kufanya matokeo kuwa 2-2 katika mechi hiyo ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Vicarage Road juzi. **HABARI UK.30**

## Miraji, Makame ndani Taifa Stars

**Na Somoe Ng'itu**

MSHAMBULIAJI wa Simba, Miraji Athumani na kiungo wa Yanga, Abdul-Aziz Makame, wameitwa katika kikosi cha wachezaji 25 wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo itajiandaa na mchezo wa kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) dhidi ya Sudan.

Taifa Stars inatarajia kuikaribisha Sudan katika mchezo wa kwanza wa mashindano hayo ya kimataifa utakaochezwa Septemba 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na marudiano yakipangwa kufanyika Khartoum baada ya wiki moja.

Kocha wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, aliwataja wachezaji wengine watakaojiandaa kwa ajili ya mchezo huo kuwa ni pamoja na Juma Kaseja, Metacha Mnata, Said Kipao, Haruna Shamte, Boniface Maganga, Gadiel Michael, Mohammed Hussein "Zimbwe Jr", Kelvin Yondani, Erasto Nyoni, Iddy Mobi na Bakari Nondo.



Ndayiragije pia amewaita Jonas Mkude, Baraka Majogoro, Mohammed Issa, Iddi Suleiman "Nado", Mudathir Yahya, Salum Ablubakar "Sure Boy", Frank Domayo, Mzamiru Yassin, Shaaban Iddi, Ayoub Lyanga, Hassan Dilunga "HD" na Feisal Salum.

Stars ilisonga mbele katika mashindano hayo baada ya kuwaondoa majirani zao Harambee Stars ya Kenya kwa penalti 4-2.

Kikosi hicho cha Ndayiragije anayesaidiwa na Juma Mgunda pamoja na Suleiman Matola kitawavaa Sudan huku kikiwa na kumbukumbu ya kuwaondoa Burundi na kutinga hatua ya makundi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika Qatar mwaka 2022.

# Yanga waifuata Zesco mapema

**Na Shufaa Lyimo**

### ●●● Mbinu zilezile za Township Rollers kutumika kumalizia kazi Zambia, uongozi wafunguka kuwa...

HAKUNA kulala! Baada ya kukubali kutoka uwanjani na sare ya bao 1-1, Jumamosi iliyopita katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika kwenye mechi ya mkondo wa kwanza dhidi ya Zesco United, kikosi cha Yanga jana kimeendelea kufanya mazoezi ya nguvu kwenye Uwanja wa Polisi Chang'ombe kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wao wa marudiano, ambao utachezwa nchini Zambia Septemba 27, mwaka huu.

**Aidha, kimepanga kuwafuata wapinzani wao hao mapema kama ilivyokuwa dhidi ya Township Rollers ya Botswana ili kuzoea mazingira mapema, hata hivyo kwa Zesco itakuwa wiki moja kabla ya mchezo.**

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa kikosi hicho, Hafidh Saleh, alisema wachezaji wanaendelea vizuri kwa ajili ya mchezo huo na kila kitu kinakwenda sawa.

"Tunashukuru kikosi chetu kinaendelea vizuri kwa ajili ya mchezo wa marudiano ambao tutakuwa ugenini," alisema Hafidh.

Alisema Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera amesema anayafanyia kazi makosa machache ya kiufundi aliyoyabaini katika mchezo uliopita, ili yasijitokeze katika mechi ijayo.



Kwa upande wa Mwenyekiti wa klabu hiyo, Mshindo Msolla amesema hajafurahishwa na matokeo walitoyapata na kudai bado hawajakata tamaa ya kusonga mbele na kuingia kwenye hatua ya makundi.

Mwenyekiti huyo alisema, timu hiyo itafanya mazoezi wiki moja jijini Dar es Salaam, na kuondoka siku saba kabla ya mchezo kwa ajili ya kwenda kuzoea mazingira ya pamoja na hali ya hewa ya Zambia.

"Tutaondoka wiki moja kabla ya mchezo kuelekea Zambia kwa ajili ya kupeleka wachezaji wetu wazoee hali ya hewa nchini humo," alisema Msolla.

Aliwataka Watanzania wasikatishwe tamaa na matokeo yaliyopita, na kuwataka kuendeleza ushirikiano kama walivyowafanyia kwenye michezo iliyopita.

Yanga ilipata sare ya bao 1-1 Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, na kwa matokeo hayo inahitaji juhudi ya ziada katika mchezo huo. Ili kusonga mbele, Yanga inahitaji sare ya zaidi ya mabao mawili au ushindi.

Endapo Yanga itatolewa itaangukia kucheza mechi moja ya mchujo na timu zitakazovuka raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho, na endapo itapata matokeo ya jumla, itashiriki michuano hiyo ya shirikisho ambayo ni ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani humu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >